Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TAZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Thelathini – Tarehe 23 Julai, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 267

**Dhamira ya Kuwasomesha Watoto Yatima**

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali katika matamshi yake mbalimbali imeonesha dhamira ya kuwasomesha watoto yatima kwa gharama zake yenyewe:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kupata takwimu sahihi za watoto yatima wanaostahili kupewa msaada huo?

(b) Je, ni watoto yatima wangapi wa Wilaya ya Dodoma Mjini walionufaika na msaada huo kwa mwaka 2007?

(c) Je, ni watoto yatima wangapi wa Wilaya ya Dodoma Mjini walishindwa kuendelea na masomo ya kidato cha kwanza kutokana na kukosa msaada kama huo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI – MHE. GAUDENTIA M. KABAKA** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, jukumu la kubaini na kuteuwa wanafunzi wanaogharimiwa Elimu ya Sekondari na Wizara, ni la Halmashauri za Wilaya husika. Halmashauri kwa kutumia Uongozi wa Serikali za Vijiji/Mtaa, Kata hadi Wilaya, hubaini watoto wanaotoka katika familia zenye kipato duni wakiwemo watoto yatima ambao hawana njia yoyote mbadala ya kuipata Elimu ya Sekondari bila msaada wa Serikali. Mchakato huu wa kuwapata watoto wanaostahili kulipiwa unawezesha kupata takwimu sahihi za wanafunzi wanaostahili kusaidiwa.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2007, wanafunzi 215 kutoka familia zenye kipato duni wakiwemo watoto yatima kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma walituma maombi ya kusomeshwa. Wanafunzi 101 kati ya hao walipata nafasi ya kulipiwa na Wizara na 114 wanalipiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma.

(C) Mheshimiwa Spika, hakuna wanafunzi kutoka mazingira magumu na familia duni wakiwemo yatima waliokosa fursa ya kulipiwa karo katika Wilaya ya Dodoma Mjini.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ambayo kwa kweli yanaonesha jinsi gani Serikali inawajali watoto yatima.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kabla mtoto yatima hajaweza kufika Kidato cha Kwanza ambapo ndio Serikali inatoa msaada, inabidi asome shule ya msingi na kwa sababu ndio wakati ambao huwa unakuwa ni mgumu sana kwao, pamoja na kwamba elimu ya msingi ni ya bure lakini kuna mahitaji muhimu hasa ya *uniform*, je, Serikali haioni umuhimu wa kuwasaidia hawa watoto yatima katika hatua hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI – MHE. GAUDENTIA M. KABAKA:** Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya shule za msingi, kwanza kama alivyokiri, elimu hutolewa bure. Kutakuwa na michango midogomidogo kama hiyo ya *uniform,* ambayo katika ngazi hiyo, wazazi, familia pamoja na mashule, wanaweza wakazungumza na wakafikia muafaka. Kwa hiyo, kwa kuwa sio ya gharama kubwa, haina haja ya Wizara ya Elimu kuingilia kati katika hilo suala.

Na. 268

**Elimu ya Stadi za Kazi**

**MHE. SAID AMOUR ARFI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Elimu ya kujitegemea itasaida sana watoto kujua angalau stadi mojawapo ya kumsaidia kujiajiri hivyo kumpunguzia ukali wa maisha kwa kulima bustani, kufuma, na kadhalika:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwafundisha stadi za maisha watoto wanaomaliza Elimu ya Msingi?

(b) Kwa kuwa, watoto wengi wanaomaliza elimu ya msingi wana umri wa miaka 13, je, watoto hao wanaandaliwa vipi ili waweze kujiajiri katika umri huo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI – MHE. GAUDENTIA M. KABAKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa elimu ya kujitegemea inamsaidia sana mtoto kujua stadi mbalimbali katika maisha na hatimaye watoto wengi kujiajiri. Hivi sasa Serikali, inawapa mafunzo juu ya stadi za maisha watoto kupitia somo la Stadi za Kazi katika shule za msingi ambapo hufundishwa stadi mbalimbali za maisha.

Mheshimiwa Spika, mara wanapohitimu masomo yao ya elimu ya msingi, watoto ambao hawakuchaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari, wanayo fursa ya kujiunga na vituo vya ufundi stadi ili kujiendeleza na kujipatia taaluma zaidi za kimaisha kama vile umakenika wa magari, ufundi uashi, upishi, ufundi umeme, ushonaji, useremala na kadhalika kupitia Vyuo vya Ufundi Stadi vya Serikali vilivypo. Aidha, Serikali ina mpango wa kuanzisha Vyuo vya Ufundi vya *VETA* katika kila Wilaya ili kuwasaidia vijana kuendelea na mafunzo ya stadi mbalimbali yatakayowasaidia kujiajiri na kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 1995, umri wa kumuandikisha mtoto kuanza darasa la kwanza ni miaka saba, hivyo ni dhahiri kuwa anapohitimu darasa la saba huwa ametimiza umri wa miaka 13. Umri huo ni mzuri na unamuwezesha mtoto kupokea mafunzo ya stadi mbalimbali za maisha ambazo ni msingi wa maandalizi ya kujitegemea na kujiajiri.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nakubaliana naye kwamba stadi za maisha zinafundishwa shuleni kwa nadharia katika shule za msingi na si vitendo kama ilivyo katika shule za sekondari ambapo wanafundishwa nadharia bila kuwepo maabara za wanafunzi kujifunzia na hili ni tatizo katika kuwandaa watoto hasa kuanzia elimu ya msingi mpaka kufikia vyuo vikuu, je, sasa Wizara itakuwa tayari kuanzisha Mjadala wa Kitaifa wa kuangalia mustakabali wa maendeleo ya elimu katika nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI – MHE. GAUDENTIA M. KABAKA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nisaidie kutofautisha kati ya stadi za maisha na stadi za kazi. Anachoulizia Mheshimiwa Arfi, ni stadi za kazi ambazo vijana hujifunza kwa vitendo na kwa nadharia, ndio masomo niliyoyataja katika jibu langu la msingi. Kwa kweli, sasa hivi katika vyuo vyetu vya *VETA*, tumepata msaada wa vifaa vingi sana ingawa bado kuna vyuo ambavyo havina vifaa. Stadi za maisha ni masuala au ni elimu inayomsaidia mtoto kujitambua, kujielewa, kujiheshimu, kujiamini, ambavyo vyote tunaviunganisha katika masomo yetu ya *VETA* na katika vyuo vyetu vya ufundi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Mjadala wa Kitaifa, naomba nilitambulishe Bunge lako kwamba tuko katika harakati za kuhuisha sera yetu ya elimu na katika mambo ambayo tutafikiria ni masuala ya elimu ya msingi lakini pia na masuala ya elimu ya sekondari na kama wengine wanavyoomba sasa kwamba elimu ya msingi haitoshi, basi elimu ya *compulsory* iwe ni elimu ya sekondari itaangaliwa. Kwa hiyo, yote hayo tutayazungumzia na itakapokuwa imefikia hatua ya kuwapelekea wadau, basi hapo tutamuomba Mheshimiwa Arfi, ashiriki katika kutoa mawazo yake.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, umri wa kumaliza darasa la saba ni miaka 13 au miaka 14, ambapo vijana hawa wengi wanakuwa ni wadogo, je, kwa wale ambao hawakufaulu kwenda *Form One,* isingekuwa ni vizuri Serikali ikawandaalia kwa mwaka mmoja au miaka miwili wabaki pale shuleni kwa kufanya hizo shughuli za stadi au pengine kuiendeleza elimu hadi darasa la 10?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI – MHE. GAUDENTIA M. KABAKA:** Mheshimiwa Spika, nimejibu katika swali la msingi kwamba wanafunzi hawa wanapomaliza elimu ya msingi wakiwa na miaka 13 masomo tunayowaandalia kwanza ni yale yanayopatikana katika maeneo yao wanayoishi katika mazingira yao ili yawaandae kuishi maisha ya maeneo yale, kama ni wavuvi, wakulima au wafugaji. Umri wa miaka 13 unatosha kujifunza masomo hayo. Lakini vilevile, nimesema tunahuisha Sera yetu ya Elimu, kwa hiyo, mawazo anayoyatoa Mheshimiwa Mbunge, tunayakaribisha na mwisho wa siku tutaona ni yapi yanafaa katika kuwaandaa vijana wetu wanaomaliza elimu ya msingi.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa, ni zamu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Lakini kabla hatujaendelea, napenda mtambue kwamba leo Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, amewekwa mstari wa mbele, sijui ni dalili njema au vipi? Lakini ... *(Makofi/Kicheko)*

Swali, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi linaulizwa na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, wa Kasulu Mashariki.

Na. 269

**Mkoa wa Kigoma na Wakimbizi**

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO** Aliuliza:-

Kwa kuwa, Mkoa wa Kigoma kwa takribani miaka 40, umekuwa ukipokea wakimbizi kutoka Burundi, Rwanda, Kongo *DRC* na Somalia; na kwa kuwa, Serikali pamoja na Jumuiya za Kimataifa kupitia Shirika la Kimataifa na *UNHCR*, imekuwa ikitoa misaada kwa wananchi ambayo haitoshi ikilinganishwa na shida na madhara makubwa ambayo wananchi wa Kongo wameyapata kwa kipindi chote hicho:-

(a) Je, kwa nini Serikali kwa kushirikiana na jumuiya ya Kimataifa kupitia Shirika la *UNHCR* isijenge/kuweka kitu kitakachobaki kama kumbukumbu za kudumu kwa wananchi wa Kigoma kama vile, Kitivo cha Chuo Kikuu, barabara ya lami Kigoma – Kasulu – Kibondo, Nyakanazi, Hospitali ya Rufaa, hata mashamba makubwa ya miti kufidia miti mingi inayokatwa na wakimbizi hao?

(b) Kwa kuwa, mradi wa *Refugee Host Area Project* una *impact* ndogo sana kwa wananchi na ni wa muda mfupi hadi 2009; je, Serikali inasema nini juu ya kuongeza ushawishi kwa nchi marafiki kama Denmark, kupitia Shirika lake la *DANIDA* kuendelea na mradi huo angalau kwa miaka mitano zaidi hadi 2014?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Nsanzugwanko, kwa ruhusa yako naomba kwa niaba ya Wabunge wote wa Kagera, nichukue fursa hii nikushukuru na niishukuru Ofisi yako, nimshukuru Waziri Mkuu, nimshukuru Mheshimiwa Hamad Rashid na Wabunge wote kwa mkono mliotupa kwa msiba uliomkuta Mbunge mwenzetu kutoka Kagera, Mheshimiwa Sevelina Mwijage. Naomba nitoe shukrani za dhati kutoka kwa Wabunge wote wa Kagera, lakini pia tutoe shukrani kwa Mkuu wa Mkoa, Enock Mfuru, kwa kazi kubwa aliyoifanya kule pamoja na Mheshimiwa Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Bukoba, Mzee Lungisa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Nicodem Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa Serikali na Shirika la *UNHCR* mara baada ya makambi kufungwa, hukabidhi rasilimali zote na miundombinu kwa uongozi wa Serikali ya Mkoa. Serikali ya Mkoa kwa kushirikiana na Halmashauri husika, hupanga namna bora ya kutumia rasilimali hizo na niundombinu hiyo ikiwemo majengo ya shule, zahanati, vituo vya afya, vyanzo vya maji, visima na miradi ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa rasilimali hizo na miundombinu hukabidhiwa kwa uongozi wa Mkoa ambao nao hukabidhi kwa Halmashauri ambayo ndiyo yenye dhamana ya kusimamia na kuamua matumizi sahihi na kwa kuwa sisi sote kama Wabunge, ni Madiwani katika Halmashauri zetu, napenda kushauri kwamba kupitia vikao husika ni

vyema tukatoa mapendekezo yetu ili yaweze kufanyiwa kazi kwa ufanisi zaidi na kupata namna bora zaidi ya kutumia rasilimali na miundombinu husika kwa manufaa ya Taifa.

(b) Mheshimiwa Spika, mradi wa *Refugee Host Area Project,* ni mradi unaofadhiliwa na Serikali ya Denmark kupitia Shirika lake la Maendeleo *DANIDA.* Lengo kuu la mradi huu ni kusaidia maeneo yaliyo na wakimbizi katika miradi ya maendeleo hususani vyanzo vya maji, visima, huduma za afya, miradi midogomidogo ya kilimo na ufugaji, utunzaji wa mazingira, uanzishwaji wa Vyuo vya Ufundi, *VETA* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mradi huu wa sasa unamalizika mwaka 2009. Aidha Serikali ya Denmark haina nia ya kuendelea na mradi iwapo mpaka kufikia kipindi hicho wakimbizi watakuwa wameondoka. Mtazamo wa wafadhili ikiwemo Denmark ni kwamba mara baada ya wakimbizi hao kuondoka, Serikali kupitia bajeti yake ya maendeleo, itatenga fedha kwa ajili ya kuendeleza miradi iliyoanzishwa ili kuwa endelevu na kwa faida ya wananchi.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii.

Kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nisikitike kwamba swali bado halijajibiwa kwa sababu msingi wa swali sio makambi kurejeshwa, msingi wa swali ni namna gani ambavyo tumekaa na wakimbizi zaidi ya miaka 40 na namna gani sasa *UN* kupitia Serikali waweze kutoa *appreciation fund,* sio makambi yanayorudishwa. Kwa hiyo, naomba niseme swali hili halijajibiwa, kwa sababu nimepewa maelezo ya Halmashauri bila kujibu swali lenyewe. Sasa maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri, kupitia Wizara yake, yuko tayari sasa Wizara yake iandae kikao na sisi Wabunge wa Mikoa mitatu iliyoathiriwa na wakimbizi ili tueleze hasa tunachotaka? Hilo la kwanza na ni Mikoa ya Kagera, Kigoma na Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa jana Mheshimiwa...

**SPIKA:** Umesahau Tabora sasa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na Tabora, majirani zetu.

Pili, kwa kuwa jana Mheshimiwa Naibu Katibu Mkuu wa *UN,* ametusaidia, amelizungumzia jambo hili baada ya mimi kuwa nimeliuliza, je, Mheshimiwa Waziri, sasa yuko tayari kuandaa kikao kati ya Mwakilishi wa *UN* hapa nchini na sisi Wabunge wa Mikoa hii ili tujenge hoja wenyewe? Maana yake inaonekana Wizara hii haielewi tunachotaka, tunapozungumza juu ya *refugee affected areas,* naomba majibu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nadhani usahihi ni kwamba majibu hayakutosheleza, lakini si kwamba swali halijajibiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa hayo mawili ya nyongeza!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli, nasikitika na si sahihi kusema kwamba Wizara ama Serikali, haielewi ama haifahamu, ufahamu upo tena wa kutosha tu na ninadhani swali limejibiwa maana nilichoeleza katika jibu la msingi ni kwamba Serikali Kuu, haiwezi ikaingilia maamuzi ya nini Serikali za Mitaa wanataka kufanya na ndio maana Halmashauri zimekuwepo. Tunapozungumzia *devolution* ya madaraka, Serikali Kuu haiwezi ikaiamulia nini watu wa Serikali ya chini wafanye, *it is the other way round.* Ingekuwa Serikali ya chini, ya Halmashauri, wameomba na kusema kwamba hiki ndicho wanachokitaka, wakaleta ombi Serikali Kuu, Serikali Kuu ikawa haikuchukua hatua, hapo kungekuwa na maneno na ninadhani hapo kungekuwa na mazungumzo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninachotaka kumjibu Mheshimiwa Mbunge, na ninasisitiza kwamba swali lake limejibiwa, ningeomba sisi kama Wabunge, tunakaa katika Halmashauri, tukae tuamue ni nini tunachotaka katika maeneo yetu na likishaamuliwa kule, likaletwa katika Wizara yetu, sisi tutalifanyia kazi katika ngazi alizozisema Mheshimiwa Mbunge, kukutana na viongozi wa Umoja wa Mataifa, akiwemo *Representative* wa *UNHCR* pale Dar-es-Salaam na *Representative* wa Umoja wa Mataifa palepale Dar-es-Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, nadhani hilo halina mjadala. Mkutano tunaweza tukafanya lakini ni nini kinatakiwa, Serikali Kuu haiwezi ikabuni ni nini wanataka kule isipokuwa lile litoke kule chini lije kwetu, litafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa maana nyingine, nasikitika kwamba nachukua muda kidogo, kwa sababu katika makambi ambayo yamekwishaachwa kwa mfano kambi la Mkungwa Wilayani Kibondo ambayo imefungwa, tayari imeshaanzishwa sekondari ya wasichana na katika kambi ya Lungufu ambayo pia imefungwa tayari inaanzishwa shule ya sekondari, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Bado tuko na Waheshimiwa Wabunge wa Kigoma na Wizara hiyo hiyo. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini.

Na. 270

**Ulinzi wa Wavuvi wa Mkoa wa Kigoma**

**MHE. PETER J. SERUKAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, suala la usalama wa raia ni jambo la msingi katika nchi yoyote duniani:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalinda wavuvi wa Mkoa wa Kigoma kwenye maeneo ya Katonga, Kibilizi na Ujiji ambao wanavamiwa mara kwa mara na majambazi wanapokuwa kwenye maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola kama vile *TRA*, Uhamiaji, *JWTZ* na Idara ya Uvuvi, limekuwa linadhibiti vitendo vya uhalifu katika Ziwa Tanganyika kwa kufanya doria majini kwa kutumia boti walizonazo.

Aidha, misako na doria za magari na miguu, hufanyika katika maeneo ya mwambao wa ziwa kwa kushirikisha wananchi hasa wavuvi kwa kupata taarifa za uhalifu wa wahalifu.

Aidha, vyombo vya usalama katika nchi za Tanzania, Burundi na Kongo, vimekuwa vikishirikiana katika kubadilishana taarifa za uhalifu na kufanya vikao vya ujirani mwema kwa lengo la kuimarisha ushirikiano katika nyanja ya ulinzi katika eneo la Maziwa Makuu.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona.

Inavyofahamika na kama Serikali ilivyotuambia hapa wakati wa bajeti ya mwaka 2006/2007, kwamba ingepeleka mashua ya doria Kigoma ili iweze kufanya doria kati ya Mkoa wa Rukwa na Mkoa wa Kigoma na mashua iliyopelekwa ilifanya kazi kwa miezi miwili tu na mpaka sasa iko *grounded.* Mheshimiwa Naibu Waziri, ametuambia wanafanya doria kwa vyombo vyao, ni vyombo vyao vipi hivyo wanatumia kufanya doria ambayo haisaidii wavuvi katika ziwa Tanganyika? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, aah, Mheshimiwa Waziri, Magufuli, kwa majibu.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani, napenda kujibu swali zuri sana la Mheshimiwa Msambya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika majibu ya msingi yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, alisema kwamba Serikali kwa kushirikiana na nchi jirani, kwa mfano *DRC* Kongo, Tanzania na Burundi, lakini kwa kushirikiana vyema na Wizara ya Mambo ya Ndani na Idara ya Uvuvi, tumekuwa tukishirikiana kwa pamoja katika kuhakikisha kwamba doria zinafanyika katika ziwa Tanganyika. Lakini katika mipango hiyo hiyo,

katika bajeti ya mwaka huu, kuna fedha ambazo zimesainiwa ambapo zaidi ya bilioni 26 zitatumika kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, wito wangu ambao ninapenda kutoa kwa wananchi wa Kigoma, ni kwamba sasa watumie hiyo Sheria Namba 22 ya mwaka 2003 katika kuunda *Beach Management Units*, ambazo kwa uhakika zitaweza kusaidia ulinzi katika ziwa Tanganyika lakini pia kupitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, tuna mpango wa kupeleka boti ambapo moja itakaa Kigoma na nyingine itakaa Rukwa, ambazo zitasaidiana na Jeshi la Polisi katika kuendesha ulinzi wa pamoja katika ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa taarifa nzuri hiyo ambayo inahitimisha sasa maswali ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Tunahamia Wizara ya Maji na Umwagiliaji, swali linaulizwa na Mheshimiwa Hasnain G. Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini.

Na. 271

**Mradi wa Maji wa Makangaga**

**MHE. HASNAIN G. DEWJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, mradi wa Umwagiliaji wa Makangaga ulioko Wilayani Kilwa Kata ya Kiranjeranje unasuasua:-

(a) Je, ni lini mradi huo utakamilika?

(b) Je, mradi huo unanufaisha vijiji vingapi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hasnain Gulamabas Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mradi wa Umwagiliaji wa Makangaga ulio katika Kata ya Kiranjeranje huko Kilwa, unatekelezwa kwa gharama ya shilingi 212,058,550/=. Kati ya Fedha hizo Shilingi 149,308,550/= zinatoka *Tanzania Japan Food Aid Counterpart Fund,* shilingi 10,000,000/= ni mchango wa Serikali na shilingi 52,750,000/= nguvu kazi ya wananchi. Ujenzi wa banio umekamilika vizuri na kazi inayoendelea ni ujenzi wa mfereji wenye urefu wa km 1.8 na kazi hii inatarajiwa kukamilika mwisho wa mwezi Septemba, 2008.

Mheshimiwa Spika, bado kuna matatizo ya msingi yanayosababisha miradi mingi pamoja na mradi wa Makangaga kuchelewa. Tatizo moja ni ufunguzi wa akaunti ya

mradi ambao unachukua muda mrefu kufanyika. Kwa mfano, ilichukua zaidi ya miezi minne kufungua akaunti ya mradi wa umwagiliaji wa Makangaga.

Aidha, taratibu za Halmashauri ya Wilaya Kilwa kumpata Mkandarasi wa kujenga miundombinu, nazo zilichukua zaidi ya miezi minne. Matatizo haya yapo katika Halmashauri nyingi. Wizara yangu itawasiliana na Ofisi ya Waziri Mkuu, *TAMISEMI* kutafuta namna ya kuzisaidia Halmashauri ya Wilaya kuharakisha utekelezaji wa miradi ya maji na umwagiliaji kwa haraka zaidi.

(b) Mheshimiwa Spika, wakulima wenye mashamba katika mradi huo wanatoka katika vijiji jirani vitano vya Makangaga, Kiranjeranje, Mtandi, Mbwemkuru na Nakiu.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mimi nina swali moja dogo la kumuuliza Waziri. Kwanza ninampongeza kwa majibu yake mazuri na nisema kwamba kwa kuwa, mradi huu unaisha Septemba, je, Waziri anasemaje kutupatia wataalamu kwa ajili ya mafunzo ya umwagiliaji hapo Makangaga wakawafundishe wakulima wetu hicho kilimo cha umwagiliaji, ataweza kutupatia wataalamu hao?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumuahidi kabisa kwamba tuko tayari, tutapeleka wataalamu na hata katika utaratibu uliopangwa kwa mwaka wa fedha ujao ni kwamba suala la mafunzo kwa wakulima ni la muhimu, namshukuru kwa kuliona hilo.

**Na. 272**

**Uchimbaji wa Lambo katika Kijiji cha Seke – Ididi**

**MHE. FRED M. TUNGU** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali katika bajeti yake ya mwaka 2006/2007, ilipanga kuchimba lambo katika Kijiji cha Seke – Ididi na kwa kuwa lambo hilo halijachimbwa mpaka sasa, je, Serikali itawahakikishia wananchi wa Kijiji cha Seke – Ididi kwamba lambo hilo litachimbwa mwaka huu 2008 ili kuwaondolea kero ya ukosefu wa huduma ya maji wananchi hao?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fred Mpendazoe Tungu, Mbunge wa Kishapu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara ya Maji ilipanga kujenga na kukarabati jumla ya mabwawa 23 katika Wilaya mbalimbali. Miongoni mwa mabwawa hayo ni bwawa la Seke Ididi lililopo katika Wilaya ya Kishapu. Matangazo ya

kupata Wakandarasi wa kujenga mabwawa hayo, yalitolewa magazetini mwezi Aprili, 2007. Lengo lilikuwa kutumia shilingi 15.5 bilioni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa mabwawa hayo. Hata hivyo, kutokana na uhaba wa fedha kiasi cha shilingi 8.5 bilioni tu ndicho kilichotolewa kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa. Kutokana na hali hiyo, Wizara ililazimika kuondoa baadhi ya mabwawa na kubakiza mabwawa machache katika mpango wa mwaka 2007/2008, ambayo gharama zake za utekelezaji zinalingana na kiasi cha fedha kilichotengwa. Bwawa la Seke Ididi ni miongoni mwa mabwawa ambayo ujenzi wake uliahirishwa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 15 Mei, 2008, nilipokagua hali ya upatikanaji wa maji katika Shule ya Sekondari ya Shinyanga na Mgodi wa Dhahabu wa Mwadui, Mheshimiwa Mbunge, aliibua suala la ujenzi wa bwawa la Seke Ididi. Napenda kusisitiza majibu niliyompa kwamba kwa kuwa Serikali ilikwishaahidi kujenga bwawa la Seke Ididi katika mwaka 2007/2008 lakini ikashindikana kutokana na ufinyu wa bajeti, bwawa hilo sasa tumelichukua kama mradi – kiporo ambao tunatarajia kuutekeleza katika mwaka 2008/2009.

**MHE. FRED M. TUNGU:** Mheshimiwa Spika, kabla sijauliza swali la nyongeza kwa niaba ya wananchi wa Seke Ididi pamoja na wananchi wa Vijiji vya Mani pamoja na Chitereje na Sekebugoro, kwa namna ya kipekee kabisa na kwa dhati kabisa na kutoka kwenye sakafu ya moyo wangu, naomba niishukuru sana Wizara kwa uamuzi wake wa kuchimba bwawa la Seke Ididi mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa nilizopewa na Makamba wa Seke pamoja na rafiki yangu Mgalatia, Mkandarasi amefika katika eneo la ujenzi na anatarajia kuanza kazi hiyo.

Kwa kuwa, mradi wa kuchimba bwawa la Seke Ididi ulikuwa ni moja ya miradi mingine ya *Quick Wins* ambayo ilikuwa imepangwa kutekelezwa katika vijiji vya Iboja, kuchimba lambo la Iboja pamoja na lambo la Butuyu pamoja na ukarabati wa lambo la Lagana pamoja na Kiloleni, je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza pia miradi hiyo ya *Quick Wins* ambayo ilikuwa ni pamoja na mradi wa Seke Ididi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nipokee shukrani za Mheshimwa Fred Mpendazoe Tungu lakini pia ni wajibu wetu kufanya kazi hizo.

Sasa naomba nimjibu Mheshimiwa Mpendazoe, kuhusu *Quick Wins* kwamba Serikali au Wizara ilipoweka utaratibu huu wa *Quick Wins* tuliweka ili tuwe na miradi ambayo tunaweza tukaitekeleza haraka na kutoa majibu haraka yaani maji yaweze kupatikana kwa haraka wakati tunasubiri mchakato mkubwa sana huu wa miradi ya kutekelezwa kwa ufadhili wa *World Bank*.

Mheshimiwa Spika, lakini msingi wa *Quick Wins*, ni uleule kama alivyoeleza sasa hivi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, ni Halmashauri ya Wilaya ndiyo inayojua kwamba ni wapi tunatakiwa tufanye nini. Sasa mimi najua kabisa kwamba

katika mwaka 2006/2007, tulitenga milioni 271,381,000/= tukazipeleka Kishapu, mwaka 2007/2008 tumetenga shilingi milioni 111,229,000, mwezi Juni mwaka huu zimepelekwa Kishapu. Kwa hiyo, ni juu ya Halmashauri ya Kishapu kuangalia vipaumbele kama hayo malambo ndiyo kipaumbele basi yenyewe ndiyo itapanga.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninapenda nimuulize swali moja la nyongeza.

Tarehe 04/07, alinijibu kwamba kwenye tarehe 17, Wakandarasi wangekuwa wameshafika kwenye bwawa la Nyachitanda kitu ambacho mpaka juzi walikuwa hawajafika. Napenda Mheshimiwa Waziri anaieleze ni nini kimetokea mpaka sasa hivi hao wahusika hawajafika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shibiliti kwamba mimi mpaka sasa nilikuwa sina hakika kama hawajafika lakini katika utaratibu wa maandalizi ya ujenzi mambo mengi hutokea, inawezekana hiyo tarehe ikapitwa kidogo, hii ni taratibu za kawaida za maisha.

Mheshimiwa Spika, sasa nimuahidi tu kwamba nitafuatilia nijue ni kwa nini hawajafika pale halafu tutachukua hatua kuhakikisha kwamba wanafika.

Na. 273

**Ushuru wa VAT kwenye Nchi Wanachama wa Afrika Mashariki.**

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN** aliuliza:-

Kwa kuwa, Jumuiya ya Afrika Mashariki inao Umoja wa Ushuru wake ambazo hutoza ushuru unaolingana na nchi wanachama wa Umoja huo:-

Je, kwa nini ushuru wa VAT unatofautiana kati ya nchi wanachama wa Umoja huo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI** alijibu:-

Mheshimwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Jimbo la Kikwajuni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Afrika Mashariki inao Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki (*East African Customs Union*). Katika Umoja wa Forodha, nchi wanachama hukubaliana kuwa na utaratibu unaofanana wa kutoza Ushuru wa Forodha kwenye bidhaa zote zinazotoka nje ya eneo la Forodha (*Common External Tariff*) na kuondoa ushuru huo kwenye bidhaa zinazotoka au zinazozalishwa ndani ya eneo la

Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki. Uzoefu unaonyesha kuwa katika hatua ya Umoja wa Forodha, nchi wanachama hubakiwa na mamlaka kamili katika Sera za Kodi za Ndani, kama vile *VAT* na Kodi ya Mapato na Ushuru wa Bidhaa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mamlaka waliyonayo, ni kweli kuwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT),* inatofautiana kati ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kuwepo kwa tofauti za viwango vya Kodi ya *VAT* ni kutokana na ukweli kuwa kodi hii ni ya ndani na iko nje ya eneo la msingi la uoanishaji wa viwango vya kodi katika Umoja wa Forodha. Kwa maana hiyo, nchi wanachama wana mamlaka ya kuamua viwango wanavyotaka kutoza katika kodi za ndani.

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa, kiwango cha *VAT*, Tanzania ni kikubwa kuliko wenzetu wa Kenya na Uganda, je, Waziri yuko tayari kuangalia suala hili ili apunguze ili angalau na sisi tulingane na wenzetu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI**: Mheshimiwa Spika, kwanza nataka niseme kwamba ni kweli kodi ya *VAT* Tanzania ni kubwa ukilinganisha na Kenya, Uganda na Rwanda. Kenya wana 16%, Uganda 17%, Rwanda 18%, Burundi bado hawajaanzisha kodi hiyo wakati Tanzania tuna 20%

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niseme kwamba Serikali yetu ya Tanzania imejitoa katika suala zima la kuwa na biashara, kwa hiyo Serikali inaendeshwa na kodi. Suala la kupunguza hii kodi ili iweze kulingana na wenzetu, nataka niseme kwamba linakubalika na ninadhani tutaliangalia ili tuweze kufikia viwango walivyonavyo wenzetu.

**MHE HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, katika *East Africa* hii tumekubaliana kufanya biashara pamoja na kushindana kibiashara na kwa kuwa ushindani wa kibiashara ni pamoja na gharama hizi za *VAT*, kwa kuwa wenzetu *VAT* yao ni ndogo huoni kwamba unatupunguzia wafanyabishara wetu kuweza kuingia katika ushindani wa biashara kwa kuwa na kiwango kikubwa cha *VAT*?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwamba kodi ya *VAT* ni kodi ya ndani, kwa maana hiyo kodi hii anailipa zaidi mlaji na sioni kama wafanyabishara wa Kenya, Tanzania na Uganda watakuwa wanashindana kama kodi hii itakuwa na viwango sawa. Mimi nadhani kwamba kodi hii tutakapoiweka katika kiwango kimoja itamsaidia zaidi mlaji kuliko hata mfanyabiashara wa Kenya, Uganda na wa Tanzania.

Na. 274

**Kuboresha Mawasiliano Wilayani Mkinga**

**MHE. ERNEST G. MABINA (K.n.y. MHE. MBARUK K. MWANDORO)** aliuliza:-

Kwa kuwa, mawasiliano ni muhimu sana katika kuendesha na kusimamia shugjhuli za maendeleo na kwa kuwa, sehemu nyingi |Wlayani Mkinga kama vile Mwakijenge, Kasera, Gombero, Kwale, Manza, Boma, Tawalani, Jirihini na Nairobi mawasiliano hayapatikanai au hupatikana kwa shida:

(a) Je, Serikali itachukua hatua gani kuwaondolea wananchi kero hiyo?

(b) Je, Serikali inaweza kuzishawishi kampuni za simu kuboresha biashara yao Wilayani Mkinga?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kampuni ya *CELTEL* inafanya tafiti za masoko katika maeneo hayo ili kupeleka huduma za mawasiliano katika sehemu za Mwakijenge, Kasera, Gombero, Kwale, Manza, Boma, Tawalani, Jirihini na Nairobi na kuondoa matatizo ya mawasiliano katika Kata hizo ifikapo mwezi Juni, 2009. Aidha, *CELTEL*, imekusudia kupanua wigo wa mawasiliano Wilayani Mkinga kwa lengo la kuiongezea nguvu mitambo yake.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya *Vodacom*, imeshabaini maeneo husika ya Mwakijenge, Kasera, Bombero, Kwale, Manza, Boma, Tawalani na Nairobi pamoja na maeneo mengine yaliyo jirani hususani yale ya Mjasani, Mkinga na kadhalika. Tathmini ya kiufundi inatarajia kufanyika ifikapo Desemba, 2008 kwa ajili ya kuweka mtambo (mitambo) wa mawasiliano ili kukidhi mahitaji ya huduma hiyo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Wilaya ya Mkinga hususani eneo la Gombero limewekwa katika mkakati wa mipango endelevu ya kampuni ya *TIGO* ya mwaka 2009/2010. Aidha, kampuni ya *ZANTEL* inatarajia kufanya utafiti katika maeneo ya Horohoro ifikapo mwezi Julai, 2009 ili kuweza kuweka minara ya mawasiliano. Pia Kampuni ya *TTCL*, inao mpango wa kufikisha huduma ya mawasiliano katika maeneo tajwa ya Wilaya ya Mkinga, utekelezaji wake ni baada ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na juhudi zake za kuhimiza Makampuni ya Simu yaliyopo nchini kupeleka, kusambaza na kuboresha huduma za mawasiliano katika maeneo ya Wilaya ya Mkinga na maeneo mengine nchini ili kuwaondolea wananchi kero na kuharakisha maendeleo yao. Vilevile tunamwomba Mheshimiwa Mbunge wa Mkinga aendelee kushirikiana na Serikali katika kuwahamasisha wananchi kutumia fursa za mawasiliano katika kuibua na kutekeleza shughuli za kijamii na kiuchumi kwa maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ernest G. Mabina, swali la nyongeza, sasa sijui utauliza ya Mkinga au utauliza ya Geita!

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba sehemu za Mkinga kuna *Vodacom* ambayo ina minara kule na makampuni mengine yanafanya utafiti wa kuweka minara, kwa nini hayo makampuni yasishirikiane yakatumia minara ile ile ya *Vodacom* ili kuweza kurahisisha kuweka mawasiliano haraka zaidi katika Wilaya ya Mkinga?

La pili, kwa kuwa vijiji alivyovitaja vya Mkinga, ni sawasawa kabisa na vile vya katika Jimbo la Geita Kata ya Lubanga, Kijiji cha Isobutundwe, Lubanga, Kamhanga na maeneo mengine hayana mawasiliano mazuri kama anavyosema, je, Serikali inasemaje juu ya kupeleka mawasiliano katika maeneo yale?

**SPIKA:** Nilijua tu utafika huko. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Mheshimiwa Spika, kwa kweli ni wazo zuri sana kwa kampuni za simu kushirikiana minara kwa lengo la:-

(a) Kupunguza gharama; na

(b) Kufikisha mawasiliano kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, tayari Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, imeshawaweka kitako makampuni haya na kuwaomba kwamba pale inapowezekana waweze kushirikiana.

Mheshimiwa Spika, lakini hapa kinachogomba ni kwamba kila moja ya kampuni hizi, ina *business plan* yake, ukimwambia twende huku pamoja anakuambia mimi sasa hivi mpango wangu hauko Tanga, mpango wangu wa kibiashara sasa hivi unakwenda labda Mwanza, hilo ndilo jambo ambalo linagomba zaidi. Lakini tutaendelea kuwashauri ingawaje hatuwezi kuwalazimisha sana lakini tutaendelea kuwashauri kwamba kushirikiana katika minara ni kitu kizuri kwanza, mazingira unayaweka katika hali nzuri na pili unapunguza gharama.

Mheshimiwa Spika, napenda nimuhakikishie Mheshimiwa Ernest Mabina kwamba vijiji alivyovitaja basi tukitoka hapa anipe tu nione namna gani ninaweza kusukuma ili na yeye apate mawasilano katika vijiji vyake.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri anaonekana ni mtaalamu sana kwa mambo ya mawasiliano,

ninauliza swali moja la kule kwangu Kilwa Kaskazini kuhusu ufunguzi wa minara ya Kipatimu na Njinjo utafanyika lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Mheshimiwa Spika, fani yangu mimi ni Daktari wa Binadamu lakini ninajifunza tu haya mambo ya mawasiliano kutokana na majukumu ya kazi ambayo nimepewa.

Mheshimiwa Spika, napenda nimfahamishe Mheshimiwa Mpanda kwamba nitawasiliana na kampuni husika ambazo zimejenga minara ile ya Kipatimu na ule mwingine wa Kilwa Kaskazini, kuona je, minara ile ni kwa nini hadi leo haijafanya kazi, pengine kuna shughuli nyingine ambazo zilitakiwa zifanywe kabla ya minara hiyo kufanya kazi. Lakini ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, ninampa jibu muafaka kama nilivyompa jibu wakati akiwa na matatizo ya simu katika Wilaya yake.

**SPIKA:** Kabla sijaenda kwenye Wizara ya Katiba na Sheria ambayo ndiyo inafuata, nawakumbusha Waheshimiwa Wabunge kuhusu Kanuni ya 66. Wengine mnashindwa kabisa kunong'ona, mnaongea tu kama vile tuko nje. Sasa hii ni kinyume na sitasita kutumia mamlaka mliyonipa kuwashughulikia wale ambao badala ya kunong'ona, wanaongea tu kama vile tupo sokoni au mahali pa namna hiyo.

Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa anayeuliza sasa ni Mheshimiwa Kilontsi Mprogomyi, Mbunge wa Kasulu Magharibi. Aha! Leo hawa wa Kigoma, Mh!

Na. 275

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI** aliuliza:

Kwa kuwa, Serikali imekuwa iki–*initial* na kusaini mikataba mingi kabla ya kupitishwa Bunge na kwa kuwa, Bunge limekuwa likiletewa mikataba hiyo ili kui–*ratify* wakati mwingine kwa *Certificate of Urgency* jambo ambalo haliwapatii wabunge nafasi ya kupitia baadhi ya mikataba kwa ufanisi:-

(a) Je, kuna tofauti gani kati ya ku–*initial* na kusaini mikabata hasa kama *content* za mkataba husika haiwezi kubadilishwa na majadiliano Bungeni?

(b) Je, kwa nini Serikali haitambui umuhimu wa kutoa taarifa Bungeni kuhusu mwanzo na mwisho wa majadiliano ya mikataba hii?

(c) Kwa Serikali hu-*initial* na kusaini mikataba kabla ya kuileta Bungeni, je, Serikali haioni kuwa haiwatendi haki wananchi na Wabunge kwa kuzuia *oversight function* ya Bunge?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalila Mheshimiwa Kilontsi M. Mpogomyi, Mbunge wa Kasulu Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba unisamehe kama jibu langu litakuwa refu lakini swali lenyewe pia linahitaji maelezo marefu.

Mheshimiwa Spika, katika mgawanyo wa mamlaka ya nchi, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge limepewa madaraka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma. Mahakama imepewa mamkalaka ya kutafsiri Sheria na Serikali imepewa jukumu la kusimamia utendaji na utekelezaji wa Sheria. Kwa mgawanyo huo, Serikali ndiyo ina mamlaka ya kuingia mikataba na taasisi, kampuni au watu binafsi kwa maslahi ya nchi na Taifa.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Nchi, katika Ibara yake ya 63(3)(e), imeainisha kuhusu ushiriki wa Bunge katika suala la mikataba. Bunge linaweza kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa. Kwa kawaida aina ya mikataba katika kundi hili, ni ile inayohusu majukumu ya kila (*Soverignty Acts*). Hii inajumuisha mikataba baina ya Tanzania na nchi nyingine au Mashirika ya Kikanda au Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, aina nyingine ya mikataba ambayo Serikali inaweza kuingia, ni ile inayohusu mambo ya kibiashara (*Commercial Agreements*). Kwa kawaida mikataba ya aina hii inaendana na vipengele vya usiri (*Confidentialy Clause*). Hivyo, kwa kawaida, mikataba ya aina hii huwa haina sharti la kuridhiwa na hivyo huwa haifikishwi Bungeni.

Mheshimimiwa Spika, ku–*initial* mkataba, huwa ni hatua inayofanyika mwisho wa hatua ya majadiliano baina ya timu za majadiliano kubainisha kile kilichoafikiwa na kukubaliwa baina ya pande zinazohusika katika hatua husika ya majadiliano. *Initially* hufanyika pale ambapo ama mkataba husika haujafikia hatua ya kusainiwa kwa sababu ya kuwepo hatua nyingine zinazohitaji kukamilishwa kabla ya mkataba kusainiwa au pale majadiliano zaidi yanapokuwa bado yanahitajika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, kusainiwa kwa mkataba, huwa ni hatua inayowezesha wahusika kufungwa na mkataba husika kwa mujibu wa masharti yake. Kwa mikataba yenye sharti la kuridhiwa, mkataba hauibani nchi hadi pale unaporidhiwa. Katika hatua ya kuridhiwa, huwa haiwezekani kubadilishwa ila kinachowezekana hufanika ni ama Bunge kukataa ku-*ratify* mkataba husika au kuwa baadhi ya mikataba, ku-*ratify* lakini ikaitaka Serikali kuweka *reservations* katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyokwisha kueleza, kazi ya kujadili na kufungua mikataba ni ya utendaji na Serikali ndiyo inawajika kwa shughuli hizo za utendaji. Madaraka ya Bunge kama msimamizi mkuu wa shughuli za Serikali, ni kuweka masharti ya jumla kama itabidi, kwa kutunga sheria, kupitisha sera au kuidhinisha bajeti ya Serikali. Aidha, Bunge halipaswi kufanya kazi ya kupitisha mikataba kabla ya kusainiwa ili lenyewe libaki na uhalali wa kuiwajibisha Serikali kwa mujibu wa dhana ya mgawanyo wa mamlaka na kuchunguna, kukosoana na kuwajibishana (*Checks and Balances*). Bunge litashindwa kutekeleza jukumu lake kikamilifu iwapo litakuwa

limeshiriki katika kupitisha mkataba husika. Hivyo, utaratibu uliopo kwa sasa ni mzuri kwa kuwa unalenga kuimarisha dhana ya utawala bora kwa kuzingatia mgawanyo wa mamlaka ya uongozi wa nchi.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake.

Kwanza, kwa kuwa, wabunge wengi tumekuwa tukiomba kusiwepo na usiri kwenye mikataba mingi inayosainiwa na Serikali na kwa kuwa amezungumzia habari ya *confidentiality clause* ambayo kusema kweli haiwasaidiii Watanzania ambao mwisho wake, wao ndiyo wanaobeba mzigo mkubwa wa mikataba, je, Mheshimiwa Waziri anaweza kueleza hii *confidentiality clause* inawasaidiaje Watanzania?

Pili, kwa kuwa mikataba kama ile ya *Economic Partnership Agreements* ambayo ilikuwa *initialled* mwaka jana na kwa kuwa nchi zaidi ya 40 haziku– *initial* mikataba hiyo hasa kwa sababu walielewa uko utata na kwa kuwa, uko uwezekano mkubwa wa kujikuta mkataba huu unatuongezea umaskini mkubwa katika Taifa letu, ni nini Serikali itafanya ili kutuepusha na *negative effects* za mkataba huu?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kuwa na *confidentiality clause* katika *commercial agreements* unatokana na kwamba katika masuala haya ya kibiashara kuna ushindani, sasa katika ushindani tusingependa watu wengine wajue unafanya nini hasa washindani wako na ndiyo maana kunakuwa na hizi *confidentiality clauses*.

Mheshimiwa Spika, inaisaidiaje nchi yetu? Ni kwamba unapoingia katika mikataba hii, unabanwa tu na hizi, hawa wenzio wanafanya biashara, wanashindana na watu, wewe ni Serikali, huwezi kutoka wewe unatoa siri zao hadharani, unategemea utaendelea kufanya nao biashara? Watakataa kufanya biashara na wewe ndiyo maana kuna umuhimu wa kuwa na hizi *confidentiality clauses.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikataba ambayo tume-*initial* lakini bado hatujai-*ratify*, nasema utaratibu wetu wa kwanza kuingia mikataba mpaka tunaisaini ni mrefu, uko *very elaborate* na mpaka tufikie kusaini au kuja kuuleta hapa uwe *ratified* na Bunge hili, unakuwa umepitia hatua nyingi sana.

Kwanza, kuna timu ya wataalamu ambayo inapitia, kuna kitu kinaitwa *MTC* ambayo ni timu ya wataalamu Makatibu Wakuu, mwisho kabisa ukiwa ni mkataba mzito basi inabidi mpaka uende kwenye *Cabinet*. Sasa ukitoka pale unahitaji *ratification* ya Bunge, ndiyo unakuja hapa. Kwa hiyo, nasema *in future* wala hatutafanya makosa ambayo Mheshimiwa Kilontsi anatuonya tusiyafanye.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafsi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, utaratibu wa ku-*initial* kabla ya ku-*ratify,* ni utaratibu wetu wa ndani zaidi na si nchi zote zonafuata, nchi nyingi baada ya mkataba wowote kujadiliwa, wanaacha ku-*initial* mpaka kwanza wakubaliane ndani ya nchi yao. Je, Waziri au Serikali inasema nini kwamba sasa wakati umefika ili maslahi ya Watanzania yaweze kuzingatiwa na sisi twende na hawa wenzetu ambao kabla ya ku-*initial*, ni lazima maslahi ya nchi yatizamwe na ni Bunge tu ndilo linalojua maslahi ya nchi wakati wa kujadiliana hatuna tatizo kwamba lifanywe na Serikali?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ku-*initial* mkataba ni utaratibu wa Kimataifa na ndiyo maana tuna-*initial* mikataba siyo Tanzania tu hata tukiwa huko nje tuna-*initial* mikataba. Lakini ku-*initial* peke yake wala hakuku-*bind* sana, una-*initial* lakini ni kwamba bado tunaendelea kuzungumza lakini *page* mbili au tatu tumekubaliana, hizi tunazi-*initial* hizi nyingine ngoja tukashauriane na wenzetu tukirudi labda tutasaini. Kwa hiyo, ku-*initial* peke yake wala haina madhara lakini pia ni utaratibu wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, sasa kusema kwamba wakati umefika tuache ku-*initial* mpaka turudi kwenye Bunge kwa sababu Bunge peke yake ndiyo lenye maslahi ya nchi, napenda kusema kwamba sisi wote, Bunge pamoja na Serikali, tuna maslahi ya nchi pamoja na wananchi wote, kwa hiyo si sawa kusema ni Bunge peke yake lenye maslahi ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo tukisha-*initial* tuje Bungeni tuzungumze, turudi tukazungumze kule halafu tusaini, halafu turudi tena huku tu-*ratify,* nadhani tutakuwa tumeweka *procedure* ambayo kwa kweli haijawahi kuwekwa mahali popote na itategemea pia mkataba. *Commercial agreements* hatutaweza kuzileta Bungeni zipate kwanza kibali ndiyo zisainiwe, lakini kuna *Conventions* zile za Kimataifa ni lazima tuzilete hapa mzi-*ratify* ndiyo inakuwa sawa sasa nchi imeingia katika mkataba huo. *(Makofi)*

Na. 276

**Ukiukwaji wa Sheria ya Maadili**

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa, baadhi ya Viongozi wazito wa nchi wanakiuka Sheria ya Maadili:-

(a) Je, Serikali haioni haja ya kutoa mafunzo kwa Wabunge kuhusu Sheria hiyo?

(b) Kabla ya kutoa mafunzo, je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka sasa wa kumpatia kila kila Mbunge nakala ya Sheria ya Maadili?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mbunge wa Chakechake, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa, Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma iliyotungwa na Bunge hili Tukufu, inawalenga Viongozi wa Umma, wakiwemo Waheshimiwa Wabunge na kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wako makini katika kuzingatia masharti ya Sheria hiyo na kuwa kielelezo kikubwa cha uelewa wa Sheria yenyewe na kwa kuwa haupo ushahidi wa uhakika kwamba ukiukwaji unaofanywa na baadhi ya viongozi wazito wa nchi unatokana na kutoeleweka kwa Sheria hiyo, Serikali haioni sababu ya kutoa mafunzo kwa Waheshimiwa Wabunge kuhusu Sheria hii badala yake, Serikali inawashauri Waheshimiwa Wabunge kuisoma Sheria hiyo mara kwa mara kwa kuwa imetungwa na Bunge hili na ninaamini imeandikwa katika lugha ya kawaida.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubali pendekezo la Mheshimiwa Mbunge kuwa kila Mbunge apate nakala ya Sheria ya Maadili. Utaratibu unaotakiwa kufuatwa ni kwa Waheshimiwa Wabunge kupeleka ombi rasmi kwa Katibu wa Bunge ambaye awatasiliana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu utaratibu wa upatikanaji wa nakala za Sheria hiyo.

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa maadili ni kitu muhimu sana kwa kizazi chetu kijacho je, Mheshimiwa Waziri haoni haja sasa ya kuingiza somo la maadili katika mitaala ya shule zetu?

(b) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri katoa maelekezo namna ya kupata nakala ya sheria hiyo, sasa naomba rasmi kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, nimwombe Katibu wa Bunge tupatiwe nakala hizo.

**SPIKA:** La pili halimhusu Waziri, linamhusu Katibu na amesikia, Mheshimiwa Waziri, jibu swali la kwanza.

**WAZIRI WA KATIBA NA MAMBO YA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kweli nakubaliana naye kwamba maadili ni kitu muhimu sana na ingefaa basi kizazi chetu kijacho kifundishwe masuala ya maadili na nafikiri ni wazo zuri. Basi Serikali italizingatia na tutazungumza na Wizara husika ili tuone ni jinsi gani wanaweza kuweka hili somo la maadili kwenye mitaala yetu. Kama litakuwa somo au litakuwa vipi lakini waliweke katika mitaala ili vijana wetu waweze kujua maadili yetu ili nchi yetu hapo baadaye ipate viongozi ambao wana maadili na pengine hata hii sheria itabidi tuifute hapo mbele ya safari.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuna baadhi ya viongozi hawajazi fomu za maadili au wanajaza lakini hawarejeshi kwa wakati, je, Serikali inawapa adhabu gani hawa wanaochelewa kujaza fomu za maadili? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA MAMBO YA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, Sheria yenyewe ya Maadili imeweka adhabu kwa wale ambao hawatimizi masharti yake na mtekelezaji wa Sheria hii ni Kamishna wa Maadili. Kwa hiyo, nitamtaka Kamishna wa Maadili awe mkali, azingatie matakwa ya Sheria na awaadhibu wale wote kulingana na Sheria kwa wale ambao hawafuati masharti ya Sheria hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umekwisha.

Sasa ni muda wa matangazo na kama kawaida tunaanza na wageni. Nina furaha kuwatambulisha Wabunge wenzetu kutoka Uingereza ambao ni wanachama wa *CPA*, Tawi la Uingereza, kwa faida yao itabidi niseme kwa Kiingereza.

*It is a pleasure to welcome the MPs from the United Kingdom. As I mention your names, would you please stand up one after the other to be acknowledged. I will start with Honourable Eliot Molly, Honourable John Barrette, Lord Battier of Hamilton, Lord Johnnies of Tottenham, Lord Leah of Tonal and Miss Lucy Bowl, Secretary of the delegation. (Applause)*

*There should obviously be someone from the High Commission in Dar es Salaam, am I right? Nobody? Ohoo, okay.*

*Well, on behalf of the Parliament of Tanzania, it is a pleasure to welcome you Honourable Members from the UK, the Founder Member of the CPA. Is a special pleasure to welcome you here at Dodoma.*

*You do not know much Swahili, so I am not sure if you have benefited much from the question and answers period, ahaa, one does, okay thank you very much. It is a pleasure you must have been doing interpreting. We will help you to have a very useful stay and we will make sure that your visit is memorable in all respect. Thank you very much. (Applause)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni mwingine, Ndugu Prince Bagenda, Mwenyekiti Bodi ya Ushauri, Gazeti la Taifa Tanzania. Karibu sana. Tunafurahi Waandishi mahiri kama ninyi mnapokuja kushuhudia moja kwa moja matukio ya hapa Bungeni. *(Makofi)*

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Pindi Chana, anaitwa Ndewilwa Mbise. Yule pale, karibu sana. *(Makofi)*

Kuna mgeni pia wa Mheshimiwa Vitta Kawawa, anaitwa Ndugu Anelka, anatoka Namtumbo, ni kiongozi mhamasishaji wa kikundi cha Nyota ya Ruvuma, karibu sana. (*Makofi*)

Tunaye Bwana Theo Caspars, kutoka *European Commission* ambaye yuko Dodoma kwa ajili ya mazungumzo kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Nadhani mjadala huu umekwishaanza upo katika ukumbi fulani, tunawatakia mafanikio kwa sababu tunasubiri kwa hamu tuweze kupitisha Mfuko huu wa *CDF* mapema kadri inavyowezekana. *(Makofi)*

Nafurahi kuwakaribisha wanafunzi hamsini pamoja na Walimu wao kutoka shule ya Sekondari ya Kikuyu, naomba wasimame. Ahsanteni sana. Ninyi ndio Taifa letu la siku za karibuni, tunawatakia mafanikio katika masomo na Walimu tunawatakia mema kabisa katika kuwafundisha watoto wetu vizuri, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wanafunzi thelathini na tano wa shule ya Sekondari Chamwino Dodoma. Sijui wako upande gani, nadhani hawapo, aaa, wale pale, karibu sana pamoja na Walimu wenu. Tunawatakia mema katika masomo na Walimu tunawaomba muendelee kuwapa mafunzo kwa uhodari kadri mnavyoweza. *(Makofi)*

Wapo Maafisa kumi na moja wa Chama cha Walemavu Tanzania (SHIVIWATA). Wako upande wa kulia, karibuni sana na poleni na safari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Luhaga Mpina, anaye mgeni wake, Katibu wake wa Jimboni Kisesa, ndugu Mussa Msaji. Karibuni sana Dodoma na pole na safari. *(Makofi)*

Matangazo ya shughuli za kazi zetu, Mheshimiwa James Musalika, Mwenyekiti wa Amani *Forum Tanzania Chapter,* anaomba wajumbe wote wa Kamati ya Utendaji ya Amani *Forum,* mkutane leo saa tano asubuhi, Ukumbi Na. 231.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, anaomba wajumbe wote wa Kamati hiyo ya Maendeleo ya Jamii, mkutane mnamo saa nne na nusu yaani mara baada ya kipindi hiki katika Ukumbi Na. 231. Ukumbi huu unapendwa sana, natumaini watakuwa wamemaliza kabla wale wengine hawajaingia au Katibu atawapangia Ukumbi mwingine.

Mheshimiwa Zaynab Vulu, kwa niaba ya Mwenyekiti wa *CPA*, Tawi la Tanzania, anawataarifu wajumbe wote wa Kamati ya Utendaji ya *CPA*, Tawi la Tanzania, kuwa kutakuwa na kikao cha pamoja na wageni wetu waliopo *Speakers Gallery,* Wabunge wa *CPA*, Tawi la Uingereza, saa tano asubuhi chumba Na. 219.

Mheshimiwa Abdisalaam Khatib, Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara, anahitaji leo saa tano Ukumbi Na. 432, wajumbe wote wa Kamati hii wafanye mkutano.

Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mwenyekiti wa Wabunge au ni kwa niaba ya Mwenyekiti wa Maskauti hapa Bungeni, anaomba wajumbe wa kikundi cha Maskauti wakutane leo, saa nne na nusu asubuhi kwa kikao kifupi cha kundi hilo katika Ukumbi wa Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, kila Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, jana alipewa nakala za vyeti ambavyo vinaendeleza ile kampeni ya kupambana na ukatili dhidi ya wanawake. Nadhani mtakuwa mmegawiwa leo au kama bado basi mtagawiwa, tunaombwa kuweka saini kwenye vile vikonyo kwa sababu vinanyofolewa na kukusanywa kesho mchana. Kwa hiyo, tunaomba kati ya leo na kesho Waheshimiwa muweze kutia saini kudhihirisha kwamba sisi wote katika Bunge hili tunapiga vita ukatili dhidi ya wanawake.

Mengine nimeletewa sasa hivi, Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, anaomba leo saa nne na nusu, wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini, kwa kikao kifupi tu, Ukumbi Na. 227.

Mkurugenzi wetu Msaidizi wa Huduma kwa Wabunge, Mama Kippa, ameomba nitangaze kwamba Bendi za Muziki za hapa Dodoma, *Super Melody* na Saki *Stars*, zimeandaa burudani maalum ya dansi kwa heshima ya Wabunge na hafla hiyo itafanyika kesho katika ukumbi wa Kilimani *Club* kuanzia saa mbili na nusu usiku. Tiketi zinatolewa hapa Bungeni pale eneo la mapokezi katika jengo la Utawala. Kwa hiyo, wale wote hususan Wabunge vijana na wale wazee ambao rohoni wanajisikia ni vijana, basi tushirikiane kwenda kwenye hafla hii nzuri ya dansi ambayo utakuwa ni mchanganyiko wa miziki mbalimbali ya Tanzania. Tangazo hili hata mimi linanivutia, kwa hiyo, nina asilimia kubwa ya kuweza kushiriki.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwisho wa matangazo, sasa nitamwita Katibu kwa hatua inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 – Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, orodha yangu bado ni ndefu tu lakini tutaendelea kushauriana tuone tutahitimisha vipi. Tunao mchanganyiko ule ule, ambao hawajachangia, waliochangia mara moja, waliochangia mara mbili na kadhalika. Nitahadharishe tu kwamba silazimiki kuifuata orodha kama ilivyo kwa sababu Kanuni inanitaka nichanganye uchangiaji kwa kuzingatia jinsia, pande wa Muungano na Kambi za Vyama kwa sababu kuna Kambi ya Chama Tawala na Upinzani. Kwa hiyo, mkiona naruka, mjue ni busara za Spika zinafanya kazi.

Sasa nitaanza na Mheshimiwa William Shellukindo, nitamruka Mheshimiwa Rosemary Kirigini kwa sababu alikuwa safarini, ameniandikia yeye mwenyewe kwamba anaomba kidogo aangalie hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, ndiyo maana namruka hapa, atafuatiwa na Mheshimiwa Pindi Chana na baadaye Mheshimiwa Mgana Msindai, hawa watatu wajiandae.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nami nitoe mchango wangu kidogo kwenye hoja hii ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo moja nataka kulifafanua kidogo. Baadhi ya Wabunge walikuwa wanadhani nimeshachangia mara nyingi tu, mimi nimechangia kwenye Muswada wa *Controller and Auditor General* yaani *National Audit Bill*, katika hoja za Mawaziri, hii ndiyo mara yangu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Waziri, Mheshimiwa Wasira, kwa hotuba yake nzuri ambayo ina ufafanuzi wa kutosha na hasa ametukumbusha kwamba kuna maeneo mengi kwenye Majimbo yetu tungeyaangalia vizuri kwa mfano, miradi ya kilimo kama *PADEP* na kadhalika, namshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, hili suala la kilimo, naomba Wabunge wenzangu tusilichukue kama kitu cha kawaida tu, lazima tuwe makini katika suala hili kwa sababu kilimo kinahusu, kama Waziri alivyosema karibu asilimia sabini ya Watanzania kwa hiyo ndiyo uhai wa Taifa letu na kama hatutakipa kipaumbele basi kuna madhara tunayoweza kuyapata. Pia tuzingatie kwamba kilimo sasa hivi kinazungumzwa katika makongamano na mikutano mingi sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba viongozi wetu wa Afrika wapatao arobaini na naamini Rais wetu alikuwa mmojawapo, mwezi Juni, 2006, walikutana kule Abuja, Nigeria katika mkutano wao ambao waliuita napenda kunukuu: "*Comprehensive Africa Agricultural Development Programme*". Programu hiyo ilikuwa na shabaha zifuatazo nitapenda kuzinukuu, zinasema hivi:-

*(i) "Kuongeza pato la kilimo kwa asilimia sita ifikapo mwaka 2013;*

*(ii) Kutenga asilimia kumi ya Pato la Taifa kwa ajili ya kilimo; na*

*(iii) Kukubaliana kwamba kwa sababu ya hali isiyoridhisha ya ardhi katika Bara la Afrika, mbolea imekuwa ni kitu muhimu na ni suala la kisiasa. Kwa hiyo, walikubaliana kwamba kodi ya mbolea mipakani iondolewe na kuweka utaratibu wa kugharamia mbolea kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika pamoja na na Taasisi nyingine za fedha".*

Mheshimiwa Spika, sasa labda cha kujiuliza hapa, je, sisi Tanzania, azimio hili tumelitekeleza kwa kiasi gani? Ninapenda Waziri wakati anafunga hoja yake, atupe ufafanuzi kwa sababu kuna taarifa nyingi au makubaliano mengi ambayo yanatolewa. Sasa wakati mwingine unashindwa kuelewa, ni lipi kwa mfano, kuna makubaliano ya kutenga asilimia kumi ya Pato la Taifa kwa ajili ya kilimo, je, sisi tumefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, jana niliangalia Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Wizara hii, ametaja kutenga asilimia kumi ya bajeti ya Serikali kwa kilimo katika nchi za SADC.

Sasa, ni vizuri tukapata ufafanuzi ni asilimia kumi ya Pato la Taifa au ni asilimia kumi ya Bajeti ya Serikali?

Mheshimiwa Spika, katika kilimo, kuna suala la chakula. Sasa hivi kila ukisikiliza redio yoyote ile, inazungumzia uhaba wa chakula duniani. Ukisikiliza utasikia kila nchi inaweka mikakati yake ya kuhakikisha kwamba wana chakula, je, sisi tumeajiandaaje, chakula chetu tunakitunza?

Mheshimiwa Spika, nimeona katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, katika suala kwa mfano la kilimo cha chakula, linaingiliwa na kilimo cha mazao ya nishati ya mimea, *biogas* na nimeona pale amesema Wakuu wa Mikoa wameagizwa kudhibiti suala hilo. Lakini hivi karibuni nimesoma katika magazeti, sina hakika kwamba ndivyo ilivyo kwamba, katika Bonde la Usangu kule Mbarari, yule mwekezaji ambaye amepewa eneo hilo badala ya kupanda mpunga na mazao mengine ambayo ni muhimu kwetu, anapanda jatrofa. Naomba Serikali imnyang'anye hilo eneo kwa sababu analiharibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa za wataalam wa kilimo, ni kwamba, jatrofa inaweza kustawi katika maeneo ambayo ni kame au kwa Kiingereza "*marginal areas"*. Sasa kwa nini tuharibu maeneo yetu haya yenye rutuba kwa kuacha kupanda mazao ya chakula na kupanda mazao haya ambayo kwa kweli hayatatusaidia wakati wa njaa?

Mheshimiwa Spika, nimesoma makala moja katika gazeti la *African Business*, inayosema "*The Silent Tsunami"*. *Tsunami* ambayo inakwenda chinichini, haionekani na wamesema hii inahusu suala ya chakula.

Vilevile nimemsikia Mheshimiwa Raila Odinga, Waziri Mkuu wa Kenya wakati anatembelea maeneo yenye uhaba wa chakula kule Kenya, alitoa maneno ambayo aliyasema kwa Kiingereza kwamba "*A hungry man is an angry man"*. Kwa Kiswahili ni kwamba "mtu ambaye ana njaa ni mtu mwenye hasira". Sasa tusije kufika mahali kwa sababu ya kupanga mipango bila kuwa makini, tukashindwa kuzalisha chakula cha kutosha na kujitegemea kwa chakula, watu wakawa na hasira na itakuwa si vizuri.

Mheshimiwa Spika, nimesoma katika hii *"The Silent Tsunami"* kwamba kule katika visiwa vya Haiti, Wananchi walipata njaa, wakaingia barabarani na kupiga kelele kwamba wana njaa, ikamlazimu Waziri Mkuu ajiuzulu. Hatutaki sisi tufike hapo, tujiandae, tuhakikishe tuna akiba ya kutosha ya chakula.

Mheshimiwa Spika, halafu Maafisa wa Umoja wa Mataifa wanaohusika na kilimo, wametamka kabisa kwamba, wamejaribu kutafuta chakula katika maeneo mengi lakini wamekataliwa na napenda ninukuu hii kwa Kiingereza, wanasema hivi:-

"*Emerging market countries are now placing so many export controls on items such as wheat to conserve them for their own populations; they have refused to release supplies to the United violated Nations. We have never seen this before"*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *The Silent Tsunami* hiyo wanayoizungumzia. Sasa ni vizuri tujiandae isije kufika mahali tukasema tutaomba chakula, hakitapatikana kwa sababu kama Umoja wa Mataifa unanyimwa basi hata sisi hatutapata.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili suala la kilimo kwa kweli tulipe umuhimu wa kwanza na nakubaliana na Serikali kabisa kuipa ile Mikoa inayolima mahindi kwa wingi na nafaka nyingine, fedha za kutosha ili watusaidie kuweza kupata chakula cha kutosha. Wanapopewa nafasi au fursa hiyo wasiichezee, waitumie vizuri na sisi tunategemea kwamba wanaelewa kwamba wengine hatulimi hizo nafaka.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mimi natoka eneo linalolima chai, lakini napenda kumwomba Waziri wa Kilimo, hebu hili suala walifikirie vizuri, naona chai ni chakula. Sasa chai ingehesabika kwamba ni sawasawa na nafaka ya mahindi kwa sababu chai tunaitumia wakati wote na kama kuna upungufu wa chai basi hata hayo mahindi kama watatengeneza mikate au watachemsha, yatakosa kitu cha kuteremshia. Hebu tuiangalie hii chai, tunaiweka katika nafasi gani, naiona kama ni chakula.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri Wajapan miaka mitano iliyopita walikuwa na mpango wa msaada kwa chakula. Tulijenga hoja sisi watu wa Usambara Magharibi, kule kwenye chai, wakakubali kutusaidia kutengeneza barabara za chai ili tuzalishe chai ya kutosha na wale wakulima wa chai wanunue mahindi kwa watu wengine wa Rukwa, Mbeya, Iringa na kadhalika. Lakini inashangaza kwamba baada ya fedha zile kutolewa, awamu ya kwanza, zilikuwa na awamu kama tatu hivi, baadaye mradi huo ukazuiwa na taarifa tunazozipata ni kwamba wataalam wa kilimo walianza kubishana kwamba chai si zao la chakula lakini Wajapan wanakubali kwamba chai ni zao la chakula na wakakubali kutupa msaada wa kutengeneza barabara ili tusafirishe chai kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Mheshimiwa Waziri atupatie majibu kwa nini msaada huo ulifungwa? Ulikuwa na kiasi cha kama shilingi bilioni moja na milioni mia mbili lakini ulikuwa unakwenda kwa awamu. Kwa hiyo, tuliweza kufanikiwa tu kutumia kama shilingi milioni mia mbili, hizo nyingine hatuelewi ni nini na kila tukiuliza hatupati majibu ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru sana Serikali kwa hatua madhubuti inazozichukua. Mwezi Novemba katika Bunge la Mkutano wa Tisa, tarehe 12 Novemba, 2007, nilitoa hoja kwamba Bunge lijadili taarifa ya Benki ya Rasilimali ya Tanzania. Nakushukuru kwamba ulikubali kwamba hoja hiyo ikajadiliwa kwenye Bunge na tukafikia muafaka kwamba kuna haja ya kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameitaja kwamba watashirikiana na Wizara na Kilimo na Wizara ya Fedha kuanzisha Benki hiyo. Sasa hakuna muda, itaanzishwa lini, kwa sababu kuandika tu ni kitu kingine na utekelezaji ni kitu kingine. Napenda wakati wa kujibu, washirikiane na Waziri wa Fedha, tujue Muswada wa Kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo, utaletwa lini hapa Bungeni? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia nizungumzie suala la mbolea. Uzalishaji wa chai katika Jimbo la Bumbuli pamoja na maeneo mengine, umeshuka kama Waziri alivyoonyesha katika hotuba yake, umeshuka kwa asilimia mbili nukta tatu. Ni dhahiri kabisa kwa sababu kulikuwa na ukame, lakini nina wasiwasi kwamba uzalishaji utaendelea kushuka kwa sababu wakulima wa chai watashindwa kununua mbolea. Mbolea imepanda mno, mbolea ya *NPK* ambayo tulitumia katika msimu wa kilimo uliopita, ilikuwa inauzwa mpaka Sh.30,000/= kwa mfuko, leo hii mfuko huo unapatikana kati ya Sh.60,000/= mpaka Sh.70,000/=. Sasa katika hali hii wakulima watashindwa kununua mbolea hiyo na kuna uwezekano kuwa, uzalishaji wa zao la chai ukazidi kupungua. Kwa hiyo, naomba suala hili kwa kweli litazamwe kwa makini sana ni vipi tutaweza kuwasaidia wakulima wadogo wadogo wa zao la chai.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninapenda kulisisitiza hapa ni kwamba pamoja na mbolea inabidi kuimarisha ugani katika maeneo ya chai. Jana Mheshimiwa Mramba alizungumza kwenye kahawa, kwa kweli ugani uko nyuma sana. Kwa bahati nzuri, nasi tunanufaika na Taasisi ya Utafiti ya Chai (*Tanzania Tea Research Institute*) ambayo ipo Mufindi, imebidi tupatiwe Wataalam wa Ugani na tuwagharamie sisi kwa sababu hakuna njia nyingine ya kuwapata.

Mheshimiwa Spika, nadhani sasa umefika wakati Maafisa Kilimo wale wangepewa taaluma za mazao maalum ili katika maeneo ya kahawa, kwa kweli waende watu ambao wanajua kilimo cha kahawa, kumpeleka mtu wa pamba kwenda kusimamia zao la kahawa unampa tabu. Kuna uwezekano, wakulima wakawa wanajua zaidi zao la kahawa kuliko huyu mtu anayeletwa. Kwa hiyo, baada ya mafunzo ya jumla kuwe na *specialization*. Tunaomba, kwa niaba ya wakulima wadogo wa chai, kuwe na *specialization* katika chai ili tupate Mabwana Shamba ambao wamepewa taalama ya kina ya kushughulikia zao la chai.

Mheshimiwa Spika, sina zaidi isipokuwa napenda kusema kwamba naunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na napenda kusisitiza suala la Benki ya Wakulima kwani ni muhimu sana kwa sababu mtu anayelima chai kuanzia kupanda miche kwenye bustani inamchukua miaka minne ndipo aanze kuvuna.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika kwa muda wa mzungumzaji kumalizika)*

**SPIKA:** Tayari kengele ya pili.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii, kukushukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia Wizara hii ya Kilimo. Mimi ni Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Iringa na sisi Wabunge wa Viti Maalum hatuna Majimbo. Kwa hiyo, tunahudumia Wilaya zote zilizomo katika Mkoa na Mkoa wa Iringa ni miongoni

mwa Mikoa kadhaa iliyoko nchini Tanzania ambayo imejikita sana katika masuala ya kilimo. Kwa hiyo, nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kufanya kazi nyingi za maendeleo ya kilimo, wanajitahidi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile, nichukue nafasi hii, kuwapongeza sana wananchi wa Mkoa wa Iringa na Wilaya zake zote za Mufindi, Makete, Njombe, Kilolo, Iringa Mjini, kwa kazi kubwa ya maendeleo ya kilimo. Katika Mkoa ule wakati wa kilimo watu wanajitoa sana, saa 12.00 asubuhi tayari wako mashambani wanafanya kazi kwa bidii sana. Hata sisi wanasiasa ukisema uitishe mikutano kipindi hicho, kwa kweli humpati mtu kwa sababu wanajitoa sana. Pamoja na jitihada hizi nyingi ambazo wananchi wa Mkoa wa Iringa wamekuwa wakizifanya katika kujiendeleza na hususan kuendeleza masuala yote ya kilimo, bado zipo changamoto kadhaa ambazo kwa pamoja wananchi na Serikali lazima tushirikiane kuzitafakari na kutatua changamoto hizi.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa ambayo inawa-*face* wananchi wa Mkoa wa Iringa, ni suala zima la mbolea. Mbolea imekuwa ni kikwazo, mbolea imekuwa ni changamoto, kwanza, haipatikani na haikidhi yale mahitaji yanayohitajika. Wilaya peke yake kwa mfano Wilaya ya Njombe wanahitaji tani zaidi hata ya 200,000 kwa sababu hizi ni Wilaya ambazo zinalima mazao ya mahindi, lakini pia viazi na si mara moja tu. Ndani ya mwaka mmoja, Mkoa wa Iringa unapolima viazi wanaweza wakaweka na kuvuna vipindi vitatu na vipindi hivyo vyote vitatu, vinahitaji mbolea. Yako mazao kama ya chai, mahindi, yote haya yanahitaji mbolea. Lakini pia mbolea hii ikipatikana bei yake huwa ni ya juu sana ukilinganisha na kipato cha wananchi na wakati mwingine inapatikana kwa msimu.

Mheshimiwa Spika, suala la ruzuku limesaidia kwa kiasi fulani, lakini mbolea hii ya ruzuku, ule utaratibu wa ruzuku ni muhimu sana tukautafakari, tunaweza tukafanya nini. Wizara lazima iweke mpango wa kuagiza mbolea vipindi vyote ndani ya mwaka, isiwe tu wakati wa kilimo ndipo mbolea inaingia nchini na ile nayo kuwa *produced* hapa nchini iwe *produced* mwaka mzima. Itasaidia uwepo wa mbolea nyingi na hivyo bei inaweza ikapungua. Lakini pia wawekezaji, hebu Wizara iangalie wawekezaji wengi katika sekta hii ya mbolea na tunapokuwa na wawekezaji wengi upande wa mbolea maana yake kunakuwa na mashindano ya biashara, kwanza *quality* itaongezeka, mashindano na hatimaye bei itapungua. Kwa hiyo, hili jambo limekuwa ni changamoto kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hili, baadhi ya maeneo Serikali imejitahidi sana kwa kuweka ule mfumo wa stakabadhi, kwa mfano maeneo ya korosho, kuna mfumo wa stakabadhi, kwa Mkoa wa Iringa, tutashukuru sana kama Serikali itatafakari utaratibu huu wa stakabadhi hasa Wilaya zile za pembezoni ukatumika hata katika mazao ya mahindi. Baadhi ya Wilaya kutokana na miundombinu yake, wafanyabiashara wanaokwenda kununua mahindi katika maeneo hayo huwa ni wachache sana, wengi wanaishi maeneo ya Makambako au Njombe ambako kuna barabara ya lami. Lakini wafanyabiashara wengi hawafiki maeneo ya pembezoni kwa mfano Wilaya ya Ludewa, Makete, Kilolo kutokana na barabara. Hivyo, mkombozi mkubwa wa wakulima katika maeneo hayo, huwa ni Serikali ambayo inanunua mahindi kupitia *SGR* wakati mwingine Serikali huwa

inasema labda mafungu hayajafika katika Mkoa husika. Kwa hiyo, tunaishauri Serikali kwamba wakati mafungu yanakuwa hayajafika basi wakiyapeleka mahindi yao kwenye maghala ya *SGR* wapewe stakabadhi zile za mazao. Kwa sababu maeneo mengine ime-*prove* kwamba utaratibu wa stakabadhi unafaa sana hivyo tungeomba sana sana ufikiriwe katika mazao haya ya mahindi nako watumie stakabadhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati umefika sasa wa kufanya mapinduzi ya kilimo *(green revolution),* nchi nyingine hata wakiwa hawana mvua za kutosha kwa mfano nchi za Mashariki ya Kati, *(Middle East)* kule maeneo mengi ya nchi huwa ni jangwa, pamoja na jangwa hilo, wamejitahidi sana ku-*produce* mazao kama matunda na inafika wakati mpaka wana *export*. Kwa hiyo, wakati umefika wa kilimo cha nchi yetu ya Tanzania kutotegemea mvua. Tunapotegemea mvua wakati wa kilimo, tunaposahau kilimo cha umwagiliaji, hii mara nyingi huwa ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, aidha, kuna mwaka tunakuwa na upungufu wa chakula, kuna mwaka chakula kinakuwa kimezidi, kwa hiyo, wakati umefika wa kuibua miradi ya umwagiliaji mingi iwezekanavyo maeneo ya kule kwetu kutokana na tatizo hilo utakuta watu wanalima kando kando ya vyanzo vya maji, wanaita vinyungu kutokana na uhitaji wa maji. Lakini tukishabuni utaratibu mzuri wa kilimo cha umwagiliaji katika kila Wilaya, kila eneo kupitia miradi yetu ya *DADPs*, *PADEP* na *ASPD* itatusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kuiomba Wizara, hebu itafakari pale Mkoa wa Iringa, kule mto wa Ruaha, Ruaha ni mto mrefu sana umeanza Iringa Manispaa unakwenda mpaka Mtera, je, isingekuwa bora tukaweka bwawa pale Ruaha ambalo miaka ya nyuma tulikuwa tunaweka kwa mfano bwawa la Mindu, bwawa la Mtera tutafakari basi ile Ruaha pale Mkoa wa Iringa tukaweka bwawa ambalo litatosheleza shughuli za kilimo cha umwagiliaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Iringa, nizungumzie pia Shirika la *National Milling Corporation*. Pale Iringa kuna shirika linaitwa *NMC* muda mrefu sana lilikuwa lina-*operate* shughuli za kilimo, lakini baadaye Serikali tukaweka utaratibu wa kubinafsisha lakini Shirika bado halijabinafsishwa liko bado mikononi mwa Serikali. Tungeomba sana shirika hili na tuliomba libinafsishwe kwa wananchi wa Iringa na hata sisi Wabunge wa Mkoa wa Iringa, tulikuwa tayari kabisa kutengeneza bodi yetu ili tupewe lile shirika tuliendeshe wenyewe kwa manufaa ya wananchi wa Iringa. Kwa hiyo, ushauri ninaoutoa *NMC*, anaweza akapewa mtu binafsi lakini lifanye zile shughuli ambazo ilikuwa inafanya kabla. Maana yake lishirikishwe lile shirika kununua mazao, kuhifadhi mazao, kusaga wakati ule lilikuwa linasaga na baadaye kuuza kutafuta masoko. Kama litaweza kuhifadhi, ikitokea sehemu moja au sehemu nyingine ya nchi kuna upungufu wa chakula, inakuwa ni rahisi sana yale mazao yaliyokuwa yametunzwa yaweze kuuzwa maeneo mengine ya nchi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, tumesema kwamba mwaka huu tutawasaidia majirani zetu wa Kenya waje wanunue chakula nchini yaani mahindi. Utaratibu huu ni mzuri kwanza utatupatia masoko lakini inahitaji *coordination* ya Wizara kwa jirani sana. Wanapokuja kununua, ni vema sana wakanunua kwa utaratibu wa kupitia

*SGR* Serikalini, kwa maana wanapokuwa wanakwenda moja kwa moja vijijini, ni rahisi sana kumlalia mkulima kwa sababu maeneo yetu mengi bado hayana vipimo. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali ijitahidi sana ku-*coordinate* suala hili kwa sababu ni kweli tunahitaji masoko lakini tuangalie na takwimu zetu ili na sisi tubakie na chakula cha kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaposema kilimo ni muhimu, tukatafakari pia suala la viwanda vya usindikaji. Mazao mengi sana ya kilimo yanaharibika haraka yaani yako *perishable*. Kwa hiyo, viwanda vya usindikaji, kwa mfano viwanda vya kusindika vitu kama viazi, matunda, vitasaidia sana. Ni jukumu la Serikali kutafakari, viwanda hivi na shughuli kama za *packing material* pamoja na kutangaza mazao yetu ambayo tunayo nchini. Utakuta matunda aina ya *Apple* yanayotoka Afrika Kusini kutokana na *packing* yake, kutokana na kutangazwa kwake kwa ile biashara tunda moja aina ya *Apple* linauzwa Sh.600 wakati *Apples* za Tanzania fungu moja yaani yanakuwa kadhaa siyo moja, linauzwa Sh.300. Mambo kama haya ni muhimu tukayatafakari, tuwasaidie sana wakulima wetu masuala ya *packing material*, *advertising* na hata wakati mwingine elimu. Tukishawaanda na tunapoita/tunapoalika soko huria linakuwa linafanyakazi vizuri. Lakini tunapoalika soko huria wakati viwango vya mazao yetu bado ni vya chini, soko huria linakwenda kumgandamiza sana mkulima. Tunajitahidi sana kuzalisha maeneo mfano ya Ilula, Ruaha Mbuyuni, vitunguu, matunda, lakini tunahitaji Serikali isaidie ku-*coordinate quality* ya bidhaa tunazozalisha. Hii iwe sambamba na mbegu bora ambazo zinazokomaa kwa muda mfupi, zitasaidia sana kuboresha suala zima la kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipongeze sana Serikali kwa jitihada zake za kutengeneza masoko, ujenzi wa masoko maeneo ya Wilaya na katika Tarafa na Kata mbalimbali, hili ni jambo la msingi sana. Ushauri wangu ni kwamba masoko tunayoyajenga yawe ni masoko ya kuuza bidhaa kwa wingi *(wholesale)* maana yake yale masoko ambayo tunayajenga ni muhimu yakawa na maghala jirani yasiwe ni masoko ambayo yanafanana na maeneo ya Makao Makuu ya Mikoa, yawe ni masoko ambayo yanalenga kuongeza kipato cha mkulima maana yake kuwe na maghala jirani. Unapoweka soko zuri bila kuweka ghala maana yake mwananchi atauza kwa kiwango kidogo kidogo, hivyo pato lake litaendelea kuwa dogo. Lakini ukishajenga soko kwa mfano soko la Mlangali pale Ludewa ukaweka ghala kubwa, vitu kama mahindi yakawa yanahifadhiwa, soko kama la Kibaigwa na maeneo mengine yakawa na maghala ya kutosha ya kuhifadhi vyakula vingi, itasaidia sana kuongeza kipato.

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo suala la Benki ya Wakulima. Benki ya Wakulima itasaidia sana. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika kwa muda wa mzungumzaji kumalizika)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, kengele ya pili hiyo**.**

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Pindi Chana ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Mgana Msindai, atafuatiwa na Mheshimiwa Rosemary Kirigini wakati huo huo ajiandae Mheshimiwa Luhaga Mpina.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Nampongeza sana Mheshimiwa Stephen Wasira, namfahamu siku nyingi na tumefanya naye kazi zaidi ya miaka 10. Naibu Waziri wake ninamfahamu na wasaidizi wake, nimefanya nao kazi kwa muda mrefu sana. Ninawashukuru wametuletea bajeti, maneno ni mazuri, lakini sijui kama utekelezaji utakwenda na yale maneno waliyoyaandika.

Mheshimiwa Spika, hapa kwetu Tanzania bado tunacheza na kilimo, hatujaamua kufanya kilimo cha tija, kilimo cha kuwasaidia wananchi wetu, kilimo cha kuongeza pato la Taifa. Sasa hivi wananchi wetu bado wana shida kubwa sana. Katika nchi yetu mvua hazitoshi, tuna Mikoa zaidi ya nusu haipati mvua inayotakiwa, lakini makorongo yapo, kila wakati mvua ikinyesha yanajaa maji na kila mwaka Serikali inasema itatengeneza tuanzishe kilimo cha umwagiliaji, sijui tutakuja kufanikisha lini?

Mheshimiwa Spika, hebu tuanze sasa na hiki kilimo tulichonacho, huko Wizarani wanapanga mipango, wanapeleka fedha lakini hawafuatilii zinafanya kazi gani? Mimi nitoe mifano miwili, mitatu ya Jimboni kwangu. Walitoa fedha juu ya kujenga *scheme* ya umwagiliaji Mwangeza na Msingi na upande wa Iramba Magharibi walitoa fedha Masagi, hizo *scheme* zimejengwa hata hazijakamilika zikabomolewa na mafuriko. Ni *scheme* ambazo zimechukua fedha nyingi sana za Serikali, lakini kwa sababu ya uzembe na kwa sababu ya kutokuwa na watu makini hazijafanya kazi mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, kama miezi mitatu, minne iliyopita, niliuliza swali hapa Bungeni, wakasema watapeleka fedha kwa ajili ya kutengeneza hizo *scheme*, lakini mpaka leo hizo fedha hazijapelekwa. Mimi ninaomba Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika atakapohitimisha hoja yake, aniambie ni lini *scheme* ya Msingi, Mwangeza na Masagi zitatengenezwa. Sisi tunahitaji hizo *scheme* kwa faida ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kutegemea mvua, ni lazima turudi kwenye kilimo cha umwagiliaji kama wenzetu wanavyofanya. Mimi ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri asisahau kunijulisha juu ya hilo. Mkoa wa Dodoma, Mkoa wa Singida, Tabora, Shinyanga, sehemu ya Mara anapotoka Mheshimiwa Waziri na Mkoa wa Manyara, ni Mikoa kame.

Mheshimiwa Spika, huu ni mwaka wa tano, tunaambiwa kwamba unakuja mradi maalum wa kuendeleza hicho kilimo. Sisi wenzenu tunalima mtama, tunalima uwele na maeneo machache yanalima mahindi. Lakini ni lini watatusaidia na sisi tujikomboe? Waliwahi kutwambia hapa hapa Bungeni kwamba mtama una soko kubwa sana Italy, tukalima, watu wakavuna sana, lakini hakuna mtama ulionunuliwa. Kwa hiyo, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha hoja yake aniambie.

Mheshimiwa Spika, kwa Mkoa wa Singida kwa kweli mimi ninaupongeza sana Uongozi wa Mkoa, Mheshimiwa Parseko Kone, *RAS* wake, Ma-*DC* wote, Wakurugenzi na Madiwani. Sisi tumekwishafanya *zones* na kujua maeneo yapi kinaota nini? Kwa mfano, tumesema kabisa mazao yetu makuu kwa Mkoa wa Singida ni mtama, uwele, mhogo, viazi na aina za kunde, mahindi katika maeneo mengi ya Mkoa wetu hayastawi vizuri. Kwa hiyo, wanaolima mahindi, wanalima kwa ubavu wao. Lakini hayo mazao niliyoyataja ndiyo mazao ambayo yapo kwenye *zones* zetu na mazao ya biashara ni alizeti, pamba, vitunguu, ufuta, dengu na asali.

Mheshimiwa Spika, lakini utaona mpaka sasa, Serikali haitilii maanani kabisa. Ukienda Bonde la Lyelembo, zamani walikuwa wanalima pamba na ilikuwa na nyuzi ndefu wakaacha kwa sababu ya kukosa wanunuzi. Juzi juzi hapa wamekuja wakatushawishi wananchi wakaanza kulima pamba, wananunua kwa kilo kwa shilingi 400 ambayo ni hasara kweli kweli. Kwa hiyo, mimi ninaiomba Serikali iangalie suala hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inahimiza wananchi wetu walime alizeti ya kutosha. Alizeti mwaka huu imelimwa sana na Jimbo ninalotoka mimi ndiyo wanaolima zaidi, lakini wanunuzi hakuna na bado wananchi wanalanguliwa. Sisi wananchi wa Mkoa wa Singida, tunaomba watuletee Stakabidhi ya Mazao Ghalani. Sisi Iramba tulijipanga, Madiwani wote na Watendaji wetu tulikwenda kujifunza kwa wenzetu wa Wilaya ya Babati wanafanya namna gani?

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ninampongeza sana Mheshimiwa Omar Kwaangw' na ndiye aliyenieleza juu ya suala hilo. Huo mtindo unakwenda vizuri sana. Kwa nini wasitusaidie na sisi wa Mkoa Singida mpango wa mazao ghalani, uje kwetu na ni lini utakuja? Kwingine wakisikia mazao yanakwama wanakimbia haraka haraka na kusema kwamba mtahakikisha mazao hayo yananunuliwa na yasiponunuliwa mnaachia ngazi, kwa Mkoa wa Singida kwa nini isiwe hivyo?

Mheshimiwa Spika, ninawaomba sana Mheshimiwa Stephen Wasira na Naibu Waziri wake, waje Singida wakaone na wawasaidie wananchi wetu. Sisi tumejipanga Mkoa mzima na tunafanya kazi kweli kweli na tunalima, lakini mazao yanaishia kwa walanguzi. Baada ya Serikali kusema kwa kipindi kilichopita kwamba inaleta kodi ya mafuta kutoka nje ya asilimia 10, sasa unashangaa wanataka kuondoa hiyo kodi, hebu hiyo kodi irudi haraka sana. Ni lazima tuwasaidie wananchi wetu, hiyo kodi ikiondolewa mafuta yatajaa kila mahali hapa, hata hicho kiasi kidogo tunacholanguliwa hatutapata. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali, hiyo kodi ya asilimia 10, irudi ili kuwalinda walaji wetu.

Mheshimiwa Spika, juzi Mheshimiwa Rais amesema ni lazima tukazanie kilimo na ufugaji. Mheshimiwa Rais ametamka, lakini ukiangalia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika bado haijafika kwenye *grass roots*, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ipo Wizarani, huko kwenye Halmashauri wana msimamizi mwingine ambaye ni TAMISEMI. Kwa hiyo, kunakuwa hakuna mtiririko wa maagizo na utendaji kazi kutoka Wizarani kwenda mpaka kwa mkulima kule chini. Maagizo yao ni lazima yapite kwenye Wizara nyingine nayo ndiyo itekeleze. Kwa kweli kwa upande wa kilimo hili halitakiwi

kabisa. Tunataka kilimo kitoke juu, sauti ikitamkwa kule na Mheshimiwa Waziri inashuka mpaka huko chini kwa mkulima.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi wafanyakazi wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, wapo wachache sana. Mkoa wa Singida mpaka tumeamua Watendaji wetu wote wamefundishwa jinsi ya kusimamia kilimo na ndiyo wamekuwa watu wa Ugani na tumetengeneza vitabu zaidi ya 1,000 na kuvigawa kote kwa ajili ya kusaidia. Sasa hata tukiimba hapa tufanye nini, tutakuwa tunacheza bila kuwa na tamko moja. Wizara ikitamka na iweke wasimamizi wengi waende mpaka vijijini.

Mheshimiwa Spika, tulipokwenda Babati, tulikuta maghala ya kuhifadhia mazao yanajengwa na *Agricultural Marketing System Development Programme.* Jana nilimuuliza Mheshimiwa Waziri, hivi hiki Kitengo kipo kwake? Akasema kipo Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa kweli niwapongeze sana, maghala waliojenga Manyara ni mazuri sana. Tunaomba hicho kitengo chake Mheshimiwa Waziri kije na Singida kitusaidie. Sasa hivi tunajitahidi kukarabati maghala yetu ya zamani na tumekwishajenga maghala mapya saba kwa ajili ya pamba na tumekarabati maghala zaidi ya 10. Lakini tunahitaji msukumo zaidi wanakuja Singida wanasema Singida ni Mkoa wa mwisho na utakuwa wa mwisho kama hamtusaidii, ndiyo, ongezeni nguvu ili na sisi tutoke hapo tulipo.

Mheshimiwa Spika, kilimo hata tufanye namna gani bila Serikali kusaidia, sisi hatulilii mbolea, kwetu tunalima kwa kutumia mbolea ya samadi ndiyo maana hatuna ugomvi na wenzetu. Wakisema mbolea hapa sisi tunanyamaza, lakini sasa tusaidieni na sisi tufike mahali pazuri. Sisi ni wakulima wazuri wa mtama, wakulima wazuri wa uwele na sisi watusifie kwa lile, siyo sifa zote zinakwenda kwa wakulima wa mahindi tu ni lazima mtukumbuke na sisi.

Mheshimiwa Spika, hili nilitoe hapa hapa, uongozi wa Wilaya ya Iramba tuliamua kwenda kujifunza Manyara, Karatu na Arumeru. Meru tulikwenda kwa ajili ya uzalishaji wa kutumia njia ya chupa kwa sababu Wizara zetu zimechanganyika, afadhali nilizungumzie hapa hapa. Madiwani wetu na Watendaji wetu, walivutiwa sana na Kituo cha Uzalishaji kwa kutumia njia ya chupa na wale walitwambia wana mbegu nyingi hazina wanunuzi. Sasa tunaomba Halmashauri zetu zote zihamasishwe tubadilishe aina ya ufugaji waende wakaone, kwa kweli hiyo itatusaidia sana kupata ng'ombe bora wa maziwa na wa nyama.

Mheshimiwa Spika, lingine tulipokwenda Karatu, wenzetu wa Karatu, umwagiliaji wao ni wa kisasa kweli kweli na wao wamesaidiwa na Serikali hii hii. Kwa nini huo utaalamu na hao wataalam wanatofautiana kwa nini wasipelekwa na Singida? Kwa nini wasipelekwe katika Wilaya nyingine wakafanya kazi nzuri, huko kwingine wanarashiarashia, kwingine wanafanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, lingine nizungumzie juu ya masoko yetu. Huu ni mwaka wa nne, Serikali imeahidi kujenga soko la Kimataifa pale Igunguno mpaka leo bado. Sasa nalo naomba Mheshimiwa Waziri atwambie nini kinakwamisha?

(*Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika*

*kwa muda wa mzungumzaji*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mgana Msindai kengele ya pili hiyo.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Rosemary Kirigini atafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Mpina na baada yake atachangia Mheshimiwa Said Amour Arfi.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipata nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika Wizara hii ya Kilimo.

Kwanza kabisa, kwa sababu sikuwepo, ninaomba nitoe pole kwa Mheshimiwa Naibu Spika kwa kufiwa na mtoto wa dada yake na vile vile Mheshimiwa Savelina Mwijage, kwa kufiwa na mtoto wake. Namwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, amin.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Stephen Wasira. Nimepitia hotuba yake ni nzuri sana na kwa kweli unapokuwa unasoma hotuba hii, unaona kweli sasa tunakwenda kwenye *green revolution*. Sina hakika sana na *implementation*, lakini nina uhakika kwa namna Mheshimiwa Waziri alivyo makini na alivyo mahiri na mchapakazi, na utekelezaji wa mambo haya yote aliyoweka kwenye hotuba ambayo ni mazuri sana ambayo yanatia moyo, utakuwa wa kina. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, naomba tu niipongeze Wizara kwa uamuzi wake wa kuanzisha mikakati ambayo ni mizuri sana mikakati ya *ASDP* na huu wa *CRMP* ambayo tumeona imekuwa ni mikakati ambayo imeleta maendeleo makubwa sana katika sekta hii ya kilimo.

Vile vile naomba niipongeze Wizara kwa kuchukua uamuzi wa kufikiria ni namna gani wanaweza kuongeza hawa *Extension Officers* kwani tunajua watu hawa ni muhimu sana na kilimo hakiwezi kuendelea bila ya kuwa na hawa *Extension Officers* wa kutosha. Jambo ambalo ningependa tu kusaidia hapa ni kwamba sote tunaona kwamba *intake* zilizopo kwenye Vyuo vya Kilimo kwa ajili ya kuwapata hawa *Extension Officers* zimekuwa ni chache sana. Sasa ningependa tu Waziri labda atufafanulie ni mikakati gani muhimu na kabambe kabisa na madhubuti ambayo Wizara inaichukua kuhakikisha kwamba vyuo hivi vinapata wanafunzi wa kutosha ili kuweza kutoa hawa *Extension Officers* kama walivyojipangia Wizara 11,000 kufikia mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho ninapenda kuongelea ni suala zima la kutilia mkazo kilimo cha umwagiliaji. Katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa nane, amesema kwamba, nitanukuu:-

*"Kuna upungufu wa vyakula vya nafaka kwa kiasi kikubwa uliochangiwa na upungufu wa mavuno ya vuli uliosababishwa na mvua za vuli kunyesha chini ya kiwango cha kawaida".*

Mheshimiwa Spika, ili tuondokane na tatizo hili, ni lazima tutilie mkazo kilimo cha umwagiliaji. Iwapo nchi yetu imejaliwa kuwa na mabonde mazuri sana, imejaliwa kuwa mito mingi sana kwa mfano kule Mkoani kwangu Mara liko bonde la Mto Mara na Mikoa mingine yapo mabonde mazuri ambayo yanaweza kutumika kwa shughuli nzima za kilimo. Lakini cha kusikitisha kwa mfano kule Mkoani kwangu kule Mara, bonde hili halijaendelezwa kabisa katika shughuli za kilimo. Vile vile ninapenda kumwomba Waziri aniambie tu ni mikakati gani ambayo ameipanga kwa mwaka huu katika kuendeleza bonde lile la Mto Mara hasa ukizingatia yeye pia anatoka katika Mkoa huo.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika suala hili la kuzingatia hali ya hewa, napenda pia niipongeze Serikali na Wizara kwa ujumla kwa kuelekeza nguvu za kilimo kwenye ile Mikoa ambayo ina mvua za kutosha, Mkoa kama wa Ruvuma, Iringa, Mbeya na kadhalika. Kweli ni jambo la maana sana Serikali imefanya katika kuelekeza nguvu za kilimo kwani nina imani kwamba Mikoa hii ikitiliwa maanani, inaweza kulisha Mikoa mingi sana ya Tanzania. Haina maana kwa Mikoa ambayo ni ya wafugaji kuelekeza nguvu nyingi sana za kilimo. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kuzingatia jambo hili.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya kilimo yatawezekana tu kama kutakuwa na mwendelezo wa mambo mawili ambayo nitayaongelea. Kwa mfano, jambo la kwanza ni utafiti wa kilimo. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kilimo chetu kimekuwa ni cha kushuka na kupanda. Kwa hiyo, ili kuondokana na tatizo hili, ni lazima kabisa Serikali ikajielekeza katika tafiti za kilimo. Kwa hivi sasa, tunaona tafiti nyingi za kilimo zinategemea fedha kutoka kwa wahisani. Hivyo si jambo baya sana lakini fedha hizi zinakuwa zinatubana baada ya kufanya tafiti zile ambazo tunazitaka sisi kama nchi, tunakuwa tunaegemea sana matakwa ya wahisani. Kwa mfano, nikichukulia Chuo cha Kilimo cha SUA kuna tafiti ambazo zinaendelea nyingi sana zikifadhiliwa na Serikali ya Norway. Kwa mfano, tafiti za *TARIP II, NAFOCO, PANTIL* zote hizo ni tafiti zinazoendelea katika chuo kile cha Kilimo. Lakini kitu cha kushangaza ni kwamba tafiti hizi zimebakia tu kuishia kwenye ripoti za Chuo kile lakini hatuelewi au wakulima hawaelezwi ni kitu gani wanatakiwa kufanya na kitu gani wanatakiwa kupanda kutokana na tafiti zile zinazofanyika kwenye Chuo kile cha Kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika chuo hicho hicho, katika tafiti hizo wanazofanya, wamegundua mbegu za maharage, mbegu hizo ni mbegu ambazo zinaoteshwa kwa muda mfupi na hazihitaji mvua nyingi. Lakini sasa tafiti hii haijawa *transmitted* kutoka kwenye chuo kile kwenda kwa wakulima wakaelewa ni maharage gani na aina gani ya mbegu wanatakiwa kupanda.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni tafiti ya zao la jatrofa. Sote tunaelewa kwamba kuna tafiti hii ambayo inaendelea na kuna Mikoa ambayo tayari wameshaanza kupanda zao hili la jatrofa. Lakini ukiangalia kwenye *internet* kule India wamegundua kwamba kuna mbegu ya zao la jatrofa au *species* ya jatrofa ambayo ina uwezo wa kukua

kwa miezi nane. Sasa nilikuwa nataka kuiuliza Wizara, je, wao wanafahamu kwamba kuna mbegu hii ya jatrofa ambayo inakuwa kwa miezi nane baada ya kuwaachia wakulima ambao sasa wameanza kujipandia jatrofa ambazo zinachukua muda mrefu miaka miwili au mitatu kwa ajili ya kuweza ku-*yield*.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninapenda tu kumwuliza Waziri katika mkakati mzima wa kuendeleza zao hili la jatrofa, ni mikakati gani wameiweka na ni fedha kiasi gani zimewekwa na ni tafiti za muda gani na zinatakiwa kufanyika katika muda gani kuhusiana na suala zima la zao hili la jatrofa?

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuongelea suala zima la *agriculture financing*. Tunaelewa kwamba wakulima wamekuwa hawapati mikopo. Benki zetu zimekuwa zikitoa mikopo lakini wakulima wamekuwa hawawezi kupata mikopo ile kutokana na riba ambayo imeonekana ni kubwa sana riba ya asilimia 15 mpaka 20 wakulima wamekuwa hawawezi ku-*afford*. Kwa hiyo, suala zima hapa tulikuwa tunamwomba Waziri na Serikali kwa jumla kuweza kuanzisha Benki ya Wakulima ambao itaweza kuwasaidia wakulima waweze kupata mikopo kwa kupitia Benki hiyo na kuweza kuendeleza kilimo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu wanafunzi wote wanaomaliza kwenye Vyuo vya Kilimo kwa mfano pale *SUA*, nikichukulia wenzetu Misri wana mkakati ambao ni mzuri kwa wanafunzi ambao wanasoma kilimo unapomaliza Digrii yako, unakuwa na Shahada yako ambayo unaipeleka kwenye Benki, *ofcourse* pamoja na mchanganuo wako mzuri wa aina ya kilimo unayotaka kufanya lakini ile Shahada yako ndiyo inaweza kukupelekea wewe mwanafunzi uliotoka kusoma kuweza kukopesheka. Kwa hiyo, naiomba pia Serikali iweze kuwaangalia hawa wanafunzi wanaomaliza pale *SUA* kwa sababu sasa hivi imekuwa wanafunzi wanakuwa hawataki kwenda kusoma haya masomo ya kilimo kutokana na kwamba hawaoni faida, wanapomaliza pale hawajui wapi pa kwenda na namna ya kupata mikopo vilevile inakuwa ni ngumu. Kwa hiyo, tuwaige wenzetu Misri kwa ajili ya kuweka zile Shahada zetu ili tuweze kukopesheka.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, ninapenda kuongelea kilimo cha *horticulture.* Mwaka jana pia niliongelea kilimo hiki. Kwa mtazamo wangu, naona tunafikiria mambo makubwa sana lakini kilimo hiki cha *horticulture* sioni kama kinapewa umuhimu unaotakiwa. Kilimo cha matunda sasa hivi kama tunavyoona matunda yanatakiwa sana nje ya nchi tunaweza tukalima matunda tukaweza kuyasafirisha nje ya nchi. Vile vile maua ni zao ambalo ukiuza unapata fedha nzuri sana. Kwa hiyo tungeweza kuwahimiza wakulima wetu pia baada ya kufikiria kuanza kulima kilimo kingine wajihusishe pia na hiki kilimo cha *horticulture* wakaweza pia kujipatia fedha kwa sababu kilimo hiki cha *horticulture* sio lazima ukachukue eneo kubwa sana unaweza ukalima tu eneo dogo lakini ukapata fedha.

Mheshimiwa Spika, suala lingine la kuzungumzia kwenye hotuba hii ni zana za kilimo. Katika Chuo cha Kilimo cha *SUA*, wamegundua aina ya trekta ambayo wanaita *Graduate Tractor*, ninapenda kuishauri Serikali waweze kufanya *coordination* na wale

watu wa *SUA*. Baada ya kufikiria kuleta matrekta nchini ambayo yatakuwa ni ghali sana kwa wakulima wanaweza wakawapatia fedha Chuo kile cha *SUA* wakaweza kutengeneza matrekta mengi sana haya ya *Graduate Tractors* ambayo wanaweza wakayasambaza kwa urahisi kwa wakulima wetu na wakulima wetu wakaweza kuyanunua kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, mwisho sitakuwa nimewatendea haki wananchi wa Mara kama sijaongelea Mara *Cooperation*. Tunalo tatizo la muda mrefu na Mheshimiwa Wasira analifahamu, ninamwomba wakati anahitimisha hoja yake aweze kunipa tu maelezo mafupi kuhusiana na suala zima la Mara *Cooperation*, watu wako pale hawajalipwa fedha zao mpaka leo. Nimekuwa nikiomba muda mrefu na ninaomba tena leo kwa kupitia hotuba yake kwa kupitia nafasi hii aweze kunifafanulia na kuniambia ni lini wananchi hawa waliokuwa katika hiki chama cha Mara *Cooperation* wataweza kulipwa fedha zao.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru Mheshimiwa Kirigini na sasa namwita Mheshimiwa Luaga Mpina, ajiandae Mheshimiwa Arfi na atakayefuatia baada ya hapo Mheshimiwa Anthony Diallo.

**MHE. LUHAGA J. MPINA**: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza napenda kutoa kwanza taarifa kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Kisesa kwamba ujenzi wa daraja la Mto Simiyu unaendelea vizuri na kufikia mwezi Oktoba 2008, ujenzi huu utakuwa umekamilika na kwa kuwa Mheshimiwa Rais alishakubali kwenda kuufungua mradi huo mkubwa kabisa ambao unategemewa na wananchi wa Jimbo la Kisesa pamoja na wale wa Bariadi na wengine basi wapiga kura wangu mkae mkao wa kula.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri haijatoa ufumbuzi wa matatizo ya wakulima waliyonayo Watanzania. Kwa maana hiyo, naweza kusema hotuba hii ni sawa sawa na kitabu cha historia. Kwa maana hiyo sitaiunga mkono mpaka nipate ufafanuzi wa mambo mbalimbali makubwa ambayo yanawakabili wananchi wetu, wakulima wetu wa Tanzania. Wananchi wetu wamekuwa na matatizo makubwa sana ambayo yamechukua muda mrefu sana kupata ufumbuzi, hasa kwa kilimo cha pamba Shinyanga, Kanda ya Ziwa. Tumekuwa na mfumo wa *passbook* kwa zaidi ya miaka mitatu sasa wananchi wetu wamelalamika na sisi wenyewe Wabunge tumelalamika kwenye mamlaka zinazoshughulikia matatizo haya lakini ufumbuzi haukuweza kupatikana.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sana, wananchi wetu wamekuwa wakicheleweshewa pembejeo, wananchi wetu wamekuwa wakifikishiwa pembejeo zisizolingana na thamani ya fedha walizochangia. Wengine wamekuwa hawafikishiwi kabisa na kuwafanya waitafute hiyo pembejeo kwa fedha nyingine wakati tayari wameshakatwa kwenye vitabu vya *passbook*. Malalamiko haya tumeshayafikisha Serikalini, malalamiko haya tumeyafikisha kwenye Bodi ya Pamba na wakati mwingine hata Mheshimiwa Waziri alipokuwa hajawa Waziri wa Kilimo, tulishiriki naye kwenye

vikao vya Bodi kukemea sana habari hizi za *passbook* na kutaka mabadiliko ya haraka. Lakini sasa ninavyozungumza ni miaka mitatu hakuna mabadiliko yoyote katika *passbook* wananchi wananyanyaswa, wananchi wanakatwa fedha zao bila ya kupewa pembejeo. Juzi hapa Mfuko wa Pembejeo umekuja kufutwa tu *as a ceremonial event*. Lakini inafutwa wakati huo huo Serikali yenyewe ina-*declare* kwamba wananchi wamepunjwa pembejeo, wananchi wamekatwa fedha zao bila ya kuletewa pembejeo lakini hakuna tamko lolote la tathmini gani zinafanywa ili kuweza kuwalipa wananchi hao ambao wameshapunjwa fedha zao katika *passbook*.

Mheshimiwa Spika, nauliza kama pamba inaiva mwezi wa Aprili na inakuwa tayari kuvunwa na kuuzwa, hizi sheria za mpaka msimu uwe Juni zinatoka wapi? Wananchi wana matatizo makubwa, wao ndiyo hiyo kazi pekee ambayo wanaitegemea katika uchumi wao, ameivisha pamba anakaa nayo ndani anaambiwa kwamba msimu ni mpaka mwezi Juni. Lakini kwa *experience*, katika soko la dunia, katika muda ule pamba bei yake huwa iko juu sana. Sasa Waziri anipe ufafanuzi kama hii sheria ilikuwa inakubalika kipindi kile, labda pamba ilikuwa inaiva mwezi Juni na je, sasa hivi katika mabadiliko ya hali ya hewa anasema nini? (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wetu wamepiga kelele sana juu ya suala la bei ya pamba. Bei ya pamba shilingi 400/= na sasa 450/=. Wananchi wetu wamekuwa wakielezwa na Serikali yao na kwa kupitia tamko la Mheshimiwa Waziri Wasira la juzi, tamko la Serikali ambalo alitamka hapa Bungeni katika kikao hicho, kuna kikao cha tarehe 7 Juni, 2008 na kikao kingine cha tarehe 7 Julai, 2008 ambacho wadau wa pamba walikutana kujadiliana makubaliano juu ya bei ya dira mwaka huu. Katika vikao hivyo, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ilikuwepo. Iliwakilishwa lakini wote kwa pamoja walikubaliana kwamba bei ya kuanzia ni shilingi 400/=, lakini wakati huo Wizara inafahamu fika soko la pamba la Kimataifa likoje lakini pia Wizara inafahamu fika vigezo vinavyowakwaza wanunuzi wa pamba wasitoe bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, vikwazo ambavyo alivitaja Mheshimiwa Waziri siku hiyo ya tamko viko kwenye uwezo wa Serikali na Serikali ina uwezo wa kuvishughulikia siku moja tu vikaondoka na wakulima wakapata bei nzuri. Ushahidi upo, kuna malalamiko hapa ya wanunuzi kule Mkoani Shinyanga anakwenda kwenye Wilaya anasema mimi nakuja kununua pamba anaambiwa kwamba wewe hukuwepo kwenye kikao cha kwanza ambacho tulikaa kuwapitisha wanunuzi, kwa hiyo huwezi kupata nafasi, ukiritimba tu. Serikali inakula hasara gani kwa yeye kuchelewa, ina *risk* nini na ana kila kitu ana kiwanda ananunua pamba miaka yote kisa tu amechelewa kile kikao chako kwa nini usim-*task* hata kwa ajili ya gharama za kuendesha kikao, lakini ukamruhusu akanunua pamba. Serikali ilikuwa ikisingizia Halmashauri lakini kuna barua hizi zimesainiwa na Wakuu wa Wilaya Mkoani Shinyanga wanakatazwa wanunuzi wa pamba *monopoly*, Serikali inashirikiana na wafanyabiashara kwa namna nyingine kuwagandamiza wakulima.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana, lakini suala linakuja hii bei ya pamba, Waziri Mheshimiwa Wasira amekuwa ni mkereketwa mkubwa sana wa kilimo hata kabla hajaingia kwenye Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Nakumbuka kwenye kikao cha Bodi japo hatukuambizana lakini tuliudhiwa na wajumbe wa Kamati ya Bodi, mimi na yeye tuliondoka kwenye kikao kile cha Bodi kwa sababu tunakaa kikao ambacho hakitoi ufumbuzi wa matatizo ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ametoa ufafanuzi wa mustakabali wa mkulima wa pamba kwamba ni kujiunga tu na ni pale ambapo Vyama vya Ushirika vitakuwa vimejiunga na utaratibu wa stakabadhi ya mazao. Kama alivyosema yeye mwenyewe kwenye taarifa, stakabadhi ya mazao anayoizungumzia Mheshimiwa Waziri katika Mkoa wa Shinyanga kuna Vyama vya Ushirika vya Msingi 16. Kwa hiyo, ni suala ambalo sio ufumbuzi wa tatizo la wakulima ni tatizo ambalo litachukua muda mrefu sana. Sasa Waziri atamke anachukua hatua gani ya kuondosha vikwazo vinavyowakwaza wafanyabiashara wa zao la pamba, wanunuzi wa pamba katika mkoa wa Shinyanga au Kanda ya Ziwa kwa ujumla na sehemu zingine zinazonunua pamba ili waweze kutoa bei nzuri ya mkulima walau sasa kutoka hapa kwenye 450/= ifike kwenye 550/= walau mkulima ataweza kumudu gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, utajiuliza, ukiangalia kwenye takwimu, hotuba hii imesema hivyo. Ukiisoma hii hotuba nzuri, nimei-*terms* kama historia, hotuba za kilimo ukizisoma miaka yote, ni nzuri kweli kweli. Ukisoma hotuba, utasema kweli sasa tunaingia kwenye mapinduzi ya kilimo, lakini hakuna kitu, miaka 20 kilimo kinakuwa kwa asilimia nne. Ukiangalia uzalishaji wa pamba wa mwaka 1977/1978 ni tani 174,000, ukija uzalishaji wa pamba wa mwaka 2006/2007, ni tani 130,000 pamoja na ongezeko la watu na sababu zingine zote, haiwezekani! Tunahitaji mabadiliko makubwa, Mheshimiwa Waziri atangaze sasa, aondoe vikwazo ili bei ya pamba ya wakulima wetu iweze kuongezwa.

Mheshimiwa Spika, sasa ninakimbizana na suala muda, suala lingine ambalo linakwaza sana ni pamoja na wakulima wa mazao ya chakula kukatazwa kusafirisha mazao yao nje. Hawa wakulima wanalima *for their own risks, for risking their assests,* lakini *from no where,* Serikali inasimama inasema kwamba inazuia usafirishaji wa chakula nje ya nchi. Suala la upungufu wa nchi ni la mtu binafsi, kwa sababu huyu mtu kazi yake ya kulima ndiyo anajipatia kipato halali na yeye. Je, wale wasiolima wanachangia nini katika upungufu wa chakula wa Taifa?

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ninavyozungumza, Kigali bei ya mchele ni Sh.1,400/=, Dar es Salaam bei ya mchele ni Sh.800/=, tofauti ya mkulima pale ni shilingi 600/=, mkulima wetu anachangia wale wasiolima shilingi 600/= kwa kila kilo anayouza, *why*? Taifa kama lingekuwa na mkakati thabiti wa kufanya *compesation* au mkakati wa chakula nchini basi yenyewe ingemfidia mkulima ili sasa yeye aweze kuwauzia wakulima wengine wasiolima kwa bei hiyo halafu yenyewe ika-*compesate* upungufu huo.

Mheshimiwa Spika, tunawahujumu wakulima wetu, Serikali inashiriki kuwahujumu wakulima wake. Ninaomba basi Mheshimiwa Waziri alitangazie Taifa kwanza kwa kuwaomba samahani wakulima kwa mapunjo ambayo yamefanywa, lakini

pia kwa kuwaruhusu wauze mazao yao ya chakula popote vinginevyo basi Serikali yenyewe inunue ziada ya chakula cha wakulima kwa bei ya soko la Kimataifa. Wakati huo tukiwasisitiza wakulima wetu waendelee na kilimo tunasisitiza wazalishe, lakini wakati huo huo tunawawekea sheria ambazo zinakinzana na uendelezaji wa kilimo hicho. Ninaomba sana Serikali ipitie kwa makini sheria pamoja na matamko yake ya kila siku kuunga mkono jitihada za hawa wakulima.
Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii, shida kubwa ni pembejeo. Mikopo ya matrekta, Jimboni kwangu mkulima aliyepata sifa ya kupata mkopo wa trekta, ni mmoja tu Jimbo zima lenye wananchi zaidi ya 200,000. Sasa ukiangalia mgao wa trekta wenyewe haufanani na kasi yenyewe ya wananchi wetu wanavyohitaji matrekta. Sheria zenyewe za kupata hizo pembejeo ni ngumu mno wananchi wetu hawaziwezi. Ninaomba Serikali iruhusu wananchi wakaungana katika vikundi kwa mfano kule kwangu ukiwaambia wananchi 20 waungane ili wanunue matrekta na ukiwaambia watoe shilingi milioni moja ya kuanzia, milioni 20 zinapatikana mara moja unaweza ukaunda hata vikundi 20. Unawapelekea trekta wakadhaminiwa na Halmashauri zao, tukaondokana na hizi habari, matokeo yake wanawakopesha watu wanaodai kwamba wana zile sifa kwa maana wana hatimiliki ambao hata hawalimi sasa. Matokeo yake sasa hivi kuna migogoro ya watu wengi kutokulipa fedha katika mfuko huu kwa sababu wao sio wakulima, wakulima wetu wenye sifa za kukopa wengi hawana sifa hizi zilizotajwa humu. Ninaomba sana tufanye Mapinduzi ya kilimo, tuwape fursa wananchi wetu waweze kuzalisha, tuwaondolee vikwazo. Serikali yetu kuwa bingwa wa kutatua vikwazo vya wakulima badala ya kuwa bingwa wa kuwawekea vikwazo wakulima.

Mheshimiwa Spika, najua muda wangu sasa unaelekea mwisho lakini niseme kwamba ninaomba sasa ufafanuzi wa hayo mambo niliyokwisha kuyataja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli niungane na Waziri kwamba ipo haja ya makusudi ya kuleta mapinduzi katika kilimo. Lakini pia nikubaliane sana na Mheshimiwa Yusufu Makamba katika mchango wake wa jana umejibu maswali mengi ambayo tumekuwa tukijiuliza kwa kipindi kirefu na hasa pale aliponukuu vitabu vitakatifu Injili na Quran kwamba ilikuwa imejibu maswali ambayo yanaendelea kututatiza mpaka sasa hivi kwamba tumekuwa tukisema lakini hatutekelezi, sisi ni watu wa ajabu sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nizungumzie takwimu. Takwimu zinapokuwa sio sahihi hazileti majibu sahihi na nina vitabu hapa ambavyo ni vya Serikali, nina hotuba ya Waziri na nina kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa Toleo la Juni, 2008. Hivi vitabu vyote vimetolewa na Serikali, Serikali moja inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi, lakini takwimu zinapishana. Wizara inasema kwamba tunajitosheleza kwa chakula kwa asilimia 104. Taarifa nyingine inasema tunajitosheleza kwa asilimia 106. Lakini bado suala la kujitosheleza kwa asilimia 104 yameainishwa maeneo kadhaa katika nchi yetu ambayo yatakuwa na upungufu wa chakula. Najiuliza kama tumejitosheleza inakuwaje maeneo mengine yawe na upungufu, usahihi wa takwimu hizi ukoje? Lakini ukija

ukiangalia tatizo kubwa katika kilimo ni Maafisa Kilimo na Maafisa Ugani hasa katika ngazi za kata na vijiji ambako ndipo wapo wakulima.

Mheshimiwa Spika, lengo la Wizara lilikuwa ni kuajiri watumishi 2,500 lakini wameajiri watumishi 309 kwa mujibu wa hotuba ya Waziri. Lakini ukija katika kitabu hiki unakuta ni tofauti kwamba watumishi walioajiriwa ni chini ya 150. Ukija kwenye mbolea, hali kadhalika takwimu zinapishana, tena hapa ndio zinapishana mno. Wakati Wizara inaonesha kwamba mbolea zilizofika ni tani 211,013 kitabu kingine kinaonesha ni tani 44,412. Hata katika usambazaji wa mbolea wenyewe unapishana. Huku Wizara inaonesha imesambaza mbolea tani 81,000 huku taarifa inaonesha mbolea iliyosambazwa ni tani 23,000. Ukija ukiangalia *power tillers* Wizara inasema wametoa *power tillers* 16 huku zinaoneshwa tisa.

Mheshimiwa Spika, sasa kama takwimu zenyewe hazina usahihi ama hawa wanaweza kuwa sahihi ama Wizara wakawa sahihi, lakini, ni vema basi taarifa zikawa zenye uwiano hata kama zitakuwa na upungufu, usiwepo upungufu wa kutia mashaka. Tujisahihishe sana katika suala la kutoa takwimu.

Mheshimiwa Spika, nalisema hili, nakumbuka katika kikao kimoja cha *briefing* mwaka 2006, tulipewa taarifa kuhusu hali ya chakula nchini lakini katika kikao hicho mimi nilihoji kwamba mna uhakika na taarifa hizi mnazotupa kwa sababu nimetoka Jimboni kwangu, najua kuna upungufu wa chakula. Wakasema tunacho chakula cha kutosha. Baada ya miezi minne baada ya kutolewa taarifa hiyo ya hali ya chakula kwamba hali ya chakula ni nzuri, Watanzania wasihangaike, wasibabaike, Serikali hiyo hiyo ikarudi kuagiza chakula kutoka nje, tatizo ni takwimu.

Mheshimiwa Spika, takwimu zote inawezakana ni mtu anakaa juu ya meza anafikiria tu kwamba ongezeko linaweza kuwa la kiasi fulani, akajaza takwimu anavyotaka, akaziwasilisha, zikatupendezesha na tukaamini kwamba ndivyo hali ilivyo. Ukusanyaji wa takwimu ni dhaifu sana. Ni dhaifu kwa sababu hakuna watendaji huku chini. Huku kwenye ngazi ya kijiji, kata hakuna Mabwana Shamba, hakuna watu ambao wanaweza kuwaleteeni taarifa sahihi. Mnachofanya ni kupita na magari, mnazunguka, mnakadiria, hamjaingia kuangalia uhalisi wa hali ya mazao yalivyo. Unakaa tu kwa sababu ni mtaalamu, unasema hapa watavuna tani 100, matokeo yake shamba hilo halizalishi tani hizo 100, labda wanapata tani 15. Kwa hiyo, takwimu zinakuwa si sahihi, tujitahidi sana katika eneo hili la kupata takwimu sahihi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuliangalia hili, nafikiri pia ni lazima tutafute suluhisho hasa katika eneo la wataalam, hawa watalaam wa kilimo. Ninafikiri ingekuwa ni busara sasa kwa Serikali ikatoa udhamini kwa wanafunzi wote wa kilimo kuanzia Cheti, Stashahada mpaka Digrii, wasomeshwe na Serikali kwa sababu tuna mahitaji makubwa sana ya watalaam katika eneo hili. Badala ya kuwapa mikopo, wapewe *grants*, wasome ili waje watusaidie ili hayo mapinduzi yanayofikiriwa leo, yaweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unapoangalia kitabu hiki ambacho kimetolewa na ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, imeainisha mambo kadhaa. Lakini, ninataka kutizama maeneo mawili tu kwamba "zitafanywa jitihada za makusudi za kuvuna maji ya mvua". Lakini hakuna mahala popote pameelezwa kwa miaka miwili iliyopita, wamejiandaa kwa kiasi gani kuvuna maji ya mvua yanayopotea. Tunafikiri kwamba suluhisho la kutusaidia ni pamoja na kuhakikisha maji hayo tunayatumia kwa ajili ya kuleta mabadiliko katika kilimo, mbali katika kilimo, hata kwa matumizi ya kawaida ya binadamu, haya maji ya mvua tumeyavuna kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri, kuna wakati unaweza ukapita pale kwenye Mto Ruvu, ukakuta maji yamefika mpaka karibu ya kingo za daraja na baada ya wiki kadhaa, unakuta maji yameteremka kabisa. Maji haya yanapotea, yanaingia katika bahari ya Hindi lakini, maji hayo ndiyo chanzo cha maji ya matumizi ya binadamu katika mji wa Dar es salaam, kuna jitihada gani za kuhifadhi maji ya mvua katika Mto Ruvu?

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika kitabu hiki hiki wanazungumzia kwamba watakopesha matrekta 330 kwa mwaka lakini, Serikali haielezi ni mpango gani ambao watatumia kuweza kuwakopesha watu matrekta. Ni mipango inayoandikwa ndani ya vitabu, tunasoma kama kasuku, lakini hatutekelezi. Nataka kupata maelezo, wana mfumo gani ili watu waweze kukopeshwa matrekta? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako, mfano mzuri, hapa nina barua ya wananchi wa kijiji cha Ikola. Barua hii ni ya tarehe 15 Machi, 2005. Wakulima hawa walikuwa wanaomba mkopo wa *Power Tiller* na mashine ya kuvutia maji *(Water Pump)*. Toka mwaka 2005 hata kujibiwa barua yao, haijajibiwa, halafu tunasema tutaleta maendeleo na mapinduzi katika kilimo, bado safari ni ndefu!

Mheshimiwa Spika, nimezungumza haya kwa ujumla, sasa nijikite katika eneo ambalo linanigusa sana la tumbaku. Tumbaku katika Jimbo langu, Wilaya yangu ya Mpanda na Tabora pia ambao wanazalisha tumbaku kuliko hata Mpanda, yapo matatizo kadhaa. Moja ya tatizo kubwa ni haya makampuni ambayo yananunua tumbaku. Ushiriki wao katika shughuli za ujenzi na maendeleo ya wananchi ni mdogo sana, hawachangii katika barabara, hawachangii katika madarasa, hawachangii katika zahanati na kadhalika. Lakini kibaya zaidi, kwa zaidi ya miaka 40 tumbaku inalimwa Urambo na Mpanda, bado haijabadili hali ya maisha ya wakulima wetu, ni kwa sababu ya bei, bei wanayopewa wakulima hairidhishi. Gharama ni kubwa sana na eneo ambalo wanatuumiza makampuni haya ni pembejeo na hasa mbolea. Katika mbolea, makampuni yamekuwa yakiwadhulumu, yakiwakandamiza sana wakulima na kuwanyonya.

Mheshimiwa Spika, ni lazima sasa hii mbolea ya ruzuku izidishwe mara dufu ili iweze kuondoa kabisa tatizo la wakulima wa tumbaku kutegemea kupata pembejeo kutoka kwenye makampuni ambayo yanawakandamiza. Lakini, bado haya makampuni hayajihusishi kabisa na maeneo ya uharibifu wa mazingira, ni kwa kiwango tu na ni juhudi za wakulima wenyewe mmoja mmoja na wala si makampuni. Tunahitaji makampuni haya yatoe mchango mkubwa kutokana na uharibifu wa mazingira unaofanyika katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la mazao ya chakula. Sasa hivi kule Mpanda, tunalima Jatrofa. Karibu hekta 81,000 za ardhi nzuri yenye rutuba imekatwa na imeanza kulimwa Jatrofa badala ya kulima chakula. Jana tumemsikia hapa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Taifa, anazungumzia hali ya dunia ilivyo. Wakubwa wanaozalisha nafaka sasa hivi, nafaka yao ama inatengeneza mafuta, ama inalisha nguruwe. Sasa sisi ni lazima tuitumie nafasi hii kuzalisha chakula kwa ajili ya kujitosheleza kama nchi na ziada tuweze kuuza nje. Matokeo yake, tunajiingiza katika kilimo ambacho tunakipeleka katika ardhi yenye rutuba ambayo ingeweza kuzalisha chakula kwa ajili ya watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa ni kwamba Mbeya, Rukwa, Ruvuma, Iringa ilikuwa inaitwa *The Big Four* kwa sababu mazao yote ya Mikoa hii yalikuwa yanakusanywa na mtu mmoja, *National Milling Corporation*, walikuwa wanaweza kujua idadi ya mavuno yanayopatikana katika Mikoa hii. Sasa hivi mnasema mna chakula, chakula hakipo kwa sababu walanguzi wameenda kununua chakula mashambani. Ni lazima tutengeneze muundo wa kuhakikisha kwamba chakula chote kinachozalishwa na wakulima katika Mikoa hii kinahifadhiwa, kinanunuliwa kwa bei nzuri na hasa Serikali iongeze fedha katika *SGR* ili iweze kununua mazao yote ya ziada ya mahindi katika Mikoa hii mine vinginevyo, ni kwamba tutafika mahala tutaanza kwenda kutafuta chakula.

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kumalizika kwa muda wa mzunguzaji)*

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kwamba, hiyo ni kengele ya kwanza au ya pili?

**SPIKA:** Ya pili!

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana! *(Makofi)*

**MHE. ANTHONY M. DIALLO:** Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru kwa kuniona ili na mimi nichangie kwenye hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nimshukuru Mheshimiwa Waziri na wenzake wote kwa *presentation* nzuri ya bajeti ambayo ukiisoma imegusa maeneo yote…

**SPIKA:** Nisamehe, dakika moja!

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo la sasa hivi kwamba *PAC* wakakutane na wageni saa 6.00. Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali wakakutane na wale wageni wetu kutoka Uingereza kwenye ukumbi namba 219. Samahani sana, tutafidia hizo dakika zako, tunaendelea!

**MHE. ANTHONY M. DIALLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nilikuwa nasema, napenda kwanza niunge mkono hoja na nimshukuru sana Waziri, naelewa ni

mahiri sana kwenye sekta hii na nina hakika alichokifanya kule Kusini kwenye korosho, maeneo mengine pia ataweza kutuletea taratibu ambazo zitatunufaisha.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya Wizara ya Kilimo ni mengi, lakini mengine ya kisera, mengine moja kwa moja yanahusu sekta ambazo zinatakiwa kutoa mchango, kuendeleza sekta ya kilimo kutokana na kutokuwa na hali nzuri. Mfano, matatizo ya barabara, matatizo ya shughuli za kibiashara ambazo ziko kwenye Serikali za Mitaa na kadhalika. Kwa hiyo, ni sekta ambayo inahitaji usaidizi kutoka pande zote ili waweze kufaulu.

Mheshimiwa Spika, pia tuna tatizo kubwa sana kwa mazao karibu yote, tunauza mazao yaliyo *raw* (ghafi) na mwono wa watu wetu wengi walio kwenye hii biashara ni kuuza mazao yote haya nje badala ya kuuza bidhaa ambazo zinatokana na hayo mazao. Kwa hali ya namna hiyo, tunakuwa na matatizo makubwa sana ya kuweza kupata kipato ambacho wakulima na Taifa kwa ujumla kiuchumi, tungeweza kupata.

Mheshimiwa Spika, tuna matatizo pia ya *storage* au jinsi ya kuhifadhi, jinsi ya kupata nyenzo mfano kama majokofu yakatumia umeme kwenye sehemu nyingi kwa sababu umeme haupatikani kila sehemu, haya maghala hayako kila sehemu. Nadhani kama nilivyosema awali ni vizuri tuangalie uwezekano wa kuunganisha hizi sekta zote zinazoshabihiana ili tuweze ku-*move* mbele.

Mheshimiwa Spika, mfano, *point* ambayo ameizungumza hapa ni ya maji, jinsi ya kuvuna maji ya mvua. Sijui, wataalamu wetu wanasafiri sehemu nyingi sana, hawawezi kuona, mimi nikienda India, nikienda China, hata kama siyo mtaalamu wa kilimo, unaona kabisa mito yote imewekewa *dikes* kwamba maji hayawezi kutoka tu yakaenda baharini bila kutumiwa sehemu nyingine, yanapotuama unakuta wanayatumia kwenye uvuvi, wanayatumia kwenye umwagiliaji. Sasa, vitu kama hivi vinahitaji nadhani *coordination* za kuweza kutufikisha tunakotaka.

Mheshimiwa Spika, kuna suala moja ambalo Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake ukurasa wa 97 amelizungumzia. Hii *zoning* ya mazao kwamba sehemu fulani mnaweza kulima mpunga, sehemu fulani mkalima kitu fulani. Inaonekana imewekwa kwenye nadharia tu na iko *focused* kwa ajili ya anayekuja kuwekeza ili aone wapi kwa kwenda na ndio maana tusishangae kwamba tunapeleka watu kulima jatrofa kwenye ardhi ambayo ni nzuri sana ambapo *bio-fuel* tungeweza kuipata hata kwenye mahindi, maana siyo lazima upate kwenye jatrofa tu. Wenzetu Marekani mahindi sasa hivi yako juu, bei zote duniani ziko juu kwa sababu bei ya mahindi imepanda kwa sababu anaitumia kwenye kuzalisha mafuta. Sasa kwa nini tutumie jatrofa kitu ambacho hata ukiwa na kiu huwezi ukakata, ukanywa? Kwa hiyo, ni maeneo ambayo tunatakiwa tuwasaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu usimamizi wa masoko yetu, kweli tuna matatizo makubwa sana. *Cartels* au njama za kuungana ili wamuumize mkulima, bado zinaendelea. Sheria ipo, haitekelezwi! Kwa hiyo, unakuta kwamba tuna matatizo mengi

ambayo nadhani siyo ya Wizara moja tu, inatakiwa *coordination* ifanyike au kuwe na utaratibu mzima wa kuangalia matatizo yanatoka wapi.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie zao la pamba maana ndiko ninakotoka. Matatizo ya kiujumla ya zao la pamba ni yale yale ambayo tunayaona kwenye mazao mengine, lakini nadhani kwa upande wa pamba yamezidi sana.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia tangu nizaliwe, nimekua, wafanyabiashara wa pamba kazi yao ni kuuza nyuzi au pamba ambayo imechambuliwa nje. Utakuta kile kiwango cha kilimo mwaka 1960 na kiwango cha pamba inayouzwa, yaani *percentage wise* siyo *volume*, unakuta *actually* sasa hivi tuna-*export more* kuliko tulivyokuwa tunafanya hapo awali wakati wa *Textile Mill,* Shirika la *Texco* na wengine walikuwa na viwanda vingi vya kuzalisha nguo.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi, *it is worse,* asilimia kubwa sana ya pamba yetu inakwenda kama nyuzi na hii utalia, utalia tu na utoe machozi ya damu kwa sababu bei ya nyuzi za pamba inabaki ni hivyo hivyo na kama alivyosema Mheshimiwa kutoka Meatu, wakati zao hili lina bei nzuri, hapa tunazuia watu wasiuze. Sasa tunazungumza jamani soko huria, kwa nini usiseme kwamba ukiivisha pamba Februari, uza? Ukiivisha pamba mwezi wa Kumi na mbili, uza kwa sababu hali ya hewa hapa nchini inabadilika badilika sana sasa hivi. Sehemu ambako kulikuwa na mvua, sasa hivi utakuta hakuna mvua tena.

Mheshimiwa Spika, *gene capacity* imeongezeka, nakubali, lakini utakuta nia yake ni kupeleka nyuzi za pamba nje badala ya kui-*process* hapa. *Textile Mills* zimepungua kwa sababu tulikuwa na *Textile Mills* muda fulani nyingi sana na zilizopo teknolojia yake ya zamani kweli, badala ya kuunga nyuzi kwa *splicing*, inaunga nyuzi kwa vifundo. Kwa hiyo, ile *material* inayotengenezwa kuna masoko *limited* kwa kuwa siyo masoko yote yanayoweza kununua hiyo nguo ambayo tunaitengeneza.

Mheshimiwa Spika, tuna matatizo sana kwenye soko, nadhani Waheshimiwa wengi sana wamezungumzia mambo ambayo yanahitaji ufumbuzi, la sivyo wananchi watakuwa wanalalamika. Mfano, mwaka huu bei ya pamba, *influence* kubwa ya bei hiyo kubaki pale ni mabenki. Mabenki yalipokuja kuwakopesha wanaonunua pamba, yakawaambia usinunue kwa bei zaidi ya hii kwa sababu siwezi kujua kwamba unaweza ukaanza kula hasara, nikala hasara mimi! *In so doing*, ina maana wamepanga bei, siyo wale wanunuzi, lakini ni mabenki yamepanga bei. Kwa hiyo, tunaweza kulia mpaka tutoe machozi kwamba nunua pamba kilo moja kwa Sh.500 lakini haiwezekani, kaambiwa huyu kwamba nakukopesha pesa, nenda ukanunue pamba kwa Sh.400 au Sh.450 mwisho na ndio kinachotokea. Sasa Wizara hili nadhani wanalifahamu na bila kulitatua, tutapata matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, tuna maeneo mengi ambayo tunaumia *exchange rate* nayo ni matatizo wakati pamba mnaanza kuuza nje, ndiyo *exchange rate* ina-*drop*. Kwa hiyo, yule anaye-*export,* atakula hasara tu hata kama alijua hilo linaweza lisitokee.

Mheshimiwa Spika, ufumbuzi wetu, cha kwanza ni *cooperatives* kwa sababu kwenye *cooperatives* usambazaji wa mbolea, usambazaji wa dawa, viatilifu na kadhalika unafanyika kwa *coordination* ambayo unaweza kuikadiria na ukapata matokeo. Lakini kwa hawa wanunuzi wanaokuja mmoja mmoja wanafika mpaka vijijini kule sidhani kama tutafika. Takwimu kwanza zitakuwa hovyo, maana kila mmoja anajitahidi kuficha ili adanganye asilipe *cess.*

Mheshimiwa Spika, lakini pia, upande wa *markerting*, nadhani Wizara sasa hivi ni vizuri tukazanie maeneo ambayo tuna *competitive advantage* kuliko wengine. Mfano, kwa sasa hivi kuna hii kilimo hai na kuna kuuza pamba hai. Sasa hivi kwa taarifa zao, Tanzania ndio wa kwanza Afrika kwa kuuza pamba hai, lakini hatuendelezi mashamba. *So far*, mwaka jana tumeuza tani 1663, lakini bado tulikuwa *number one*, hata kwenye *chart* ya *organic cotton* duniani, tuna-*appear* pale kama nchi, siyo kama *others*, maana maeneo mengi tunaonekana kama *others* kwenye *Continent* la Afrika. Kwa hiyo, tungeweka nguvu zaidi kwa sababu bei yake iko *between 15%* na *25% more* kuliko ile *conversional cotton*. Sasa ni maeneo ambayo tunaweza kujizatiti, tuna *competitive advantage* kwanza, ardhi yetu sehemu kubwa haihitaji mbolea kwenye hii *black cotton soil* ambako pamba inalimwa.

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu pia wa kuangalia maeneo mengine, mfano, haya mambo ya masoko imekuwa ni kilio karibu kila mwaka. Wizara nadhani kuna umuhimu wakafanya *plan* mapema, *at least* mtu anajua kwamba mwaka huu nalima pamba, gharama yangu ni shilingi kadhaa kwa kilo. Sasa kama ninajua bei na ndilo tatizo ambalo tunalipata kila mwaka kwamba kila mwaka mtu analima, anamaliza kulima, hajajua atauza kwa bei gani, ana pamba yake kwenye ghala na *actually* hatuna maghala nyumbani kwetu kule, inatafuta chumba kimoja ndani ya nyumba, unaiweka pamba yako unasubiri soko, baada ya msimu kufunguliwa ndio unapeleka, kuna tatizo kweli la madeni.

Mheshimiwa Spika, sasa, nadhani tuangalie uwezekano wa ku-*hedge* wakulima wetu, unawa-*protect* kwa njia ambayo nina hakika kama hii stakabadhi ya mazao kama itasaidia, itatusaidia sana. Lakini pia haiwezi kusaidia kama muda bado ni ule wa kuuza pamba ndio muda ule ule wakati pamba duniani haihitajiki, tutaendelea nayo. Kama alivyosema Mheshimiwa Mpina, mwezi *April*, *March*, bei ya pamba duniani huwa juu sana. Tunapoanza kuuza pamba mwezi Juni, karibu masoko yote au nchi zote zinazolima pamba na zenyewe zinaanza kuivisha ambazo tuko karibu nazo hapa, mfano, *Mozambique* na kadhalika, kwa hiyo, kuna umuhimu wa kuangalia utaratibu mpya ambao utawasaidia zaidi wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, naona muda karibu unakwisha, nipende pia kushukuru sana Wizara kwa *efforts* wanazozifanya kwa sababu ni kama ndege ilikuwa inakwenda chini, sasa hivi wanajaribu kwanza ui-*stabilize*, halafu ndio uanze tena kwenda juu. Wanajitahidi sana, napenda niwashukuru na ninaunga mkono hoja iliyo mbele yetu, asanteni sana! *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante Mheshimiwa Diallo kwa mchango wako unaodhihirisha uzoefu mkubwa katika zao hasa hilo la pamba.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie katika hoja iliyoko mbele yetu ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

Mheshimiwa Spika, naanza kutoa mchango wangu wa jumla kwa kuipongeza Wizara kwa jitihada inazozifanya za kuboresha kilimo. Jitihada hizo zinaonekana katika mikakati iliyoandaliwa na kuelezwa hapa katika Bunge lako Tukufu kupitia kitabu hiki cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, wote tunakubaliana kwamba kilimo ingawa tunakiita ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu, lakini bado kiko duni. Watanzania zaidi ya asilimia 70 wanategemea sekta ya kilimo kwa maisha yao, lakini kilimo bado kiko duni na kwa maana hiyo kuna kazi kubwa mbele yetu ya kufanywa na Serikali ili kuweza kukibadilisha kilimo. Ukuaji wa asilimia nne wa kilimo, kwa kweli hauonyeshi kama kuna mwelekeo mzuri wa kuweza kukiboresha kilimo hiki kuondokana na uduni uliokuwepo na kukifanya kilimo kuwa na tija. Kwa hiyo kuna mambo mengi ya kufanya.

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo mengi, moja, likiwemo lile tatizo la ufinyu wa bajeti. Bajeti iliyotengwa mara hii haifikii hata ile asilimia 10 ya uamuzi wa nchi za *SADC* sambamba na uamuzi wa Ilani ya Uchaguzi, bajeti ya kilimo kufikia asilimia 10 ya *total budget* ya Serikali. Kwa hiyo, katika miaka ijayo tufikirie hili ili angalau kuongeza ukuaji wa kilimo, asilimia nne ni chini sana.

Mheshimiwa Spika, kilimo kinapambana na matatizo mengi. Katika Ilani ya Uchaguzi yameainishwa baadhi, la kwanza linasema, kutokueleweka kwa kanuni za kilimo bora. Ni kweli na hata hotuba imeelezea hilo kwa sababu kilimo bora kinatakiwa wakulima waelimishwe hizo kanuni za kilimo bora. Lakini waelemishaji tunaowatumia zaidi na Maafisa Ugani *(Extension Officers)***,** imeainishwa hapa kwamba *Extension Officers* hawatoshi kabisa. Lengo ni kuajiri 2500 kwa mwaka, lakini tumeajiri 309 mwaka 2007/2008. Kwa hiyo hapa kuna kazi kubwa ya kufanya ili mkakati huu uweze kutekelezeka. Serikali ijipange vizuri tupate Maafisa Ugani wa kutosha. Kama ilivyoelezwa, Maafisa Ugani hawa wasambazwe katika vijiji vyote na kila kijiji kiwekewe malengo na Maafisa Ugani wasimamie malengo hayo. Afisa Ugani anayevuka lengo, awe *motivated*, apatiwe kama *bonus* au zawadi yoyote ili aweze kufanya kazi yake vizuri. Kijiji kinachovuka lengo, basi nacho kipatiwe *award* kukubaliana na kazi nzuri waliyofanya ili waweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile kuna tatizo la UKIMWI. Hapa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameainisha kuwa kuna mambo fulani yanaendeshwa katika Wizara kuhusiana na UKIMWI kwa sababu kila Wizara ina *budget line* ya UKIMWI, wananchi wanasema elimu ya UKIMWI inatolewa katika ngazi za juu tu huku mijini, haijafika vijijini. Kwa hiyo, nashauri Serikali kupitia Maafisa Ugani, wanapotoa mafunzo kwa Maafisa Ugani wapewe pia hii elimu ya UKIMWI ili wanapokwenda kule vijijini

wanapotoa elimu ya kilimo, vile vile watoe na elimu juu ya janga la UKIMWI, hii inaweza ikasaidia na elimu ya UKIMWI kufika huko katika ngazi ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine lililoainishwa ambalo tunapambana nalo, ni kuwa wakulima walio wengi wanalima vishamba vidogo vidogo. Hii inaeleweka, ni muhimu kuwa na kilimo cha mchanganyiko, mashamba makubwa na mashamba madogo madogo. Lakini wakulima wetu hawawezi wakalima mashamba makubwa kutokana kwanza na zana duni wanazozitumia, wanatumia zana za tangu enzi za ujima, za mababu na mabibi zetu, kijembe cha mkono na pengine kijembe chenyewe cha mkono kimebakia nusu wanaendelea kutumia hicho hicho, hakimruhusu kabisa kulima shamba kubwa. Lakini hata hilo shamba dogo analolima, basi kwa nini halitoi tija kubwa, mavuno *per acre* ni madogo sana, lakini sababu zinajulikana. Sababu inazungumzwa kuwa mbegu bora hazitoshi. Kishamba chake kidogo, wanahitaji mbegu bora, hamna. Ni asilimia 54 ya mahitaji ya mbegu bora zilizoweza kupatikana na katika hizo asilimia 27 tunategemea kutoka nje. Hivi jamani Watanzania, tumeshindwa kufanya *multiplication* ya hizi mbegu zetu tukapata za kutosha humu humu ndani, tukapata na kuwagawia watu wetu angalau wakalima wakapata tija! Kwa hili, tujitahidi, tuongeze mashamba ya uzalishaji wa mbegu na tuachane na kutegemea nje, tumeshaona kutegemea nje wakati mwingine kunatuangusha kasipopatikana tunaharibikiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile kuna tatizo la mbolea, tumesema mbolea haiwafikii watu walio wengi wengine wanapata na wengine hawapati hata kama wanahitaji. Ni vema mbolea ipatikane kwa wingi na kwa bei nafuu kwa sababu bei ya dunia tunaijua ilivyokuwa ghali. Hatuwezi kununua mbolea nje tukawatosheleza watu wetu kwa hiyo juhudi ziendelezwe kwa nguvu zote ili mbolea ipatikane humu ndani.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna tatizo la zana za kilimo. Tulileteva hapa Bungeni *power tiller* moja inauzwa milioni tano, ni mkulima gani huyo mdogo wa kijijini kule anayeweza kutoa milioni tano akanunua trekta kwa bei hii? Hapa ndiyo linakuja lile suala la kuwa na Benki ya Kilimo, lakini vile vile kwa wakati huu ambapo benki bado haijawa tayari suala la kuwahamasisha wakulima wakajiunga na vikundi angalau basi kwa kuanzia kikundi cha watu watano mpaka kumi, *maximum* iwe kumi wapate mkopo kupitia *SACCOS* kwa kuchangiana wanunue *power tiller* moja halafu watakuwa wanasaidiana kwa kutumia trekta lile lile na wakamaliza mashamba yao, watakodisha na wengine na utaratibu wa malipo utalipwa kutokana na mazao ambayo watayazalisha.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilishazungumzwa sana hapa ni tatizo la kutegemea mvua. Sasa hivi kuna tatizo la *global warming*, hali ya hewa imebadilika haipo kama vile tulivyokuwa tunaona ikifika muda fulani tunapata mvua, ikifika muda fulani tunapata kiangazi hivi sasa saa yoyote linaweza kutokea lolote. Tatizo hili ndilo lililozungumzwa kwamba kilimo chetu kimeshuka kwa sababu ya kutegemea mvua lakini kwa wakati huu hali ya hewa inabadilikabadilika.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu tumejaliwa kuwa na maji kila pembe, hapa Dodoma tulipo, ukichimba tu kidogo, unasikia maji yanatoka. Tuna mito na maziwa makubwa, tufanye jitihada kutumia maji haya. Mungu ametuletea haya maji siyo

tuyatizame tu lakini tuyatumie kwa manufaa yetu kwa kutumia maarifa na akili zetu ambazo Mwenyezi Mungu ametupa.

Mheshimiwa Spika, kuna maji ya mvua yakija yanakuja mengi baada ya muda kunabakia kukame, hakuna tunachopata. Kuna nchi ambazo ni jangwa kama vile Misri, Uarabuni lakini wanazalisha mpaka matunda wanakuja kutuuzia sisi, *juice* tunakunywa za kutoka nje. Hiki ni kitu cha aibu, utajiri tunao, tuuendeleze utajiri huu ili utunufaishe na kututoa katika janga la umaskini.

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo la kutumia nguvu kazi za akina mama kwa kilimo. Asilimia kubwa ya wakulima ni akina mama, tumechoka jamani kulima, akina baba tuwahamasishe na wao washiriki katika kilimo, wanashiriki katika kuvuna tu na kupeleka mazao sokoni. Tuwahamasishe walime wawasaidie na akina mama.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni utafiti, ili tuendeleze kilimo chetu, suala la utafiti litiliwe mkazo. Bajeti ya utafiti iwe inaongezwa, kuna vituo vingine vya utafiti havina hata vitendea kazi kwa maana hiyo matokeo ya utafiti hata yawe mazuri kiasi gani hayawezi kuwafikia walengwa.

Mheshimiwa Spika, tulikwenda kituo cha Mikocheni tumekuta hawana gari, wanagari bovu yaani ile gari wakitaka kusafiri fundi awe ndani ya gari hilo na spana zake ziwemo humo. Wakienda kilomita moja, wasimame fundi ateremke atengeneze gari kwanza halafu ndiyo liende mbele. Kweli matokeo ya utafiti yatawafikia walengwa? Mabwana Ugani hawana hata pikipiki, ni tabu sana, tujitahidi kuboresha masuala haya.

Mheshimiwa Spika, tatizo la njaa duniani, wenzangu wamezungumza sana lakini mimi nasema njaa haina itikadi, haina CUF, CCM, wala CHADEMA, viongozi wote wa Serikali na chama, tushirikiane kuwahamasisha watu kulima ili kuondokana na njaa. Vilevile Serikali ijitayarishe kununua mazao ya wakulima yakiwa mengi, wawapatie masoko ili wanufaike na shughuli wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali ijitayarishe kununua mazao ya wakulima yakiwa mengi, wawapatie masoko ili wanufaike na shughuli wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Watu wanalima nafaka, mizizi na matunda lakini hakuna usimamizi, soko liko wapi? Naomba tuhamasishe uwekezaji wa viwanda vya usindikaji ili watu wetu wapate manufaa na kilimo chao hicho.

Mheshimiwa Spika, kunazalishwa ndizi nyingi hapa nchini hata baadhi ya Wabunge wanasikitika kwa kukosa soko. Mfano Mheshimiwa Ligallama mwaka jana amekuja hapa na kusema jamani twendeni kule Kilombero mbona kuna ndizi nyingi, sina namna ya kuzifanya, kuna nyingine ni kubwa kuliko hata ukubwa wa Mheshimiwa Waziri wangu wa Kilimo lakini zinauzwa shilingi elfu mbili tu kwa mkungu, anatafuta

watu wakanunue hizo ndizi, kukiwa na hizi Bodi za Mazao Mchanganyiko labda watasaidia.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kilimo na vijana. Tumepata taarifa kuwa vijana hawapendi kilimo lakini hawapendi kilimo kutokana na hali yake ya sasa ilivyo. Kwanza, kilimo hakina *return* ya haraka haraka, hakuna miundombinu kwenye kilimo hamna mikopo, kijana gani atakipenda? Lakini kilimo kikiboreshwa, watarudi wakalime. Tuendeleze *youth settlement,* tuwape maeneo vijana, tuweke miundombinu, tuwape fedha, tuzungumze na *Habitat* wawajengee nyumba za bei nafuu. Kijana gani anapenda kuzurura kupita kuuza pipi huko Dar es Salaam kutwa nzima hajui wakati *future* yake ikoje? Kila mtu anataka aishi maisha ambayo yapo *decent*, awe na familia yake na aendeleze maisha yake. Tukitayarisha mambo yetu vizuri katika kilimo, nina hakika vijana tutawapata.

Mheshimiwa Spika, lingine linahusiana na kuhamasisha kaya. Kila kaya ikiwa na angalau hekari moja na ya kilimo ambacho kimelimwa vizuri, kisasa na kuna mbolea, watumie pembejeo zote kama mbegu bora, nadhani tatizo la njaa litaondoka. Hili linawezekana kwa sababu historia inatuambia hivyo kwamba siasa ni kilimo, kilimo cha kufa na kupona, mbona watu walilima na matokeo yalionekana kuwa mazuri! Kwa hiyo, uwezo wa kuboresha mambo yetu tunao, isipokuwa tujipange vizuri kuboresha kilimo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ni kuhusu Bodi za Mazao haya ya Kawaida ya Biashara, ziendelee kuimarishwa. Bodi za pamba, tumbaku, chai na kadhalika ziimarishwe waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja (*Makofi*)

**MHE. MOHAMMED S. SINANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii adimu ili nami nichangie hoja iliyopo mbele yetu.

Kwanza kabisa, ninapenda kumshukuru Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Wasira, kwa niaba ya wananchi wa Mtwara, kwa kazi nzuri aliyotufanyia yeye akishirikiana na timu yake nzima kwa kuondoa tatizo la bei ya korosho. Kwa hakika, tunakupongeza kwa hilo ingawa umejipalia mkaa sasa unatakiwa kila mara utangaze kujiuzulu pale panapokuwa na matatizo ya kilimo, pole sana kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Mheshimiwa Waziri ulifanya hivyo kwa kuona ni jinsi gani wananchi wa Mtwara walivyokuwa wanateseka na kunyanyasika na walanguzi

wa zao hili. Ukakerwa na ukaahidi na kujitolea mhanga kwamba ulikuwa tayari kuachia ngazi kwa ajili yetu, tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, pia ninapenda kutoa pongezi kwa Kituo cha Utafiti cha Naliendele, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya ya utafiti wa mazao kama korosho, ufuta na kadhalika. Kwa hakika, wataalamu hawa wanafanya kazi nzuri sana hata baadhi yao husafiri kwenda nchi za jirani kuwasaidia wenzetu. Wamekwenda Msumbiji, Ghana na katika nchi nyingine mbalimbali kwenda kutoa elimu hii ya zao la korosho na mazao mengine. Kwa hakika, watafiti wa Naliendele wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, pia ninapenda kutoa pongezi kwa Chama cha Ushirika cha Mtwara, kwa kazi nzuri walioifanya. Ninaomba kazi hii ambayo imeanzishwa na Mheshimiwa Wasira, iendelee pia katika pembejeo za korosho. Safari hii pembejeo zimechelewa na zitaathiri zao la korosho. Mavuno yataathirika, hayatapatikana kwa kiwango ambacho tulitarajia. Wanasema udhu wa Ijumaa unaanza Alhamisi. Kwa hiyo, naomba safari hii Wizara yako ianze mapema kushughulikia suala la pembejeo za korosho na bei nayo iangaliwe ili wananchi waweze kumudu pembejeo hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, naona kuna tatizo moja katika Wizara ya Kilimo, tatizo kubwa ni taarifa haziwafikii wakulima au walengwa. Tafiti zilizofanywa kwa mfano Naliendele, wamefanya tafiti kwa zao la korosho. Wakulima wengi hawajui na hawajapata taarifa kwamba kuna korosho hivi sasa unaweza ukapanda na kuvuna baada ya miaka miwili, wamezoea korosho zilezile ambazo unapanda na kuvuna baada ya miaka mitano. Vilevile hawajui kuna tafiti zimefanywa na kwamba kuna mbegu mpya za ufuta, inaitwa Naliendele 92, Ziada 94 na Lindi 2002.

Mheshimiwa Spika, mbegu hizi ni za kisasa ambazo huvunwa kati ya siku 110 mpaka 120 ukilinganisha na mbegu za asili ambazo huvunwa baada ya siku 180 na pia zinahimili magonjwa. Ufuta huu ni ufuta mweupe ambao ndiyo wenye soko zuri katika soko la dunia. Taarifa hizi hawana wamezoea mbegu asili ambazo ukipanda unapata iko 300 ukilinganisha na kilo kati ya 1000 na 1200 kwa hekta kwa mbegu hizi za kisasa ambazo zimefanyiwa utafiti.

Mheshimiwa Spika, ufuta ni zao la kwanza la mafuta katika nchi hii, pia ni zao la pili kwa Mikoa ya Kusini ukiondoa korosho. Kwa hiyo, ni zao muhimu sana katika Mikoa hii miwili, ni zao mbadala. Badala ya kutegemea zao la korosho, ufuta ni zao la pili ambalo linaweza likakomboa mkulima na pindi wakipata taarifa hizi kwamba ufuta mweupe ndiyo hasa unaotakiwa katika soko la dunia na ufuta huu ambao umefanyiwa utafiti unaweza kuvuna kati ya kilo 1000 mpaka 1200 kwa hekta lakini nina hakika taarifa hizi hawana. Asilimia 80 ya wakulima wa ufuta, wa Kusini, hawana taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, pia nilipata bahati kukutana na Mbunge wa Dodoma naye hazijui tafiti hizi. Kwa kutoa ushahidi wa kutokuwa na taarifa sahihi, nilikwenda banda la sabasaba la *TANSEED International*, nikakuta kuna ufuta mweupe huu ambao nimeuelezea hapa Naliendele 2002. Nikamwuuliza wameupata wapi? Wakasema tumeupata Mtwara. Nikawauliza, mnalima wapi shamba hili la mbegu za ufuta? Wakasema tunalima Morogoro. Nikauliza kwa nini msilime Mtwara? Wakasema sisi tunafuata soko. Sasa kwenye soko wakati Mtwara na Lindi ndiko wanakovuna asilimia 75 ya ufuta lakini shamba la mbegu lipo Morogoro, wao hawajui hilo. Nikawashawishi na kuwaambia waje Mtwara tutafanya utaratibu wa kupata ardhi mlime mbegu hizo Mtwara. Kwa hivyo inaonekana tafiti hizi zinafanywa lakini tulio wengi hatupati taarifa. Naishauri Serikali kwamba tafiti zikishafanyika na sisi Wabunge tujulishwe tuwekewe katika *pigeon hole* zetu.

Mheshimiwa Spika, nikisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri, naona kuna mbegu za mhogo, kuna mbegu za mahindi lakini wakulima wengi taarifa hizi hawana na baadhi ya Wabunge wengi hatuna. Kwa hiyo, tunaomba hizi taarifa zitolewe ili wananchi wafahamu haya.

Mheshimiwa Spika, pia ninashauri hawa washiriki wanaponunua ufuta kuwe na mizani mbili, moja ya ufuta mweusi na moja ya ufuta mweupe na bei zitofautiane kwa sababu katika soko la dunia sasa hivi ufuta mweupe imefikia dola 2300, ufuta mweusi hauna bei nzuri katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, jitihada zikifanywa na wananchi wakaelimishwa na pembejeo zikipatikana, wananchi wanaweza wakafaidika na umaskini wao ukapungua kwa kiasi kikubwa. Mimi sijaona hata tani moja ya wakulima ambao wamevuna ufuta mweupe.

Mheshimiwa Spika, zao la ufuta katika Mikoa ya Kusini lilipanda kutoka tani 1900 mwaka 1990 mpaka tani 40,000 mwaka 2005 na ikalipatia Taifa karibu bilioni 25. Wakulima waliweza kupata bilioni 25, ni kiasi kikubwa cha fedha kwa hiyo siyo zao la kulifanyia mchezo hata kidogo. Ninaomba sana Wizara itusaidie kwa hili kwa sababu hili ni zao la pili la kibiashara katika Mikoa yetu. Zao la ufuta lina tatizo, madawa hayatoshi na wakulima hawafahamu taarifa za ufuta mweupe, wanaujua ule ule wa zamani. Napenda kusisitiza kwamba suala hili Mheshimiwa Waziri aliangalie.

Mheshimiwa Spika, sasa nije katika suala la ubanguaji wa korosho. Serikali nia yake kubwa ni kubangua korosho badala ya kuuza korosho ghafi kwenda nchi za nje, lakini ndoto hii inavyoelekea itachukua muda mrefu, tunahitaji kutafuta njia mbadala.

Ninashauri tuanzishe viwanda vidogovidogo waanze kwa ku-*process* kwa kiwango kidogo (*semi- process*) kitu ambacho kinawezekana. Vijijini kuwe na viwanda vidogo ambavyo wataingia mkataba na viwanda vikubwa wabangue korosho kwa hatua ya mwanzo baadaye zile korosho zilizobanguliwa kwa hatua ya mwanzo zipelekwe katika viwanda vikubwa kuendelea na hatua zinazofuata kwa sababu hatua zinazofuata zinahitaji ujuzi zaidi na utaalam zaidi labda ni vifaa vya kufanyia kazi vingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, hatua hii ya mwanzo ikiwa kwa mfano kiwanda cha Masasi kitaingia ubia au kitaingia mkataba na wazalishaji au wabanguaji wadogo ambao viwanda vidogo vitajengwa katika maeneo yao, wanaweza wakabangua korosho kwa hatua ya kwanza ambayo haihitaji mitambo *sophiscated* na ambayo ni aghali zaidi ni *boilers* na mikasi ya kukatia korosho, ikianzia hatua ile, basi hatua zinazofuata wapeleke katika viwanda vikubwa waendelee na hatua zinazofuata. Mpango huu utasaidia kuleta ajira katika vijiji pia itasaidia korosho zetu kubanguliwa kwa wingi zaidi ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, hizi korosho ndiyo zao ambalo sisi tunalitegemea, ni lazima ufanyie kazi kile ambacho unacho mkononi. Kwa hiyo, korosho zikibanguliwa, nchi itapata fedha za kigeni na vilevile wananchi hali zao zinaweza zikaimarika kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, niingie katika zao la mhogo. Mhogo hauna soko katika Mkoa wa Mtwara zaidi ya kuliwa tu lakini kwa kutengeneza vitu kama *starch* na kemikali zingine, bado haujafikia hatua hiyo. Kwa hiyo, tunaiomba Wizara ya Kilimo, ijitahidi kwa hilo ili tupate ujuzi au utaalam wa ku-*process* mhogo kwani ni mwingi na unaweza kuleta ajira kwa kutumia mazao yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi sina zaidi ya kuendeleza, nisipigiwe kengele ya pili kwa leo nimeona nichangie kwa kiasi na ninaunga mkono hoja, ahsante sana.

**SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Sinani, umeepuka sekunde kengele ya pili hiyo, namwita sasa Mheshimiwa Anastazia Wambura baada ya hapo ajiandaye Mheshimiwa Elisa Mollel.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuhangia katika hotuba hii ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mnyimi wa fadhila kama nisipompongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Kuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii, kwa ufafanuzi wao wa kina katika masuala mbalimbali ya kilimo ambayo

tumeyasikia katika hotuba yake ya bajeti. Hotuba ilikuwa ni nzuri na imejibu mambo mengi ambayo hata mimi binafsi, nilikuwa nikijiuliza mara nyingi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, narudia tena kuipongeza Wizara kwa kutekeleza mambo mengi ambayo yapo katika Ilani ya CCM ya mwaka 2005. Kwa kweli, imetekeleza mambo mengi. Lakini nitaje machache ambayo nimeyaona na kuyashuhudia. Kwa mfano, ni kilimo cha umwagiliaji, Wizara hii imejitahidi kwa kupitia mpango wake wa *ASDP* na kwa kushirikisha Halmashauri zetu, imeweza kuimarisha kilimo cha umwagiliaji katika maeneo mbalimbali. Kwa mfano, maeneo ya Mtwara, tuna umwagiliaji katika bonde la Kitere, bonde la Mahurunga, vilevile wananchi wanajitahidi katika bonde la Lwelu lakini wanapeleka maombi yao katika Wizara wanakwama kutokana na kwamba eneo hili liko katika Manispaa. Bonde hili lina *potential* kubwa sana ya uzalishaji wa mazao ya mboga mboga pamoja na mpunga, tunaiomba Wizara ilifikirie suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuna utekelezaji mwingine wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 katika kuhakikisha kwamba wananchi wanapata mbegu bora. Kwa mfano, katika Manispaa ya Mtwara, tumeweza kuzalisha miche bora ya korosho ipatayo elfu 16 na zaidi. Kwa hiyo, haya ni maendeleo makubwa ambayo tumeweza kuyaona na miche hii itasambazwa kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda kuipongeza Wizara hii kwa kuimarisha ushirika. Kama alivyotangulia kusema Mheshimiwa Sinani. Kwa kweli, uimarishaji wa Ushirika katika Mikoa ambayo inalima zao la korosho na kuimarisha huku hasa kwa kuondoa madeni katika Vyama vya Ushirika, kumewezesha bei ya zao la korosho kupanda na kwa wastani mwaka jana bei ya korosho shambani ilifikia shilingi 700 hadi 750 kwa kilo moja. Lakini wakulima wenyewe pia wanaendelea kushukuru kwa sababu zoezi hili limepunguza wizi kwa kiasi kikubwa. Wizi wa korosho kwenye mashamba ulipungua na hata wale ambao walikuwa hawavuni korosho kwa miaka mingi mwaka jana wameweza kuvuna korosho zao na wameweza kuziuza kwenye vyama vya ushirika, kwa hiyo, wanashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuzungumzia mpango wa maendeleo ya kilimo, *ASDP*. Mpango huu, kwa kweli umechambuliwa vizuri sana. Ukiangalia vitabu vyake na hata mwaka 2006 Mheshimiwa Waziri wa Kilimo aliweza kutuwasilishia mpango huu mzima, ni mzuri sana, umechambua matatizo mengi na vilevile umetuonesha jinsi gani matatizo mengi ya kilimo yanaweza yakatatuliwa.

Mheshimiwa Spika, kuna swali hapa ambalo nafikiri ni la msingi sana tujiulize. Mpango huu tunao na una gharama kubwa sana, lakini je unatafsiriwa vipi kupunguza umaskini huu wa mahitaji ya msingi? Kwa sababu tunaona kwamba bado tunao umaskini

mkubwa na *level* ya umaskini wa mahitaji ya msingi, ni asilimia 21 kwa mwaka 2007 na hii tunaipata katika kitabu cha *Poverty and Human Development Report.*

Mheshimiwa Spika, vilevile katika malengo ya milenia, tupunguze umaskini huu kufikia nusu yake itakapofika mwaka 2015, je, mpango huu wa *ASDP* utafikisha nusu hii? Hili ni swali ambalo nimekuwa nikijiuliza na hata juzi nilipouliza swali langu, nilikuwa nimelenga kutaka kujua kama kweli tunawea tukafikia ukuaji wa uchumi wa asilimia kumi itakapofikia mwaka 2010. Mheshimiwa Waziri aliniahidi kwamba atanijibu katika hotuba yake, namshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, tunayo maswali mengi sana vijijini, kila tunapopita vijijini, wakulima huwa wanatuuliza na mara nyingi wanachouliza ni kwamba ninyi mnapokazania elimu, sisemi kwamba elimu ni mbaya, lakini haya ni maswali ambayo tunaulizwa, kwamba mnakazania elimu lakini kilimo vipi mbona mmekiacha? Hii inaonesha kwamba kilimo bado hakijajitokeza au bado hakijawa wazi. Serikali haijaweka wazi vijijini kwamba inafanya nini, pamoja na kwamba yapo mambo mengi ambayo yanafanyika lakini bado uelewa ni mdogo kuhusiana na Serikali inachokifanya.

Mheshimiwa Spika, tunazo sera nyingi katika mpango wa *ASDP*, kuna Sera ya Ardhi inazungumziwa, kuna Sera ya Maji inazungumziwa na Sera ya Huduma ya Fedha Jinsia na Ushirika, lakini ukichunguza sana kuna masuala ambayo yanatiliwa mkazo. Sera ya Jinsia, haikuwa wazi na haikupewa kipaumbele katika bajeti. Ninaomba niisome kwa kifupi Sera hii inasema kwamba:-

*"Kipaumbele mahsusi kitakuwa katika kuhakikisha kuwa wanawake wanapatiwa ardhi na rasilimali nyingine za uzalishaji, mafunzo na teknolojia ya kurahisisha kazi".*

Mheshimiwa Spika, hii imo ndani ya kitabu kile cha mpango wa maendeleo ya kilimo. Ukiangalia sana masuala ya jinsia yamewekwa kando kabisa hususani wanawake, vijana na wazee. Mimi nilitarajia kipaumbele hiki kijitokeze kama vile suala la umwagiliaji lilivyojitokeza ambapo katika mpango mzima tunaambiwa kwamba katika umwagiliaji kitatengwa kiasi cha fedha ambacho ni zaidi nadhani ya asilimia 70.

Lakini masuala ya jinsia hakuna kinachoelezwa. Nilitarajia tungesema kwamba labda asilimia 30 au asilimia 10 lakini walau tuonyeshe kwamba kuna kipaumbele fulani katika masuala ya jinsia.

Mheshimiwa Spika, ninalizungumzia hili kutokana na kwamba katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri tumesikia kuna msisitizo wa kulima mazao kama mtama katika maeneo mbalimbali ambayo yana ukame. Kuna kulima mtama na baadhi ya mazao. Tunasisitiza pia kilimo cha mhogo. Lakini tunasahau kwamba mchakataji mkubwa wa mazao haya ni mwanamke na kwa kweli mwanamke ana mzigo mzito sana wa kazi na

hili linajitokeza hata kwenye hotuba yake, linajitokeza pia katika mpango mzima wa *ASDP*. Lakini je, tunamfikiria vipi mwanamke huyu? Tunasikia kwamba kuna mashine zitapelekwa lakini ni mashine kweli au ni *sample?* Kwa sababu zipo *sample.* Utakuta kwa mfano Wilaya ya Newala ina mashine moja ya kukamulia muhogo na kutoa sumu kwenye muhogo, ni moja tu Wilaya nzima.

Lakini akina mama wengi sana wanahitaji kuchakata mhogo wao. Kwa mfano, kuna kipindi nimewahi kutembelea eneo la Wananchi wa Newala na walilalamika sana kwamba kuna magunia mengi ya mhogo yanaharibika kutokana na uchakataji duni wa zao hilo. Lakini tutakapokuwa na zana bora kama hizi za kukamilia hii sumu tunaweza tukauboresha huu mhogo na ukaweza kuuzika vizuri na hivyo kuwasaidia wananchi kuinua hali zao za maisha.

Mheshimiwa Spika, kuna suala pia la maji ambalo limeachwa kando, nadhani ingekuwa vizuri hata huu mpango wa *ASDP* kumpunguzia kazi mwanamke ukafikiria jinsi ya kuweka hata yale matanki ya *plastic* ambayo hayana gharama kubwa sana. Kwa muda tu angalau waweze kupata maji ya kupikia au ya kunywa, lakini tunaangalia kuboresha miundombinu ya barabara ambapo yule mama anapokuwa akitoka shambani anakuwa na mzigo mkubwa sana wa kazi. Wakati mwingine inachangia hata kudumaza lishe za watoto na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kidogo kuhusu suala la watalaam wa kilimo kuhusiana na upandishwaji wa vyeo na maslahi yao pamoja na kupewa vitendea kazi. Watalaam wa kilimo ni wa muhimu sana na wanatusaidia sana katika ukusanyaji wa takwimu, vile vile kuwaelimisha wananchi juu ya matokeo ya utafiti pamoja na kuwaelimisha kuhusu kanuni bora za kilimo. Lakini utashangaa kwa mfano katika Halmashauri ya Manispaa ya  wapo watalaam ambao wamekaa miaka 10 pale hawajapandishwa vyeo kabisa na zaidi ya miaka 10 hawana usafiri. Sasa tunatarajia hizi takwimu tutazipata vipi na hizi takwimu ndizo ambazo tunazitumia katika kupanga mipango yetu ya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba suala hili lifikiriwe sana kuhusiana na watalaam hawa wa kilimo kwa sababu suala hili linawakatisha tamaa sana na sijui tunaweza tukapima vipi utendaji wao kazi endapo watashindwa kuwafikia wakulima na ndiyo kama hivi tulivyosikia mzungumzaji aliyepita kwamba matokeo ya utafiti hayafiki vijijini, lakini tunaowatarajia ni hawa ndiyo ambao wanaweza wakatusaidia kwa sababu vyuo vya utafiti ni vichache na watafiti hawa ni wachache, sio rahisi kusema kwamba mtu anatoka Naliendele, anatoka sijui Maluku au anatoka Ukirigulu kwenda kufikisha matokeo haya ya utafiti kila mahali.

Mheshimiwa Spika, kuna suala moja pia la mtaalam mmoja wa kilimo ambaye yeye tangu mwaka 1998 bado yuko kwenye *TGS. B2*, hajaongezewa mshahara wake mpaka leo yupo na alimaliza *BSC*, alimaliza *MSC* lakini bado anahangaika na mshahara huu ambao unalingana na wale ambao walimaliza baada yake.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri atupatie majibu kwamba vigezo vya kupandisha mishahara katika Wizara vikoje ili angalau tuweze kufahamu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napenda kuzungumzia pia kuhusu elimu kwa Maafisa Ushirika. Kwa kweli hawa tunawatarajia sana katika kuimarisha ushirika na hasa katika kusaidia kuendeleza *SACCOS* zetu. Lakini utashangaa elimu kwa wale wana vyama vya ushirika bado ni ndogo, lakini tatizo kubwa hasa ni kutokana na elimu ndogo ambayo iko *specified* tu kwa eneo moja kwa hawa Maafisa ushirika. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Maafisa Ushirika wetu wapewe *short courses* kuhusiana na maeneo mbalimbali hasa elimu ya *SACCOS* ili kusudi wanachama wa *SACCOS* waweze kuelewa hasa vigezo vya kukopeshana waweze kutambua vigezo vya kusajiliwa na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napenda pia kugusia suala dogo la mbolea. Mbolea mpaka sasa hivi mahitaji ni makubwa lakini usambazaji bado hautoshi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naishauri Serikali kwa sababu tuna gesi katika nchi yetu, Serikali ijitahidi kuhakikisha kwamba inatumia gesi tuliyonayo katika nchi yetu ili kusudi kuweza kuzalisha mbolea nyingi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Anastazia Wambura. Sasa namwita Mheshimiwa Elisa Mollel na sina hakika kama tutasalia na muda wa kutosha baada yake kwa mchangiaji mwingine, lakini tutaona.

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie machache katika hotuba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa kwa maandalizi mazuri ya bajeti hii ya Wizara ya Kilimo ambayo licha ya kuwa na ufinyu wa bajeti, kwa kweli niseme kwamba ime-*cover* maeneo yote ambayo ni muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi zangu hizo, naomba kwa idhini yako nitoe maneno ya shukrani kupitia kwako.

Mheshimiwa Spika, tarehe 4 Julai, 2008, mimi, Mbunge wa Arumeru Elisa David Mollel na Mbunge wa Longido - Mheshimiwa Michael Lekule Laizer tumeachiwa huru na Mahakama katika kesi ambayo tulikuwa tumesingiziwa wakati ule wa uchaguzi wa Chama mwaka 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa kupitia kwako nitumie fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao walitusaidia kwa mawazo na wananchi wetu wapiga kura wa Arumeru Magharibi, Mashariki na wa Jimbo la Longido walitusaidia kwa michango mbalimbali, mawazo, fedha za kwenda kwenye kesi kama nauli na hata kutuchangia kwenye malipo ya Mawakili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulifarijika sana, tunawashukuru sana wale wote ambao nimewataja. Kipekee tunasema tumenyanyasika sana, tumeonewa sana, tumedhalilishwa sana, lakini mwisho haki imetendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba neno hili dogo la shukrani kwa kupitia kwako liwafikie wahusika wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tafakari yetu baada ya kuwa huru ni kwamba kesi hiyo tulisingiziwa ili tusiweze kushiriki katika uchaguzi wa Chama kwa nia na malengo ya kibinafsi kabisa. Naomba tena kushukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa shukrani zangu, naomba sasa nichangie kama ifuatavyo:- Kuna upungufu mkubwa sana wa chakula katika dunia nzima na nchi yetu ya Tanzania siyo tofauti. Tuna upungufu wa chakula na sasa upungufu huo umeanza kuongeza bei ya chakula ambayo hatimaye inachangia katika mfumuko wa bei. Nchi mbalimbali duniani zimeanza kuwa na mikakati mbalimbali ya kudhibiti hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, nchi za *SADC* kama tunavyofahamu zimeanza kuwekeza asilimia 10 ya bajeti zake katika Sekta hii muhimu ya kilimo. Naomba niishauri Serikali kwamba na sisi tufuate mfano wa wenzetu wa *SADC*. Sasa hivi tunawekeza asilimia nne ya bajeti yetu katika kilimo. Ni vizuri tukaongeza asilimia sita ili ifikie kiwango hicho cha wenzetu wa *SADC*.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kilimo kwa nchi yetu ni kama ifuatavyo:- Kilimo chetu kinabeba asilimia 80 ya Watanzania wote kwa maana ya ajira, kilimo chetu kinalisha zaidi ya asilimia 90 ya wananchi wetu na kilimo chetu ni chimbuko au kinaweza kuwa chimbuko la kuongeza au kuibua ajira mpya kwa vijana wetu wa Tanzania ambao wengi hawana kazi.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tukaliangalia suala la uwekezaji katika kilimo chetu. Nisingependa kupanua hili, lakini tukitazama nchi ambazo zina upungufu mkubwa wa chakula kama Sudan, Ethiopia na Somalia na hata Zimbabwe tutaona kwamba nchi hizo hazina usalama kabisa, na usalama ni mdogo sana na sisi tusipoangalia tukawa na upungufu mkubwa wa chakula katika nchi yetu tunaweza kuingia kwenye matatizo kama hayo na kama kuna njaa hakuna usalama na nchi haitawaliki. Naomba kwa umuhimu huo nisisitize kwamba tuongeze uwekezaji katika kilimo chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kidogo juu ya *green revolution*. *Green revolution* ni hatua nzuri sana ambayo Taita letu linataka kuingia ama kutekeleza. Lakini hii itahitaji mambo yafuatayo:- Tunahitaji mbolea kwa wingi, tunahitaji hiyo mbolea iwe *affordable* kwa wakulima wetu, kwa hiyo, tupunguze ushuru na tuongeze ruzuku katika mbolea na mbolea hiyo iwafikie wakulima kwa muda unaotakiwa. Aidha, tunahitaji pembejeo na madawa na zana za kisasa za kilimo.

Mheshimiwa Spika, vitu vyote hivyo vitahitaji uwekezaji katika Sekta hii ya kilimo na hiyo ni kwamba inahitaji tuongeze hiyo asilimia sita kwenda asilimia 10 na

zaidi ili tuweze kukuza kilimo chetu ambacho sasa kipo kwenye ukuaji wa asilimia nne kwenda kwenye asilimia zaidi ya nne mpaka kufikia asilimia 10 kama alivyosema Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo, ama kama tunataka kufanya hivyo ni lazima tuwe na mitaji na hiyo mitaji itatokana na kuwa na Benki ya Wakulima au chombo kingine chochote ambacho kitasaidia kutoa mikopo ya muda wa kati kwa wakulima. *Commercial loans* ambazo zinatolewa na mabenki yetu hatuwezi kumudu kuendesha kilimo na mikopo ya muda mfupi. Ni lazima tuwe na chombo ambacho kinawahudumia wakulima ili waweze kupata mikopo inayolingana na shughuli zao za kilimo na waweze kupata mikopo hiyo kwa riba ambayo inaweza ikalipika kwa shughuli za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kidogo juu ya mbolea. Pamoja na jitihada za Serikali za kutoa mbolea ya ruzuku na pembejeo kama dawa bado kuna malalamiko makubwa sana katika usambazaji na upatikanaji wa mbolea katika sehemu mbalimbali. Bei zake zipo juu kuliko hizi ambazo Serikali imepitisha na mahali pengi mbolea hiyo hufika baada ya msimu wa kupanda.

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Wizara kwamba iwe makini na isimamie vizuri zaidi na kwa karibu zaidi usambazaji wa mbolea hiyo iweze kupatikana wakati muafaka ili wakulima waitumie kwa wakati muafaka na hivyo ndivyo tutakavyoongeza uzalishaji wa chakula katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba ukulima wetu kwa asilimia kubwa unategemea mvua. Ni kilimo ambacho hakina uhakika, mabadiliko yoyote ya hali ya hewa, mabadiliko yoyote ya hali ya mvua katika nchi yetu inasababisha tuwe na uhaba wa chakula.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Wizara ikasimamia kikamilifu kabisa utumiaji wa mbegu bora na zinazostahimili ukame. Wizara isisitize utumiaji wa mbegu hizi kwa wakulima ili kuepukana na tatizo hili la mvua kuwa haba au mvua kutokunyesha kabisa.

Mheshimiwa Spika, lakini ukombozi wetu mkubwa utakuwa kwenye kilimo cha umwagiliaji. Tupanue kilimo cha umwagiliaji ambacho ni kilimo cha uhakika kabisa. Tuna maeneo mengi ambayo yana maji mengi, tuna maeneo mengi ambayo yana ardhi nzuri na yanafaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Tuwekeze katika kilimo cha umwagiliaji ili tuweze kuondokana na tatizo hili la uhaba wa chakula.

Mheshimiwa Spika, kuna upotevu mwingi sana wa mazao ya chakula wakati wa mavuno. Tukiangalia mboga mboga, matunda, nyanya, vyote hivi wakati vinakomaa vinakuwa havina soko, kwa sababu ya wingi wake na tukiangalia mazao mengine kuna upotevu mkubwa sana wa kiasi fulani cha mazao wakati wa uvunaji.

Mheshimiwa Spika, ningeshauri kwamba Wizara itazame upya njia ya kuunda na kuweka mazingira mazuri ya kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya usindikaji wa mazao

ya kilimo kwa nia ya kuongeza thamani na kuvitafutia soko vyakula hivi ambavyo vinaharika wakati wa mavuno kwa kutokuwa na soko la uhakika.

Mheshimiwa Spika, katika hili, niombe tu kusema kwamba ni muhimu kuandaa mazingira mazuri ya kuwa na umeme katika vijiji vyetu. Umeme ni nishati muhimu ambayo inachochea maendeleo na katika vijiji vyetu hata usindikaji huu ambao ninauzungumzia kama hakuna umeme, usindikaji huo wa mazao unaweza kuwa wa shida sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba niseme ninaunga mkono hoja hii ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba niongee yafuatayo. Kwanza muda uliosalia hautamtendea haki mchangiaji ambaye angefuata. Ila habari njema tu ni kwamba, kutokana na ratiba yetu kusitishwa kwa muda jana na Wizara hii kutokupata muda wake unaostahili, tumekubaliana na Serikali kwamba jioni saa 11.00 wachangiaji waendelee. Kilimo ni suala muhimu sana, hatuwezi kukatiza katikati na kupunja uchangiaji. Kwa hiyo, ninatoa fursa kwa Wabunge 11 jioni leo kuchangia.

Ataanza Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, bahati mbaya Mheshimiwa Jenista Mhagama ametakiwa Jimboni kwa hiyo hayupo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura halafu Mheshimiwa Suleiman Kumchaya. Nadhani hapo kwa makadirio na uzoefu tulionao hawa 11 wanaweza kupata nafasi. Lakini tutaweka tu kwenye orodha Mheshimiwa Castor Ligallama na Mheshimiwa Paul Kimiti, ili kama mmojawapo atakuwa na udhuru kati ya wale niliowataja, basi Mheshimiwa Ligallama na Mheshimiwa Kimiti wanaweza wakapata nafasi.

Sasa bado nawakumbusha kujaza vile vyeti vya mapambano yetu dhidi ya Ukatili kwa Wanawake maana yake kuna muda wake na kesho mchana nadhani vitakusanywa tukiwa Wabunge wote tumekwishakubali hilo, basi nadhani itakuwa ni vizuri. Baada ya kutangaza hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.53 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*(Majadiliano janaendelea)*

*Mwenyekiti (Mhe. Zubeir Ali Maulid) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala wa hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kilimo na sasa namwita Mheshimiwa Magdalena Hamisi Sakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Keenja na Mheshimiwa Godfrey Zambi ajiandae.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana kunipatia nafasi hii nami niweze kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Kilimo, Ushirika na Chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukue nafasi ya kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na Wataalam wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba hii ya kutuletea hapa Bungeni ili tuweze kujadili na kuweka mawazo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi ambazo zinafanywa na Serikali katika kuporesha kilimo hapa Tanzania, bado hatujawa na mapinduzi ya kweli ya kilimo ili tuweze kubadilisha maisha ya Watanzania ambayo asilimia kubwa sana wanategemea kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa sekta hii ya kilimo umekuwa unapanda na kushuka. Tukiangalia hata kwenye ripoti mbalimbali na pamoja na hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukuaji umekuwa unakwenda 4.5%, 4.4% hadi 4.7%. Kwa hiyo, hali halisi na ukiangalia mwaka 2007 ukuaji wa asilimia 4.7 inaonyesha ukuaji wa sekta hii unaendelea kudumaa badala ya kushamiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma hapa Tanzania suala la kilimo lilipewa uzito wa kutosha na wananchi wengi waliweza kutumia kilimo katika kuendesha maisha yao bila kuwepo na wasiwasi wowote. Wakulima waliweza kujenga nyumba bora, waliweza kupeleka watoto wao shule, waliweza kufanya mambo yao yote kwa kutegemea kilimo tu. Lakini ni kwa sababu kilimo kilipewa umuhimu wa aina yake na tukiangalia kwa sasa hivi kwamba fedha inayotengwa kwenye kilimo, pamoja na kwamba tumekuwa tunajadili hapa suala hili mara nyingi kwa njia ya maswali, kwa njia ya hotuba mbalimbali, lakini bado tunaona kila mwaka fedha inayotengwa ni kidogo. Ndiyo Mheshimiwa Waziri anatuambia kwamba kuna mpango wa kuwa na *Green Revolution.* Lakini ni kwa nini isitafsiriwe kwenye hotuba kamili tuone kwamba angalau mwaka huu fedha iliyotengwa kwenye kilimo, inatoa tafsiri kwamba kweli tuna nia na lengo la kuweza kuleta mapinduzi ya kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina wasiwasi sana kwa mwendo tunaokwenda nao, hatuwezi kubadili kilimo Tanzania hata siku moja. Bila kuweka malengo na nia ya kweli hatuwezi kufanikiwa kwa suala la kilimo ambalo asilimia 80 ya wananchi wa Tanzania wanategemea kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu walioendelea nchi za nje hawakuweza kufanikiwa kwa suala la kilimo hivi hivi waliweka juhudi na malengo ya dhati, walidhamiria kweli kweli. Mimi kwa bahati nzuri mwaka 2006, namshukuru sana Mheshimiwa Spika kwa hizi nafasi anazotupatia Waheshimiwa Wabunge kwenda nchi

mbalimbali kujifunza kwa wenzetu. Tumejua mengi ambayo tunayatolea mapendekezo, tunatoa maoni, lakini ni machache yanayotekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka juzi nilipata nafasi ya kwenda *Vietnam* na tulikwenda *purposely* kwa kuangalia suala la kilimo. Tulipofika, tulipelekwa maeneo mbalimbali, tuliweza kutembelea mashamba ya korosho, viwanda vya korosho, mashamba ya kahawa, mashamba ya mpunga na viwanda vya mpunga. Sasa kwenye majadiliano wakati wa kushirikishana mawazo, wenzetu walikuwa wanatuambia, hivi nyie Watanzania tunawashangaa sana! Mnacho kila kitu! Shida yenu, hakuna utekelezaji wa yale mnayopanga. Mnapanga vizuri sana. Walituambia kwamba hamuwezi kuamini kwamba sisi mbegu ya kwanza ya korosho tumeipata kwenu. Lakini leo wao ni *second producer* wa korosho Duniani. Wakatuambia kwamba mbegu ya kwanza ya kahawa tumeipata Tanzania. Lakini leo sisi hapa ni *standard producer* wa kahawa duniani. Nyie kwa nini hamtaki kuweka mapinduzi ya kweli kwenye kilimo?

Wakatuambia kwamba: “Tunashangaa nyie mnakuja kujifunza kwetu nini, wakati sisi mengi tumeyapata kwenu.” Kwa hiyo, unaweza kuona kwa jinsi gani ambapo hata wale ambao walipata mbegu kwetu wameweza kupiga hatua. Kwa kweli ukiangalia mpaka unaona raha. Lakini sisi tunayo sababu moja tu, ni kwamba hatujawa na nia ya kweli. Hatujaamua kuwekeza kikamilifu kwenye kilimo, ndiyo maana tumekuwa tunapiga *mark time* leo, wananchi wanaendelea kuteseka, vijana wanahama vijijini wanakimbilia mijini kwa sababu kilimo hakina tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nategemea kabisa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri atatuambia angalau mwaka huu tumeajiri wataalam wa ugani idadi fulani. Lakini hapa hakuna! Nilichoona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, anasema kwamba, Wizara imeajiri wataalam 330 halafu masuala ya wataalam wa ugani itashirikiana na TAMISEMI kuweza kusomesha wanafunzi na baadaye wawaajiri angalau wafikie 2,500 kwa mwaka, ili 2011 wawe elfu kumi na ngapi sijui mia ngapi hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona mpango huu ni wa muda mrefu, tutafika kweli! Leo tunaambiwa kwamba mwaka 2007 tu wameajiriwa wataalam wa ugani wangapi, hawa 2,500 mwakani watapatikana wapi? Mwaka 2009/2010 watapatikana wapi? Mimi nilikuwa nafikiri kwamba hatua za haraka zingeweza kuchukuliwa. Sasa hivi kuna wataalam wa ugani wengi sana, kuna vijana wengi ambao wamesomea masuala ya kilimo, wana fani za kilimo wametoka kwenye vyuo mbalimbali kama vile Tengeru, *SUA*, lakini wanafanya kazi tofauti na fani zao. Wanafanyakazi kwenye mashirika, wanafanya kazi kwa watu binafsi, wengine wamejiari peke yao.

Nilifikiri kwamba ili kuhakikisha kwamba tunachukua juhudi za haraka na mpango wa haraka Wizara ingejaribu jinsi ya kuwavutia hawa ambao wako nje na Wizara hii ambao wanafanya kwenye maeneo mbalimbali, waweke vivutio mbalimbali na ikiwezekana kupandisha mishahara ili angalau waweze kuwavutia watoke kule walipo, waweze kuja kutoa huduma kwenye hii Wizara ambayo ni muhimu sana.

Lakini kwa mpango ambao tunaambiwa na Mheshimiwa Waziri hapa sidhani mwaka 2011 tutafikia hapo Mheshimiwa Waziri anaposema. Kwa hiyo, suala la ugani ni suala ambalo linatupa tatizo sana. Wakulima wetu wamekuwa hawalimi kwa tija kwa sababu hakuna utaalam unaotolewa. Wengi wanalima kwa kilimo ambacho ni kidogo kidogo sana. Hakuna wataalam wa kutosha kuweza kuwasaidia ili waweze kulima kwa kitaalam na waweze kulima kwa tija zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ulikuwa ni ushauri wangu kwamba naomba Mheshimiwa Waziri aangalie namna yoyote, wapo wengi sana, wengine wanafanya *clearing and forwarding* wengine wako kwenye makampuni mbalimbali, wawafuatilie hata kama ni vyuoni kwamba wanafunzi hapa walimaliza mwaka gani, wako wapi wale ambao hawako kwenye kilimo, waweze kuwavuta kwa vivutio mbalimbali waweze kuja kuweza kutoa huduma hiyo muhimu sana kwenye Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ningependa Mheshimiwa Waziri atuambie kuna mahusiano gani kati ya Wizara hii ya Kilimo na Sekta ya Utalii hapa nchini. Ni jinsi gani Wizara hii muhimu, inavyosaidiana na Sekta ya Utalii kuweza kupata masoko ya mazao kwa ajili ya wakulima hapa Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tumeona kabisa kwamba hoteli nyingi za kitalii hapa nchini wanaagiza kila kitu kutoka nje. Wanaagiza nafaka kutoka nje, wanaagiza matunda kutoka nje. Wanaagiza hata mboga mboga kutoka nje. Ninapenda kuuliza kwani Tanzania hivyo vitu havipo? Vile ambavyo vinalimwa na wakulima wetu haviwezi vikasambazwa kwenye hayo mahoteli. Ukienda hata *Super Market* sasa hivi utakuta vitu vingi vinatoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependa kusema Wizara imefanya juhudi gani kuhakikisha ndani ya *Super Market* zetu hapa Tanzania kunakuwepo vitu vilivyosindikwa vizuri vitu ambavyo ni vya wakulima wa Tanzania. Kwa sababu tatizo linalotukumba pia wakulima wa Tanzania ni suala la masoko. Lakini masoko ya hapa hapa nchini yamejazwa na vitu vya nje, ni juhudi gani Wizara inafanya kuhakikisha kwamba *Super Market* zetu, hoteli zetu, maeneo yote ambayo watalii watafikia wakapata huduma mbalimbali yanakuwa na vyakula vyetu nafaka zetu, matunda yetu na mboga mboga ili tuhakikishe kwamba wakulima wetu wanapiga hatua kwa kile kilimo wanachokifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala kubwa kama nilivyozungumza, ni suala la masoko. Limekuwa ni tatizo. Pia kukosekana kwa viwanda vya kusindika matunda, vya kusindika mboga mboga ni suala ambalo ni tatizo. Mimi suala la Serikali kuachia suala la viwanda vya ku-*process* vyakula, pamoja na suala la matekta kwenye sekta binafsi au kwa kutegemea wawekezaji. Mimi naona hapa hawajasaidia wakulima, kwa sababu anapokuja mwekezaji huwezi kuwekeza mahali ambapo hajapachagua yeye mwenyewe. Mwekezaji anataka awekeze mahali ambapo ni *first gaining*, yaani anapata hela ya haraka haraka. Ni vigumu kwenda kuanza kuwekesha kwenye kiwanda ambacho mpaka afanye tathmini aone kwamba kweli hapa nitanufaika. Maeneo kama haya muhimu

nilikuwa nategemea Serikali yenyewe ndiyo ingewekeza. Ihakikishe kwamba inakuwa na viwanda vya ku-*process* vyakula ili wakulima waweze kupata masoko mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha sana kwamba kipindi cha msimu, labda msimu wa matunda. Kwa mfano, sasa hivi hata ukienda hapa Dodoma sokoni, machungwa yanaoza kabisa. Sasa hapo ni sokoni tu, hujaenda mashambani. Mashambani ndiyo kabisa hivi yameoza huko chini ya miti yametapakaa kabisa. Lakini baada ya msimu tu kwisha, hakuna chungwa litakaloonekana. Chungwa ni mpaka Sh. 200/=, Sh. 300/= utanunua. Lakini cha ajabu, sisi Watanzania tukienda madukani kwenye *Super Market* tunanunua *juice* kutoka Zimbabwe, Kenya na *South Africa*, tena kwa gharama kubwa sana. Ni kwa nini Wizara isichukue jukumu la kuhakikisha kwamba haya matunda yanayooza kila kipindi cha msimu yanatengenezwa *juice* ziweze kuwekwa madukani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo tunasema tu mapinduzi ya kilimo, kama hatujaweza kujipanga vizuri hata, kama tutawashawishi wakulima wakalima, lakini tukawakosesha masoko, tukaacha kuwatafutia masoko mazuri, pia tunakuwa hatujawakomboa katika kilimo chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri wakati ana-*wind-up* atuambie kwamba haya matunda yanayoharibika kila siku ni mpango gani mkakati uliyowekwa kuhakikisha kwamba wakulima wetu wanaweza kutengeneza *juice*, wanaweza kusindika vyakula vikaweza kuuzwa kwa bei nzuri kama hizo ambazo tunanunua kutoka huko nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la wakulima wa Mkoa wa Tabora. Mkoa wa Tabora ni Mkoa ambao tunategemea sana kilimo cha tumbaku na ndiyo zao la biashara na zao hili limekuwa linaliingizia Taifa hili pesa nyingi sana. Tukiangalia kila hotuba inayokuja hapa kila mwaka ni lazima sigara inapandishwa ushuru. Wanapandisha ushuru kwa sababu inaliingizia Taifa pesa nzuri. Sasa kama Taifa linapata fedha nzuri kutokana na tumbaku, ni kwa nini mkulima asiangaliwe? Leo mkulima wa Tabora ambaye analima tumbaku hanufaiki na lolote na tumbaku anayolima, wanaonufaika ni makampuni wanaonunua hii tumbaku.

Mheshimniwa Mwenyekiti, tumbaku ya Tabora imekuwa inapangwa bei na wenye makampuni. Kwanza, mwenye kampuni analeta mbolea kwa bei ambayo ni ghali sana. Wakulima wanalazimishwa kukopa mbolea kwa bei kubwa, tena inaendana na kupanda kwa dola. Dola ikipanda leo, kesho atamwambia bei ya mbolea imepanda. Ikipanda kesho ataambiwa bei imebadilika. Lakini tukija kwenye suala la ununuzi sasa bei ipo pale pale na hata angefanya nini hawabadilishi bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa Tabora wamekuwa wanalalamika sana kuhusiana na makampuni ambayo yameweka kama yamenunua hati miliki ya maeneo yale kwa ajili ya kununua haya mazao. Lakini Serikali imekuwa haiwasikilizi. Tumbaku wananunua wanavyotaka, kwanza wanagredi katika madaraja manne. Ukiangalia bei ya hilo daraja la kwanza, utashangaa! Usije sasa kwenye hayo madaraja madogo, ndiyo kabisa mkulima hanufaiki lolote!

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, unakuta kwamba lile gunia ambalo mkulima anauzia tumbaku, ananunua na mwakani atanunua tena lile lile. Halafu kwenye lile gunia moja ambalo anauza linapunguzwa kilo moja, wanasema eti ni hii ni uzito wa gunia. Kwa hiyo, gunia kama lina kilo 100 anaambiwa kilo zako ni 99 kilo moja ni ya gunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini Serikali inaruhusu makampuni haya kuendelea kunyanyasa wananchi, kuendelea kuwalalia, ili waendelee kuwa maskini na wao waendelee kunufaika? Suala lingine ni kwamba makampuni haya yamekuwa wakati mwingine yanachuikua tumbaku kwa mfano *Dimon* ya Morogoro, inachukua tumbaku kutoka Tabora, inafikisha kiwandani, wanarudisha mpaka Tabora wanasema kwamba tumbaku hii ilikuwa haina ubora, au tumbaku hii haijafika kile kiwango kinachotakiwa. Ilichukuliwa kwa makosa. Huu kwa kweli ni uonevu. Haiwezekani mfanyabiashara achukue bidhaa shambani halafu afikishe kiwandani arudishe. Inaonekana kwa jinsi gani kwa makampuni haya ambayo hayana mtu ambaye anawasimamia, yameamua kutumia wananchi kwa ajili ya kujinufaisha.

Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, kwa moyo ule ule ambao alitumia kule Mtwara kusaidia wananchi wa Mtwara kuweza kukomboka kwa zao la korosho, sasa hivi wameweza kunufaika nalo kwa juhudi hizo hizo naomba Mheshimiwa Waziri naomba uhamie Tabora ukawasaidie wakulima wa Tabora waweze kunufaika na zao la tumbaku. Vinginevyo wakulima wa Tabora wameshachoka kulima zao la tumbaku kwa sababu hawanufaiki nalo bali wanaendelea kuwa maskini na huku makampuni yakiendelea kushamiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la wakulima wa mpunga wa mashamba ya Mbarali Mkoa wa Mbeya. Mwaka juzi hapa tulilijadili sana hili suala hapa Bungeni. Wabunge walichangia kwamba jamani mashamba haya vijana wengi sana wamejiajiri wenyewe kule na wanayatumia kwa ajili ya kujinufaisha wenyewe na ndiyo njia ya kuwakomboa vijana katika masuala ya maisha. Lakini Serikali ilisema kwamba haya mashamba tunayakodisha kwa mwekezaji ndiye atakayeleta maendeleo kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichofanyika ni tofauti na tulivyokuwa tunategemea. Kilichofanyika ni kwamba wakati mashamba haya hayajakodishwa kwa mwekezaji, wakulima walikuwa wanayakodisha kutoka kwa *PSRC* kwa Sh. 375,000/= kwa *plot* moja. Alivyoingia mwekezaji tu hakubadilisha chochote, lakini yale mashamba waliweza kukodishiwa wakulima wale wale kwa shilingi milioni moja.

Kwa hiyo, tulichofanya hapa tumemnufaisha yule mwekezaji, hatukumnufaisha mwananchi. Sasa yule mwekezaji kuanzia amekodisha yale mashamba mwaka 2006 mpaka leo hajafanya lolote. Ameweza kulima hekta 100 tu mwaka jana. Na hizo heka 100 aliweza kuvuna ni heka 30 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, anachokifanya ili kuweza ku-*justify* kwamba anaweza kuzalisha ananunua mpunga kutoka kwenye vijiji vilivyo jirani anaweka kwenye *yard* yake na ananunua mpunga kwa Sh. 5,000 debe moja, tena hapimi kwa kilo, ananunua kwa Sh. 5,000/= kwa debe moja, ndoo ya lita 20 na anaishindilia. Huu ni wizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Waziri asaidie wakulima wa Mbarali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Magdalena.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ahsante sana Mheshimiwa Magdalena Hamisi Sakaya. Sasa namwita Mheshimiwa Charles Keenja, atafuatiwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi na Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula ajiandae.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie mada hii muhimu na nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Wasira, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa hotuba nzuri sana aliyotoa hapa Bungeni ambayo imefafanua kwa undani ni mambo gani tunatakiwa tufanye ili kilimo chetu kiweze kutimiza malengo yake. Jambo moja tu lenye matatizo ni kwamba yaliyopo ni mambo mengi, mambo muhimu lakini rasilimali tunazotenga hazilingani na mahitaji ya sekta hii. Nina hakika hata hivyo kwamba kutokana na ujuzi wake na uzoefu, nafikiri yuko katika Wizara hii kwa mara ya tatu, hakuna mtu ambaye ana uzoefu na Wizara hii kama Mheshimiwa Wasira na ataweza kutuvusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo bado ni sekta kiongozi katika nchi hii. Tumebadilisha utaratibu wetu wa takwimu ili kubadilisha mwaka wa msingi wa takwimu hizo, kwa hiyo, mchango wake ukashuka mpaka asilimia 26.5. Lakini kilimo kazi yake wala siyo kuchangia tu uchumi wa nchi hii. Kina mambo mengi sana kinayofanya katika nchi hii. Kwanza ni kinachangia uchumi ambao hakuna sekta nyingine ambayo inakifikia. Lakini vile vile chakula tunachokula humu nchini asilimia 95 mpaka 97 kinatokana na uzalishaji wa humu humu ndani. Nafikiri kazi ya kwanza ambayo tungeifanya huku Bungeni ni kuwapongeza sana na kuwashukuru sana wakulima wetu kwa kazi hii nzuri ambayo wanafanya. *(Maokofi)*

Kuna nchi Afrika huku, kwa mfano Botswana, ambao wanajitegemea kwa chakula kwa asilimia tatu tu. Sasa Tanzania tungekuwa tunajitegemea kwa asilimia 50 tungekuwa katika *crisis.* Lakini kwa kuwa tunajitegemea kwa kiwango kikubwa sana, hali yetu ni nzuri. Naomba hii sekta ya kilimo tuendelee kuitukuza na kuienzi kwa sababu kwa kweli ndiyo sekta muhimu sana katika maisha yetu. Naomba niseme kwa unyenyekevu kabisa, madini yanaweza yakatusaidia katika muda mfupi, lakini yakishachimbwa kutoka huko ardhini yakatoka, basi hakuna tena madini. *(Makofi)*

Kilimo tutaendelea kukitegemea baada ya hayo madini kwisha. Tunachoiomba Serikali ni kwamba ihakikishe kwamba mapato tunayopata kutokana na madini, haya madini ya dhahabu, sijui na rubi na nini, kuna mengine hata siyajui, pamoja na gesi,

tuyawekeze katika kilimo ili kilimo kikue. Tutakapoishiwa haya madini tuwe na kilimo endelevu ambacho kitaendelea kutusaidia kuimarisha uchumi na kutupatia mahitaji yetu ya Taifa. Lakini kilimo ndiyo sekta moja muhimu sana, ndiyo sekta ambayo tunaitegemea na tutaendelea kuitegemea kwa muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati najiandaa kuchangia katika mada hii imebidi nirudi nisome Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ambayo naona na Wapinzani wanaisoma kwa makini kwa malengo tofauti. Nafikiri lengo ni kutukosoa. Lakini sisi tunaisoma kwa lengo la kujikumbusha mambo ambayo tumejipangia kufanya katika miaka mitano ya uongozi wa CCM wa Taifa hili.

Mheshimiwa Makamba ambaye ni mzoefu wa siku nyingi amefanya kazi katika ngazi zote za nchi hii. Alitukumbusha kwamba miaka 36 iliyopita, tulipitisha Azimio la Iringa linalojulikana kama Siasa ni Kilimo. Yanayosemwa katika azimio lile na yanayosemwa katika Ilani na yanayochangiwa kwenye Bunge hili ni yale yale. Miaka 36 tunajua ugonjwa, tunajua tiba, lakini mikono imekufa ganzi, tunaendelea pale pale tulipokuwa. *(Makofi)*

Mengine tumesema wenyewe, maana haya yaliyoko kwenye Ilani tumeyaandika sisi wenyewe. Haya tunayoeleza katika Siasa ni Kilimo tunaandika sisi wenyewe. Katika hayo tunatoa maagizo mengine *very specific* ambayo yakitekelezwa kilimo chetu kitabadilika. Lakini kwa miaka 36 hatutekelezi haya. Mimi nimesoma kwa makini sana hii hotuba ya Waziri na makaratasi yake mengine mengi ambayo yameandikwa na Wizara juu ya suala hili la kilimo.

Tulikwenda Maputo, tukakubaliana kwamba kilimo kitatengewa asilimia 10 ya bajeti ya Serikali. Ilani nayo ikatambua mchanguo huo kwamba tutatenga asilimia 10 ya uwekezaji wa Serikali na kukipa kilimo. Lakini mwaka jana ilikuwa asilimia 6.2. Mwaka huu ni asilimia 6.4 lakini sina hakika sana kama ni asilimia 6.4 mwaka huu kwa sababu kiasi cha pesa tulichopata mwaka huu ni kidogo kuliko tulichopata mwaka jana. Hata kule tulikokubaliana kwenda kwenye asilimia 10 hatuendi. Sasa hiki kilimo kitakuwa namna gani? Maana hiki kilimo kinataka uwekezaji wa uhakika ndipo kiweze kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwa masikitiko sana kwamba badala ya kilimo kwenda mbele tumekuwa tukirudi nyuma. Tulipata kuwa na kiwanda cha mbolea Tanga, kilikuwa na uwezo wa kunazalisha tani 125,000 za mbolea kwa mwaka. Kile kiwanda kimefungwa tangu mwaka 1994. Kwa hiyo, mbolea tunayotumia sasa hivi ukiacha hiki kidogo inayotoka Minjingu. Mbolea yote tunaagiza kutoka nje. Tunapendekeza kwa Serikali kwamba Serikali ichukue hatua madhubuti kabisa za kuhakikisha kwamba tunafufua viwanda vya mbolea humu nchini. *(Makofi)*

Tujenge viwanda vya kutengeneza *phosphate,* tunacho kimoja Minjingu naambiwa kuna *phosphate* Mbeya, kuna *phosphate* Mpanda, tujenge viwanda tujitosheleze kwa mbolea. Duniani kuna upungufu wa mbolea. Sijui kama watu wanajua hilo, kwamba tukienda kwenye soko kununua mbolea, Mchina akifika sisi hatuoni ndani.

Au akafika Mmarekani ambaye ananunua mamilioni ya tani sisi hatuwezi kupata mbolea. Kuna upungufu wa mbolea katika soko. Mwenyezi Mungu katujalia tuna *deposits* za *phosphate*, tuna gesi ambayo inaweza ikatengeneza *nitrogen fertilizers.* Sasa kwa nini tusitengeneze mbolea? Mimi kuna jambo linalonitisha sana na naliogopa kweli kweli! Ni pale Serikali inaposema imejitoa katika mambo kama haya. Inabaki katika mambo gani sasa? Maana mambo tunayoyataka Tanzania ndiyo haya. *(Makofi)*

Tunataka Serikali iwezeshe kujengwa kwa viwanda vya mbolea. Serikali iwezeshe kujengwa kwa viwanda vya zana za kilimo ikiwa ni pamoja na matrekta. Tulikuwa na kiwanda cha *UFI* pale Ubungo, kilikuwa kinatengeneza zana za kilimo. Tulikuwa na ZZK Mbeya, kilikuwa kinatengeneza zana za kilimo. Kile kiwanda cha Dar es Salaam kinatengeneza mabomba ya maji. Ninashukuru kwamba tunatengeneza mabomba humu nchini, lakini hamna zana za kilimo zinazotengenezwa sasa hivi cha Mbeya kimefungwa, hakifanyi kazi kabisa. Sasa huyu mbinafsishaji anayenunua kiwanda halafu akakifunga na sisi tutakaa kimya, yeye ana kasoro na sisi hatuna unafuu. *(Makofi)*

Tunataka tuzitengeneze hizi zana za kilimo humu nchini. Sasa hivi hata jembe la mkono halipatikani humu nchini, tunaagiza kutoka Uchina na tunatumia humu nchini majembe milioni nne kila mwaka. Unaweza kufikiria ni kiasi gani cha fedha za kigeni tunazotumia kuagiza zana za kilimo ambazo tulishajenga uwezo wa kuzitengeneza humu humu ndani. Tumerudi nyuma sana. Tulikuwa na viwanda vya kusindika, Mheshimiwa Sakaya anazungumza hapa kwa uchungu na kwa ukali kabisa juu ya viwanda vya kusindika matunda. Tulikuwa na *TANGOLD* kilikuwa kinatengeneza maji mazuri sana ya makopo kutokana na matunda.

Vile viwanda akakodishiwa mfanyabiashara mmoja, cha Korogwe akaacha kimebomolewa, hakuna kilichobaki, cha Dar es Salaam anakoroga haya maji, maji yanayokorogwa yenye rangi na sukari na harufu fulani na kuuza. Mkataba ulikuwa umeandaliwa vibaya sana. Namwomba Waziri aende akataze ule mkataba, mimi ulinishinda. Aende akatazame ule mkataba tutafute njia ya ku-*wriggle out* ule mkataba. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule mkataba unasema kwamba mkodishaji ataanza kulipa pango baada ya kuanza kuzalisha maji ya matunda. Sasa hazalishi maji ya matunda anatengeneza hii mikorogo ambayo kwa kuwa sio maji ya matunda basi halipi miaka zaidi ya kumi na mingapi sasa hivi. Hivi sheria kweli inaweza ikaruhusu Serikali ikaonewa kiasi hiki! *(Makofi)*

Lakini tulipata kuwa na viwanda vya kutengeneza maji ya matunda...

**MWENYEKITI:** Samahani husikiki, *okay!* Rudisha chombo.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika hizo chache zilizopotea.

**MWENYEKITI:** Tumezingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda cha korogwe sasa hivi wala hakiwezi kuponyeshWa tena, kile kimekuwa *vanderlized* mabati yamechukuliwa na matofali na nini. Tulichonacho pale pengine ni *site.* Lakini tulipata kupiga hatua kiasi hicho.

Tulipata kuwa na mashamba makubwa katika nchi hii Shirika lililoitwa *NAFCO* pamoja na mashamba makubwa ya *BASUTO* ekari 70,000/= tulikuwa tunalima ngano, tunajitosheleza kwa ngano. Sasa hivi karibu ngano yote tunayokula katika nchi hii inabidi tuagize kutoka nje kwa sababu yale mashamba hayazalishi.

Kuna viwanda vya kusagisha viko vingine Iringa, kuna viwanda vya kukoboa mpunga, viko *all over the country.* Tulishapiga hatua, lakini yote haya yamekwama. Sasa ombi langu kwa Serikali ni kwamba hebu turudi tukafufue haya mambo yaliyokwama. Pale tunapofikiri kwamba sekta binafsi inaweza ikatusaidia, basi tufanye mambo mawili. Kwanza, tuiandae hiyo sekta binafsi na pili tuiwezeshe. Tunapozungumzia sekta binafsi lazima tuwe waangalifu sana maana tunazungumzia sekta binafsi halafu wanakuja watu wa nje ndiyo wanakuwa sekta binafsi. Watanzania tutafika siku tukakuta tumegawa kila kitu kwa sekta binafsi kutoka nje na sisi tukabakia kuwa vibarua. *(Makofi)*

Lakini tukiwezeshwa nina hakika tunaweza kabisa tukajenga viwanda hivi tukaagiza hayo matrekta yanayohitajika, tukayaleta humu ndani yakaja yakalima na uchumi wetu ukaendelea na sisi tukaendelea nao. Katika kurudi nyuma mwaka 1970 tulikuwa na matrekta 18,000 yaliyokuwa yanalima. Mwaka jana tulikuwa na matrekta 7,000.

Kwa hiyo matrekta tuliyonayo nchini sasa ni theluthi moja ya matrekta tuliyokuwa nayo miaka 30 iliyopita. Tumerudi nyuma na matrekta yanayoingia nchini sasa hivi ni matrekta 200, 300, 400 tu kwa mwaka. Hayatoshi kujaza hili pengo tufike mahali tuweze kufanya kilimo ambacho ni *mechanized* kwa maana ya kutumia matrekta. Waziri anasema, tunahitaji matrekta sio chini ya 1,000 kila mwaka. Lakini yanayoingia hayazidi 400 kila mwaka. Tunaambiwa na Waziri wa Fedha kwamba yataingizwa matrekta 1,000 kila mwaka, lakini kwa kutumia sekta binafsi.

Hii sekta binafsi inayoagiza matrekta 1,000 mimi sijapata kuiona. Kama tunataka sekta binafsi iagize matrekta 1,000 ni lazima tuiwezeshe, lazima tuiandae kwa makusudi. Kwamba kuna kazi hapa, chukua fedha hizi nenda ukaagizie, uza matrekta yako rejesha hizi fedha za Serikali. Tukifanya hivyo tutakwenda. Lakini kama tunasema tu kwamba iko sekta binafsi itakayozinduka siku ikatuagizia matrekta, tutangoja mpaka mwisho wa dunia hii hakuna matrekta yatakayoingia nchini. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iangalie suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo, kujenga viwanda, tunasema viwanda vitajengwa na sekta binafsi, ipi? Imekuwa wapi siku zote hizi? Kama unaitaka lazima uiandae uiwezeshe ndipo ijengwe, vinginevyo tungojee tupate watu wanaotoka nje wanaoitwa wafadhili ama wahisani waje wakatufanyie kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna uwezo mkubwa sana wa kufufua kilimo, lakini moja ya mambo ambayo ni lazima tufanye ni kuwapa wakulima wetu mafunzo. Wizara hii ilikuwa na vyuo vya wakulima 21. Sasa hivi wana vinne na kuna Vyuo vya Maendeleo ya Jamii sasa ambavyo vimeunganishwa na hivi vilivyokuwa vya kilimo 56, ukiongeza na vinne tuna vyuo 60 na mimi namwomba Mheshimiwa Waziri azungumze na Waziri mwenzake wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto sasa ili vyuo hivi vitumike kutoa mafunzo kwa wakulima na vipangiwe ratiba ya mwaka mzima. Hii ya kusema tunangojea *extension officer* aende akamfundishe mtu kilimo akielewe vizuri itatuchukua miaka mingi sana.

Marehemu Sokoine, alikuwa ameliona hili miaka mingi iliyopita akauliza, hivi haiwezekani kuwafundisha wakulima kilimo *directly* wakajua kilimo kwa kutoka darasani? Jibu ni ndiyo, tuna vyuo vya maendeleo ya jamii 56 na vyuo vya kilimo vinne, tukivitumia vyote vyuo hivi tunaweza kabisa tukafundisha idadi kubwa sana ya wakulima kila mwaka na wao wakaenda vijijini wakafundisha wenzao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Wizara ishirikiane na hii Wizara ya Maendeleo ya Jamii, kuhakikisha kwamba hivi vyuo vinapangiwa ratiba ya kufundisha kilimo mwaka mzima *non stop,* ili tuondoe hii kutokuwa na ujuzi, halafu tuagize sasa matrekta, tutumie plau, mashamba yawe makubwa tuondokane na hivi vishamba vidogo vinavyolimwa bila utaalamu. Tuwe na mashamba makubwa yanayolimwa na wakulima waliosoma. Katika nchi zote za nje wakulima ni watu waliokwenda shule wakapata digrii ndio wanakwenda kwenye kilimo. Kama wewe mwenyewe mwenye shamba hukusoma kilimo unaajiri Meneja aliyesoma kilimo, sasa kwetu hivi Keenja, amekulia kijijini pale basi ni mkulima. Ukulima sio jambo la kurithi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya kilimo. Lakini na mimi niseme naunga mkono bajeti hii, lakini nina mambo machache ambayo ningependa niyazungumze. Lakini bahati nzuri sikujua kama ningeweza kupata nafasi ya kuchangia kwa kuongea. Niliandika na ninadhani mengi ambayo nitayazungumza tayari nilishayaandika. Lakini nikizungumza, nadhani yatakuwa na msisitizo ambao unastahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Mbozi. Mbozi ni moja ya maeneo ambayo tunalima sana mazao ya biashara na mazao ya chakula. Kwa maana hiyo, siwezi kuacha kuzungumza suala la mbolea hata kidogo pale ninapopata nafasi ya kuzungumza. Waheshimiwa Wabunge, walionitangulia wamezungumza kwa uchungu sana suala la mbolea, nami napenda niungane na wenzangu kwamba bado Serikali haijaonyesha *seriousness* ya kutosha katika suala zima la mbolea pamoja na pembejeo za kilimo, hakuna *seriousness* ya kutosha.

Nami nasema hivi, kama ingekuwa tumefika mbali sana, kwa sababu tumekuwa na maazimio mengi sana yanayozungumza suala la kilimo. Kuanzia Azimio la Iringa ambalo limesemwa sana hapa, mpaka leo. Mambo ambayo tuliyazungumza kwenye Azimio la Iringa kwamba tuyatekeleze mpaka leo hayajatekelezwa, kwenye azimio la iringa tunasema kwamba tutahakikisha kwamba mbolea inawafikia wananchi pamoja na pembejeo na zana za kilimo kwa wakati. Mpaka leo tunazungumza hilo hilo kwamba pembejeo za kilimo hazitoshi, haziwafikii wananchi kwa wakati wake, miaka 35 zaidi iliyopita tunazungumza lugha hiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa hapaonyeshi *seriousness* ya Serikali hata kidogo. Nadhani kungekuwa na *seriousness* tungeweza kwenda mbali kwa sababu kama kwenye elimu tumeweza kwa nini kwenye kilimo tunashindwa? Kwenye elimu tulisema ikiwezekana tunataka tupeleke watoto zaidi ya asilimia 60 kwenda sekondari mpaka mwaka 2010, lakini mwaka 2010 haujafika tumeshapeleka zaidi ya asilimia 90 ya watoto sekondari, tumeweza. Maana yake tumeonyesha *seriousness.* Kwa hiyo, kwenye kilimo tungeonyesha *seriousness* ya namna hiyo, nina hakika tungefika. Hakuna *seriousness* hapa!

Naomba niseme jambo moja ambalo kidogo limenishangaza kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 33. Naomba ninukuu. Maneno hayo kidogo yamenishangaza! Ni ibara ile ya 54, lakini nitaanzia pale katikati, anasema: *"Mbolea yenye ruzuku kutofika Wilayani kwa wakati kutokana na uwezo mdogo wa kifedha wa mawakala."* Kwa hiyo, tulishajua kwamba hilo nalo ni tatizo la mawakala ambao hawana uwezo, bado tunaendelea kuwapa kutupelekea mbolea kwa wananchi na hawaifikishi kwa wakati. Lakini nasema vituo vikuu vya kununulia mbolea Mikoani kuwa mbali na wakulima; kama tunalijua hili, kwa nini tuweke vituo mbali zaidi na wakulima na leo tunalichukua kama sababu ya kuchelewesha mbolea kwa wakulima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunasema, *"Kuwepo kwa bei mbili za mbolea yaani bei ya soko na bei ya ruzuku."* Nami sasa hapa nitaomba Mheshimiwa atufafanulie kama hiyo mifumo miwili inaondoka kwa sababu zilikuwa ni changamoto kwa ajili ya mwaka jana, msimu uliokwisha. Kulikuwa na mifumo miwili ya mbolea, ilikuwa tatizo. Sasa Mheshimiwa Waziri, atuambie, mifumo hiyo haipo?

Lakini jambo lingine ambalo pengine limenishangaza zaidi, ni pale Mheshimiwa Waziri anaposema: *"Kutokuwepo kwa takwimu sahihi za mahitaji halisi ya pembejeo..."* Kwa kweli mimi hapa nimesikitika sana, Wizara ya Kilimo haijui? Haina takwimu sahihi za pembejeo zinazohitajika na wakulima wa nchi hii? Hili ni lazima liwe la kusikitisha sana. Nami ninaomba kwa sababu Mheshimiwa Waziri, ameandika, hebu atufafanulie, hili linakuja namna gani? Hatujui takwimu? Kama hatujui, maana yake hatujui tunakokwenda. Basi kama ndio hivyo, kama hatuwezi kujua takwimu sahihi za watu ambao wanahitaji pembejeo katika nchi hii ni hatari sana. Nadhani hilo Mheshimiwa Waziri, atueleze vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Mheshimiwa Waziri na hili nimu-*address* yeye mwenyewe, alikuja Mbeya mwaka jana tarehe 03 Oktoba, 2007, wakati huo

aliongozana na Mheshimiwa Aggrey Mwanri, wakati alipokuwa Katibu wa Mwenezi. Tulifanya mkutano pale kwenye viwanja vya Ilomba katika Jiji la Mbeya, Mheshimiwa Waziri kwa kinywa chake, (Mheshimiwa Wasira), wakati huo alikuwa Waziri wa Kilimo na ninashukuru amerudi tena, alisema tutahakikisha mbolea kwenye msimu huu wa 2008/2009 inapatikana vijijini kama soda ya *Coca Cola* inavyopatikana. Wananchi wa Mbeya walikusikia Mheshimiwa Wasira. Tunataka sasa uwaeleze mbolea hiyo itapatikana kama soda ya *Coca Cola* au *Fanta* inavyopatikana kule vijijini. Maana hiyo ilikuwa ni kauli ya Serikali. Anaposema Waziri, maana yake ni Serikali inazungumza. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa hebu tueleze kwamba mbolea hiyo itapatikana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza. Mwaka jana tulisema lengo la mbolea la Taifa ni tani 385, lakini leo mbolea ambayo tuna hakika nayo ni tani 130 za Minjingu, hatujui mbolea nyingine inayokuja kutoka nje kama imekuja. Mimi nina wasiwasi kama tutafikia lengo na hili ndio jambo ambalo ninaendelea kuzungumza kwamba inawezekana kabisa kwamba hatuna *seriousness* na suala la kilimo katika nchi hii na kwa maana hiyo tutaendelea tu kama vile tunatwanga maji kwenye kinu kwa sababu tunayozungumza kimsingi hatuoni *serious implementation* ya mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ambalo ningependa nilizungumze ni suala zima la bei za mbolea. Bei ya mbolea leo na kama alivyoonyesha Mheshimiwa Waziri mwenyewe kwenye kitabu cha bajeti ukurasa wa 95, bei za mbolea zinatisha. Hii ni kwa bei za Dar es Salaam, sina sababu ya kusoma kwa sababu Waheshimiwa Wabunge, wote mna vitabu, ukurasa wa 95. Sidhani ni mkulima gani anaweza aka-*afford* bei zile zilizotajwa pale, ni mkulima gani masikini wa Tanzania? Mimi nimetoka Mbozi leo, bei ya mfuko mmoja wa mbolea ya *DAP*, inauzwa Sh.105,000/=, mkulima gani atanunua mbolea hiyo na tunategemea tuafanye mapinduzi kwenye kilimo? Labda kutokee miujiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka Mheshimiwa Waziri, atueleze Watanzania watalima? Nami waliniuliza: Mheshimiwa Mbunge, tutalima kwa bei hizi? Kwa hiyo, naomba Watanzania wasikilize bei za mbolea kwa kipindi hiki Mheshimiwa Waziri, zitakuwa namna gani? Je, ile mifumo miwili ya mbolea, ile mbolea ya bei ya soko na mbolea ya ruzuku zinaondoka kwa maana hiyo kuondoa mwanya wa rushwa kwa wale wenzetu wanaopenda kujinufaisha wao wenyewe?

Ningependa Mheshimiwa atupe majibu katika eneo hilo ambalo wananchi wa Tanzania, wakulima wa kule Mbozi, Mbeya na maeneo mengine wanakolima na kutegemea kilimo sana watayasikia na wawe na uhakika kabisa kwamba mwaka huu wataweza kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie suala la kahawa. Jana Mheshimwa Mramba, alizungumzia vizuri sana suala la kahawa. Zao la kahawa ni la kwanza katika kuiingizia nchi hii fedha za kigeni na Wilaya ya Mbozi ninakotoka mimi, tunazalisha zaidi ya asilimia 28 inayolimwa katika nchi hii. Pamoja na kwamba kuna Wilaya nyingine, kwa mfano Ileje Mbeya na Rungwe, zinazolima kahawa katika Mkoa wa Mbeya, lakini Wilaya ya Mbozi peke yake inazalisha karibu tani 12,000 katika nchi

hii. Wote tumeona tani za kahawa ambazo zinazalishwa, karibu wastani wa tani 41,000 lakini tani 12,000 zinazalishwa kutoka Mbozi. Lakini kuna matatizo makubwa ya zao la khawa, sasa kumekuwa na kupungua pia kwa uzalishaji wa zao la kahawa.

Mheshimiwa Waziri, alipozungumza alisema kwamba na ninaomba ni-*quote* hapa, kwanini kumekuwa na upungufu kwenye zao kahawa, anasema: *"Upungufu huo umetokana na tabia ya zao la kahawa kupunguza tija katika msimu unaofuatia misimu ambayo uzalishaji ulikuwa mkubwa."* Sidhani kama sababu hizi ni za kweli sana, inawezekana wataalamu wake wamemweleza huyu Mheshimiwa Waziri, lakini mimi sidhani kama ni za msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ambazo ninazijua na kwa vyovyote vile wakulima wanazijua, kwanza ni kutokuwa na soko la uhakika la zao la kahawa na kuyumba kwa bei za soko la kahawa. Watu wengi walianza kukata tamaa kwenye uzalishaji wa zao la kahawa, walianza kukata tamaa. Lakini pili ni bei yenyewe ya mbolea ambayo Mheshimiwa Waziri, haitaji humu. Bei ya mbolea ambayo tunatumia zaidi katika uzalishaji wa kahawa *CAN*, kwanza haikuwa kwenye ruzuku, lakini pili bei yake kama ilikuwa inauzwa kati ya Sh. 60,000/= mpaka Sh. 70,000/= wakulima wangapi wataweza? Kwa hiyo, unapozungumza kuzalisha kahawa zaidi na bei za mbolea ama pembejeo zikawa juu zaidi maana yake tunaji-*contradict* wenyewe, hatuwapi wananchi *support* inayotosha ili waweze kuzalisha vizuri zaidi.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, atuhakikishie, awaeleze Watanzania na wakulima wa kahawa maeneo yote katika nchi hii kwamba wanafanya nini ili kweli tuweze kuinua kiwango cha zao la kahawa. Lakini pia Maafisa Ugani wa zao la kahawa hawatoshi, kule Mbozi, tuna vijiji zaidi ya 100 vinavyolima kahawa, lakini Maafisa ugani tulionao hawazidi 50, tunategemea nini? Maafisa ugani 50, tunategemea miujiza gani katika zao hili? Vyovyote vile tusitegemee miujiza hata kidogo! Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, aongeze pia *speed* ya kupeleka Maafisa Ugani katika Wilaya yetu ya Mbozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kahawa iweze kuzalishwa vizuri na wataalamu wanavyosema, ule mti mmoja wa mbuni una uwezo wa kuzalisha kilo tano za kahawa. Lakini kwa sababu ya matunzo hafifu kwenye zao la kahawa, leo sisi mti mmoja unazalisha gramu 250, tunategemea nini? Mti mmoja utuzalishie kilo tano za kahawa, lakini kwa sababu ya matunzo duni na ambayo sio makosa ya wakulima, mti mmoja unaweza ukatuzalishia gramu 250. Wenzetu Mbinga, kwa maelezo wanavyosema, wataalam wamekwenda angalau kwenye gramu 500 kwa mti mmoja. Lakini wenzetu Kenya, wanafika mpaka hizo kilo tano kwenye mti mmoja. Kwa hiyo, wenzetu wamekwenda mbali na Serikali yao inajali. Hatuwezi kwenda mbele kama *speed* itakuwa ndio hii.

Mheshimiwa Lowassa, alipokuwa Waziri Mkuu, alikuja Mbozi, aliona hali halisi, wananchi wanalima na kwa kweli alishawishika na akakubali kwamba hapa kuna sababu ya kupeleka msaada. Mimi namshukuru Mheshimiwa Lowassa aliliona hilo na kwa kweli wananchi wa Mbozi aliwatia nguvu sana, Mheshimiwa Lowassa na sisi tunakushukuru sana. Lakini pia Mheshimiwa Lowassa alipokuwa Waziri Mkuu, aliwaita wadau wote wa

zao la kahawa na wadau wa mazao mengine akawaambia ya kufanya katika kuongeza mazao hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini moja na ambalo nakumbuka lilikuwa agizo kwamba tutoke kwenye tani karibu 45,000 au 50,000 twende kwenye tani 120,000 ndipo tunaweza tukasema tunazalisha kahawa. Lakini kama *speed* ndio hii na mapungufu kwenye zao la kahawa yanabaki kama yalivyo hata maagizo haya ya viongozi wetu hayawezi kufikika hata siku moja, tutakuwa tunazungumza yanabaki kwenye vitabu, hatutafika hata siku moja. Naiomba Wizara ifanyie kazi mambo hayo.

Jambo lingine ninaomba Mheshimiwa Waziri, apige marufuku ununuzi wa zao la kahawa ile *cherry*, wanayoita *cherry coffee.* Kwa sababu ile inapunguza ubora wa kahawa kwa sehemu kubwa sana na kimsingi unawatia umasikini wakulima wetu. Mtu anachuma kahawa debe mbili anakwenda kuiuza kwa Sh. 250/= debe moja, anachuma debe 10 anakwenda kuziuza anakuja kumaliza msimu hakuna alichoambulia. Kwa hiyo, naiomba Wizara ione uwezekano wa kupiga marufuku kabisa ununuzi wa kahawa ile ambayo haijawa *processed,* yaani ile wanayoita *cherry coffee.* Naomba sana Mheshimiwa Waziri, hilo atusaidie sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hebu mwasaidie wakulima na pale Mbozi tuna kituo cha kuzalisha miche ya mibuni, tunaomba mwasaidie wale waweze kuzalisha vizuri zaidi. Pesa ambazo wanatengewa takribani Sh. 10,000,000/= hazitoshi kitu katika kuzalisha hii miche bora ambayo tunadhani inaweza ikatuletea uzalishaji ukawa mzuri na tukafikia uzalishaji wa kilo tano kwa mbuni mmoja, tunaomba sana hilo mtusaidie.

Jambo la mwisho, ninaomba mfuko wa pembejeo, yaani Mfuko wa Pembejeo wa Taifa pamoja na haya tunayosoma kwenye magazeti, lakini bado unafanya kazi nzuri. Nami nashukuru kwamba angalau umeongezewa hela kutoka bilioni tatu kwenda bilioni saba, inaweza ikatusaidia. Ninaomba, Dar es Salaam mbali kutoka Mikoani, kwa vile tunapeleka maamuzi Mikoani, tunaomba huu mfuko uwe *decentralized,* mtu anatoka Mbozi, anatoka Sumbawanga anafuata mkopo Dar es Salaam kwenye mfuko wa pembejeo akae siku tano anafuatilia pale, hapati kitu ni tatizo kubwa. Tunaomba Wizara iangalie namna ya ku-*decentralise* shughuli za mfuko wa pembejeo pamoja na kazi nzuri zote wameweza kuzifanya lakini wapeleke mfuko huu huko Mikoani ili wananchi wetu wasipate mahangaiko na taabu ambazo wanazipata wanapofuatilia mikopo yao kule Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kengele itagonga muda wowote, naomba tu niseme kwamba ninaunga mkono bajeti hii, lakini Mheshimiwa Waziri, hebu awaeleze Watanzania watumaini nini kwenye suala zima la kuinua kilimo katika nchi. Mheshimiwa, nakushukuru sana ahsante.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Chakula, Kilimo na Ushirika. Nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara kwa kuandaa bajeti hii

ambayo inatoa dira na maelezo na mwelekeo wa bajeti hii katika kuboresha kilimo nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, nianze kuongelea suala la bei ya pamba. Unajua ninatoka katika Mikoa inayolima na kuzalisha pamba. Tumekuwa na tatizo sana sisi wakulima wa zao la pamba tunaotoka Kanda ya Ziwa au pengine na sehemu nyingine. Pamba mwaka jana ilikuwa na bei ya Sh. 500/= kwa kilo na bei ya mwaka jana katika soko la dunia ilikuwa ndogo sana, mwaka huu bei katika soko la dunia imepanda, lakini bei yetu kwa wakulima ni ndogo sana, inafika hatua wakulima tunawakatisha tamaa. Mwaka jana wakulima waliuza pamba kwa Sh. 500/=, mwaka huu wanauza kwa Sh. 400/=, wanacheza sasa 420/=. Tarehe 10 Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika alitoa kauli ya Serikali hapa Bungeni akitaka, akielezea na jinsi ambavyo makampuni yanayonunua yaweze kulipa vizuri bei kwa wakulima lakini bado hata kauli hii haitekelezeki, wanunuzi wa pamba bado wameungana wanawanyanyasa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kabisa kushawishika kuomba wakulima wetu wa zao la pamba, kama ikiwezekana wasiuze pamba, wasubiri pamba ianzie Sh. 500/= kwa sababu katika hali ya kawaida wakulima hawafaidi chochote. Tukumbuke kwamba sasa hivi mazao mengine tofauti na pamba yanalipa, ukilima mahindi yanalipa sana, mpunga unalipa sana na dengu, lakini tunajitahidi kuwahamasisha wananchi wetu walime pamba ili kuingiza fedha za kigeni katika nchi yetu.

Ninaomba sana Serikali tuingilie kati katika suala hili. Wanasema kwamba kuna sababu ambazo zinatolewa kwamba pengine Halmashauri zinaingiza vitu mbalimbali mle ndani, lakini sio kweli, huu ni muungano wa wafanyabiashara, wamekubaliana na inawezekana kwamba wanunue kwa bei hiyo na msimamo ukawekwa pale na kwa sababu wanajua hakuna mfumo mwingine unaoweza kusaidia. Ninaomba wakulima wasaidiwe. Wilayani Bukombe, kwa kweli mpaka sasa hivi watu hawajauza sana pamba. Tunazalisha sana pamba na bado wananchi wamekaa na pamba yao na mimi bado nawashawishi wakae na pamba yao wasubiri bei iendelee kupanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani. Mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani ni mfumo mzuri sana kwa jinsi tulivyouona ulivyofanya kazi katika Mikoa ya Kusini. Lakini pia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameeleza katika ukurasa wa 56 kipengele cha 95, ameeleza jinsi walivyofanya majaribio katika Mkoa wa Manyara, Mkoa wa shinyanga; Mkoa wa Shinyanga alijaribia vijiji vichache. Ninaamini wakulima waliouza kwa mfumo ule walipata sio chini ya Sh. 900/= kwa kilo. Lakini leo mfumo huu ambao tumejitahidi hata kuuhamasisha bado unasuasua sana, una vikwazo vingi sana.

Ninaiomba sana Serikali, kama vile alivyoweza kuingilia kati Mheshimiwa Wasira, ndugu yetu, kaka yetu, kwenye zao la korosho, tunaomba aingilie kati katika mfumo huu. Viko vyama vya msingi vilivyokubalika kununua kwa mfumo huu katika Mkoa wa Shinyanga, lakini mpaka leo bado havijapata pesa, wanawekewa vizingiti mbalimbali, hawapati pesa kwa sababu chanzo cha pesa ni kile kile. Anakochukua

mfanyabiashara binafsi ni huko huko, wanakochukua hawa wa mfumo ni kule kule, lakini kwa nini Serikali iliweza kutoa *Government guarantee* katika zao la korosho? Ninaomba Serikali mwasaidie wakulima hawa, saidieni mfumo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inanipa ugumu sana, mimi binafsi nimejitahidi sana kufanya kazi ya Serikali, nikahamasisha mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani katika Wilaya yangu ya Bukombe. Kuna vyama viwili ambavyo vilikubali kufanya kazi hii, Chama cha Ushirika cha Lugunga na Nyasato, lakini matokeo yake mpaka leo hamna, wamekaa tu. Wananiuliza, Mbunge, tufanyaje? Siku ile kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, nikachangia suala hili, nikaamini kwamba labda suala hili litatatuliwa, lakini mpaka leo hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnapofanya hivi, mnatukatisha tamsa hata sisi wanasiasa kufanya kazi ya Serikali ya kuhamasisha. Inaonekana ni afadhali nikahamasishe masuala mengine ambayo hayaingilii nguvu ya Serikali pale. Ninaomba Serikali mtusaidie. Kuna chama cha msingi kule cha Nyasato, cha Lugunga, vimejipanga kununua katika mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani Wilaya ya Bukombe na mkoa mzima wa Shinyanga na kanda ya Ziwa sehemu mbalimbali wengine, tunaomba mtusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongee suala la benki ya wakulima pamoja na *SACCOS.* Tunajitahidi sana na tunasema sana kubadilisha mfumo na maisha ya wakulima, lakini suala hili nimeona Mheshimiwa Waziri amelijadili vizuri sana. Tunaomba sana Serikali tusilete hoja tu, kila wakati tunasema tutaanzisha benki. Tusipoanzisha benki ya wakulima, wakulima wetu hawakopesheki, tunaomba sana tuwasaidie, benki ianzishwe ili tuone namna tutakavyowasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Pembejeo ambao unatoa mikopo inakuwa ni vigumu sana kutoa mikopo kwa wananchi walioko vijijini kama Bukombe ambapo hata hati miliki za mashamba hawana, hawana kila kitu, lakini tunaomba sana Serikali mtusaidie, *SACCOS* ambazo zimekuwa zikiwasaidia zimekuwa na upungufu sana wa wataalamu. Nilikuwa naomba Serikali iangalie sana kwa sababu *SACCOS,* vyama vya ushirika tulivyovianzisha tumekuwa na historia ya vyama vya ushirika kufeli. Tumekuwa na historia ya vyama vya msingi vinapoanzioshwa vinakwenda kufa, inawezekana na *SACCOS* nyingi tulizozianzisha sio ajabu zikafika hatua zikafeli, kwa sababu tunakosa wataalamu wa kuzisimamia.  Tunaomba Serikali iangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Chuo Kikuu Kishiriki cha Moshi, ambacho tawi lake liko Kizumbi. Kwa nini Wizara hii isishirikiane na Wizara ya Elimu ya Juu ili iweze kuboresha hata Chuo cha Kizumbi waanze kusomesha watu wengi waweze kwenda kusaidia *SACCOS* hizi? Kwa sababu *SACCOS* zikiboreka ndizo zitakazoweza kuchukua mikopo na kuweza kuwakopesha wakulima wetu, vinginevyo wakulima wetu watakuwa kwenye hali ngumu, hawapati manufaa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, ninataka niongelee suala la wakulima kwa ujumla na hasa katika malipo yao ya uzeeni. Kilimo kinachangia asilimia

40 katika pato la Taifa. kilimo ni mwaka 2007 kilipochangia 19%. Inaonyesha namna gani watanzania wengi wanavyoshiriki katika kilimo. Nimekaa nikawa najadili sana suala hili nikaona leo nililete hapa Bungeni. Wafanyakazi wanapostaafu wanalipwa mafao yao na sisi Wabunge, tunalipwa *gratitude,* lakini wakulima wanaolima na kuchangia asilimia 40 ya pato la Taifa akishazeeka basi ndio mwisho wake, hata hospitali hajulikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuja na pendekezo kwa Serikali, Serikali ya awamu ya nne tunayohitaji maisha bora kwa kila Mtanzania tusije tukaishia kuboresha kwa wafanyakazi, kuwalipa kiinua mgongo, pengine kwa kulipa wanasiasa kiinua mgongo, ninapendekeza Serikali iandae mkakati maalum, wakulima hawa katika vijijini katika nchi nzima muwatambue, ili nao wanapozeeka imefika muda kwamba amechoka hawezi tena kulima alipwe kiinua mgongo na Serikali. Kwa sababu vinginevyo hawa watu wataishia maisha yao yanakwenda kwisha, yanachakaa na hakuna chochote anachofaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nisisitize sana suala la mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani. Naomba wakulima wangu, naomba vyama vyangu vya msingi vya Nyasato na Lugunga mvisaidie, vipate pesa vinunue. Mtoe *guarantee* benki ili vyama hivi viweze kununua. Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. Nimesimama hapa kuunga mkono hoja ya Wizara hii ya Kilimo na Chakula na pia kumpongeza Ndugu Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu wote walio chini ya Wizara hii. Nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwa kweli anastahili pongezi. Imesema mengi na ameonyesha kwa undani mipango yake ya mwaka 2009, ameelezea hatari ambayo itatupata endapo hatutafanya mabadiliko katika kilimo na mengine mengi. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze kwa kusema kuwa kujitawala ni kujitegemea na hasa katika chakula, watu wa kabila langu ukiwaudhi sana watakujibu kwamba sili kwako. Ndio jibu la hali ya juu analoweza kukujibu Mbena kwamba sili kwako. Sasa nilidhani kwamba Watanzania tungesema hivi tukiudhiwa sana, tunaweza tukajibu hivyo? Kwamba hatuli kwenu nyie watu wa nje, tuacheni, tunaweza! Maana katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 10 mpaka wa 11 anaonyesha kwamba tunajitosheleza kwa asilimia moja na nne. Lakini ameonyesha mapungufu katika maeneo kadhaa na ni mengi.

Sasa mimi nilikuwa najiuliza, asilimia moja na nne inatoka wapi kama maeneo yote ambayo ameorodhesha yanaonyesha kwamba kutakuwa na upungufu? Sasa kwa bahati nzuri hapa anajieleza mwenyewe kwa sababu Mikoa ya Ruvuma, Iringa, Mbeya na Rukwa, haikuorodheshwa katika maeneo ambayo yatakuwa na upungufu wa chakula.

Siri ni kwamba, kule katika miaka 10 iliyopita kumekuwa na uhakika wa mvua na ndio sababu kule kumekuwa na uhakika wa chakula. Ni kwa msingi huo, napendekeza kwamba kama mnataka chakula, basi tuelekeze nguvu zetu mahali pale ambapo pana ardhi na pana uhakika wa mvua. Tanzania inaweza ikaagiza kutoka nje magari, madwa, nguo za kuvaa, viatu, lakini haiwezi kuagiza kutoka nje ya nchi hii maji ya kilimo, hali ya

hewa, mandhari na mambo mengine muhimu. Kwa jinsi unavyoweza kwenda katika maeneo ya nchi yetu hivi sasa ni kwamba *the basic needs are in danger.* Mahitaji muhimu ya nchi yetu na ya watu wetu yako katika hatari ya kutoweka endapo tutazidi kutegemea wenzetu kutoka nje. Kuna mambo unaweza ukategemea, lakini sasa wakubwa wameamua kwamba watazuia uuzaji wa chakula nje. Wamepandisha bei ya chakula, wamebadilisha matumizi ya ardhi na kuelekeza kwenye kilimo cha mimea ya kutoa mafuta ya kuendeshea mashine na mambo mengine mengi.

Mheshimwia Mwenyekiti, Watanzania lazima tubadilike. Mambo yamebadilika, kwa mfano, wakati tunapata uhuru, Mtanzania alikuwa anaishi kwenye kibanda cha kawaida tu, hakuwa na maonjo ya juu ya kutaka sukari, nyumba ya bati na vitu vingine, lakini anaendelea na kilimo kile kile wakati maonjo yamebadilika. Hili ndiyo tatizo! Anataka atumie fedha ya kaeneo ka ekari moja *land tenure* hii kwa kukidhi mahitaji ya kisasa, anataka na luninga, redio, viatu na nyumba ya bati kwa kutumia saruji, haiwezekani! Kwa hiyo, kama unataka kujua kwa undani kwa nini mambo hayaendi, moja ya sababu ni ukame na mfumo wa kumiliki ardhi, tatizo la utaalamu kwamba bado utaalamu wetu ni wa kuning'iniza. *(Makofi)*

Kama alivyosema Mheshimiwa Keenja, peleka utaalamu kwa mkulima mwenyewe, hata tungelipata mabwana shamba milioni tukawapeleka vijijini, kama hawadondoshi utaalamu kwa mkulima mwenyewe tutakuwa tunajidanganya wenyewe. Mfundishe mkulima mwenyewe, peleka elimu kwa mwenyewe. Kwa bahati mbaya, wataalamu wa kilimo hawafuatwi kama shule, Mwalimu hata akibaki darasani, wanafunzi watamfuata, lakini siyo bwana shamba. Bwana shamba hafuatwi na wakulima, ni mahali pachache sana na ni pale labda walipoendelea sana, lakini Mwalimu anafuatwa na wanafunzi. Kwa hiyo, huyu akibaki kwenye *mental holiday* unahesabu tu wako pale wanatembea lakini hawafanyi kazi. Ni vigumu sana kuwabana kwamba hawafuatwi.

Mfano wa Iringa hasa kilimo hiki cha *hybrid* ni mfano mzuri, tumefundisha wakulima leo kilimo cha mahindi Iringa, Njombe huhitaji bwana shamba kwa sababu elimu imeenea kwa wakulima wenyewe na mimi nilidhani hii ndiyo *approach* ambayo tukifuata tutaipata. Lakini vitu kama ukame hakuna jawabu la mkato. Mkisoma vitabu vinavyotabiri hali ya baadaye ya dunia wanaseme matatizo makubwa yatakuwa ni mawili, moja ni maji na la pili ni chakula. Sasa itabidi uamue utumie maji kwa ajili ya chakula au kwa ajili ya kunywa kama ilivyo sasa wenzetu wanasema utumie ardhi kwa ajili ya mimea ya mafuta au kwa ajili ya chakula. Wenzetu wanaweza kuamua, lakini siyo sisi kwa sababu tunaongezeka kwa wingi hali ya ardhi kwa Afrika ina matatizo mengi, mvua zenyewe sio za kuaminika.

Kwa hiyo, ni matatizo magumu sana, tunahitaji kubadilika na kuwabadilisha wakulima waweze kutumia mbegu ambazo zinatoa mbegu nyingi kwa shina moja, mbegu ambazo zinahitaji maji kidogo na zinastahimili ukame. Mambo ya namna hii ni ya utafiti, sasa kuboresha utafiti ni pamoja na kusambaza matokeo ya utafiti kwa wakulima wetu. Maeneo haya bado ni dhaifu sana na inachukua muda mrefu toka mambo yamevumbuliwa mpaka yakamfikie mkulima.

Lingine ambalo naliona katika maandishi ya Mheshimiwa Waziri ambalo ni jambo la msingi, amesema kwamba kilimo cha kisasa ndiyo msingi wa uchumi wa kisasa na mimi nime-*add* hasa katika Tanzania. Sasa katika hali hii nilikuwa nauliza suala ambalo wenzangu wengi wameuliza, hivi ukitembea katika vijiji vyetu sasa hivi, ni wangapi wenye *doctorate* wanalima? Wangapi *form four* wanalima? Kwa hiyo, tuna matatizo. Hivi sasa asilimia 60 ya vijana wetu wako mijini wenye nguvu. Nguvukazi hii haitumiki, wana mategemeo yao wanaishi mijini hawalimi na waliobaki vijijini ni wazee na akina mama hasa akina mama.

La pili, bado asilimia 70 ya zana za kilimo ni jembe la mkono, labda asilimia 20 ndiyo plau, yaani jembo la kukokotwa na ng'ombe, asilimia 10 ndiyo trekta na kule Kigoma ni matrekta manne tu Mkoa wote. Sasa katika mazingira ya namna hii utafanya mapinduzi ya aina gani? Wazee wamezeeka mpaka na mgongo umepinda ndiyo analima na ndiyo tunawategemea watulishe, tunawashukuru sana wakulima wa nchi hii.

Lakini pia wanalima kwa sababu ya imani tu hawana la kufanya, lakini kama ungefanya hesabu ya muda anaotumia, mbolea kama mnavyofanya ninyi watu mnaosomea mambo ya mahesabu haya, kwa kweli ingekuwa ni wakulima na mimi hofu yangu ni kwamba hii kazi ya sulubu tusipoangalia tutawakosa watu kabisa, vizee vitatoweka, hawa vijana wakishika jembe wanatapika, kwa hiyo ni tatizo. Tutawezaje kufanya kilimo kiwe ni cha kuvutia ili vijana wabaki vijijini wanalima? Waliobaki mpaka sasa hivi labda ni Mkoa wa Rukwa na mahali pengine. Sasa katika hili ndugu zangu tuna kazi kubwa ya kufanya, sio kazi ya Keenja peke yake bali ni ya kila Mbunge na kila Kiongozi vinginevyo nchi hii tulipofikia sasa vijana wanakimbia hawataki kulima na kulima kunakatisha tamaa, unalima mwaka mzima ndiyo ukapate Sh. 40,000/= wote wanakimbilia kwenye hii biashara ambayo wanafanya biashara akifika jioni ana Sh. 40,000/= faida wewe unasubiri miezi saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, labda niende kwenye ushauri wa haraka haraka kwa sababu hizi kengele haziangalii tunachotaka kusema hapa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba ili twende kwa haraka na kuendesha nchi yetu vizuri huenda wakati umefika wa kufanya yafuatayo:-

Moja, tutumie vizuri raslimali ardhi, tuwe na ramani ya sifa za ardhi katika nchi yetu na tutumie vizuri ardhi ili sifa ziendane na aina ya zao ambalo linafaa katika eneo lile. Kwa mfano, Mheshimiwa Rais wetu aliwahi kusema kwamba Mkoa wa Morogoro ni ghala la chakula la Tanzania. Sasa nenda kaangalie hili ghala la chakula linavyofujwa na baadhi yetu kwamba tumelundika ng'ombe kule, wanaharibu ardhi na baada ya muda maji yatakauka, ardhi itachakaa na maana ya ghala itafutika.

Kama Watanzania tungekuwa *serious* na tungeamua kwa makusudi kabisa tungesema hivi mabonde haya ya Mbarali, Lwiche, Dakawa, Pangani, Kilombero na Rufiji ndiyo yawe maghala ya chakula, ndiyo Ihefu ya Tanzania na tukaamua kwamba hapa tunalima chakula kwa ajili ya Taifa letu na kuuza nje na kwa sababu chakula sasa ni

dhahabu, ni kama jatrofa. Tungeelekeza nguvu zetu kwenye chakula na tukawapa nguvu wachache na Serikali lazima ianze kujitazama upya. Swali ni kwamba, ni *law and order* wakati watu wanakufa kwa njaa, mimi sielewi *law and order* tutai-*maintain* vipi katika mazingira ya namna hiyo?

Ni lazima kwa nchi masikini hata wakati wa ukoloni *DC* kazi yake ilikuwa *law and order* na maendeleo. Sasa sisi hapa ni mwiko kwa *DC* kwa Serikali kufanya maendeleo ni mwiko, hizi ni *concept* ambazo ni za wenzetu ambao waliokwishakuwa *sophisticated* wanawake walioendelea, sisi hapa tunasema Serikali ikunje mikono, isubiri *private; private* yuko wapi? Hawa maskini kandambili hawana, redio, *box number,* wanaishi kwenye makuti *house, privilege* ni kufa upesi. Hawa ndiyo tunasema ndiyo *private sector* ya sisi hapa, ni lazima u-*stimulate*.

Mimi nimekwenda China, kila mwaka wanafundisha Wachina zaidi ya milioni 40 waingie kwenye *entrepreneurship* kwa makusudi, kwa sababu kwa miaka iliyopita walikuwa wajamaa. Kwa hiyo, hata kutabasamu kwenye biashara walikuwa hawajui na kwa ufundishi.

Sasa tukidhani hawa watakwenda hivi hivi, waliosoma vyuo vikuu hawana fedha na kwa bahati mbaya nchi hii wale wenye fedha kidogo siyo *sophisticated* sana, hawakuchelewa kwenye shule, waliochelewa kwenye shule ndiyo hawana fedha, wana mawazo. Sasa sisi lazima tuwe na makusudi ku-*handpick* watu kusema wewe nenda kalime na tunakupa nguvu hii. Vinginevyo, haiwezekani! *It is very risk* kuingiza fedha yako ya nadra kwenye kilimo ukategemea utakuwa unaniambia haiwezekani. Ni lazima tujifunze, tuangalie kwa undani kikwazo kikubwa ni nini, ndugu zangu tusipoangalia hayo tutakwama.

Lingine, ninapendekeza kwamba tupeleke utaalamu, kila Kijiji kiwe na mwakilishi wa chombo cha utabiri wa hali ya hewa kiwe na mwakilishi kusudi awe anakusanya taarifa na taarifa zile tutumie vyombo kama shule kuweka vile vyombo kusudi taarifa za kilimo ziwe tunatoa mara kwa mara na wananchi wetu waweze kujua kwa faida yao, vinginevyo hiki chombo hakikuwekwa kwa sababu ya kilimo.

Lingine niliona kwamba haya maonyesho ya kilimo tushushe mpaka ngazi ya Tarafa. Mpaka sasa maonyesho yapo kwenye miji; lengo ni la nani? Mkulima wa kawaida hawezi kufika Morogoro, Arusha au Mbeya. Tupeleke kule kule kwa lengo la kueneza elimu ya kilimo ili kusudi aweze kufaidika na kitu hiki. Mimi naipongeza *TASWA* kwa kazi nzuri wanayofanya lakini twende chini zaidi kwa lengo la kumlenga yule, vinginevyo itakuwa *another trade fair.*

Lingine ambalo nataka nimalizie hapa ni la Jimbo langu, kwamba Lupembe tunalima chai na mazao mengine mengi tu, lakini ile barabara kwa sababu ya ardhi, mwaka mzima hatuwezi. Kwa hiyo, wakati wa mvua tunamwaga chai porini, tulidhani mngeongea na Wizara ya Miundombinu muangalie kule ambapo mnapata dhahabu tupeleke barabara kusudi ile dhahabu itoke, vinginevyo inakuwa ni kazi bure, watu wanalima halafu robo tatu ya chai inapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ningependa kumalizia kwa kusema kwamba tafuteni kwanza maendeleo katika kilimo na mengine yote mtapewa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI – MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Ahsante sana. Mtu mzima dawa! Kwa hiyo, ni ushahidi tosha kwamba mchango wako ulikuwa mzuri na nilimwita Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, lakini simwoni na vilevile nilimwita Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, pia simwoni. Kwa maana hiyo, nitamwita Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba naye atafutiwa na Mheshimiwa Hamza Mwenegoha na Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura ajiandae.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kwa nafasi ulionipatia. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri. Ukisoma hiki kitabu, kwa kweli kina mikakati mingi sana ya kuleta mapinduzi katika kilimo chetu. Mimi nilitaka kwanza nijiulize, sasa hivi duniani liko tatizo.

Dunia iko kwenye *crisis* ya chakula, duniani *demand* ya chakula ni kubwa, bei ya mafuta duniani imepanda, kuna matatizo ya hali ya hewa, yaani *climate change* sasa lazima tujiulize sisi kama Watanzania katika mazingira haya tunafanyaje? Tunakwenda na *style* hiyo hiyo ambayo tumekaa nayo kwa miaka 40? Lakini kilimo chetu mvua isipokuja mwaka mmoja lazima tuombe chakula, baadhi ya Wilaya zetu lazima kuwe na njaa.

Sasa lazima tujiulize: Je, tukienda na hali hii, hatuombei itokee, lakini ikitokea mvua isiwe nzuri kwa sababu kuna matatizo haya ya hali ya hewa, itakuwaje? Kwa hiyo, ndiyo maana nikasema ni lazima mipango yetu iwe ni kufikiria huko kwa hali halisi inavyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tuna hekta milioni 40 za *erable land* tunakaribia hekta milioni sita za maeneo ambayo unaweza kufanya kilimo cha umwagiliaji, lakini tunatumia kwenye *land* hiyo, tunatumia hazipungui zaidi ya asilimia 15, ndiyo hiyo inayotumika kwa ajili ya kilimo. Sasa tunajiuliza, katika mazingira haya ambayo sasa kuna tatizo hili kubwa duniani, sisi tunafanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninasema kupanga ni kuchagua, Mwalimu alituambia. Mimi nilidhani ningeomba Mheshimiwa Waziri aje na mkakati unaopimika kwamba tuamue sisi kama nchi kwamba moja ya biashara yetu kubwa ni kuhakikisha sisi tutakuwa na chakula na Taifa lolote duniani lenye nguvu kazi ya kwanza lazima uwe na chakula hata nyumbani kama huna uwezo wa kujinunulia chakula huwezi kuwa na familia ambayo iko *stable*. Kwa hiyo, tuamue kama nchi kwamba sisi cha kwanza ni chakula, tujitosheleze, lakini pia tuanze kufikiria na sisi kwamba tuwe na *food basket ya region* hii ya Afrika, tukifikiri hivyo. Ninaamini mambo mengi sana yatakwenda. Lakini yapo mambo lazima tuyafanye ili kilimo chetu kiweze kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najiuliza, leo hii kuna habari ya *biofuel* imeanza kuja kwa kasi kubwa sana ya jatrofa. Naomba niwe mtu wa mwisho kukubali

Tanzania, sisi tuanze kulima jatrofa, ni kuchagua tu. Watu wengine walime jatrofa sisi tulime chakula, maana yake ni moja tu. Ardhi hii ambayo mtaitoa kwa ajili ya jatrofa, maana yake hamtalima chakula, lakini kesho mkipata njaa, jatrofa haiwezi kuwa *solution* ya chakula, haiwezi. Lakini *trend* ya dunia ndiyo hiyo.

Kwa hiyo, nasema anayegawa ardhi kubwa kwa ajili ya jatrofa, nasema hapana!

Lakini unajiuliza, Wazungu hawa ambao wanatuambia leo tulime jatrofa, ndiyo ambao miradi yote mikubwa ya kilimo nchini tumefanya ni hekta moja au hekta mbili, mageuzi tunayoyasema ni ya hawa wakulima wa hekta moja au hekta mbili. Lakini kwenye jatrofa wanasema tafuteni mashamba makubwa, kwa nini kwenye kilimo tusitafute mashamba makubwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninasema kwamba yapo mambo, lakini ni lazima tufanye kama nchi. Kwanza, hatuwezi kuepuka kilimo cha biashara. Kwa hiyo, ninachofahamu mimi, hatuwezi kuiepuka na hii ndiyo itakayotutoa hapa tulipo.

Mimi nilikuwa naangalia mfano wa Kigoma. Kigoma tuna hekta milioni 2,668,000 zinazolimwa ni hekta 520,000, asilimia 19 peke yake ndiyo inayolimwa. Sasa unajiuliza, tuwe na mkakati wa kulima hizi zilizobaki asilimia 80 na hizi asilimia 80, hao watu wetu wanaolima hizi asilimia 20 ambao ndiyo Watanzania, wote tuwasaidie, tuwape mbolea na tufanye kila kitu, mimi nakubali. Lakini hii nyingine tuitafutie utaratibu ili nayo ichangie kwenye uchumi wa nchi yetu. Lakini hayo hayawezekani kama mambo yafuatayo hayatawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tujiulize, sheria zetu za ardhi zinasemaje? Lazima tujue Sheria ya Ardhi *(Tenure land)* ikoje? Iko sahihi ili hawa wakulima wetu watumie ardhi hii ku-*access* mikopo, watumie ardhi yao kwa ajili ya shughuli ya kilimo na waweze kufaidika? Tunaifanyaje sheria yetu ya ardhi? Lazima tuiangalie.

Lakini pia kuna suala la kodi. Lazima wakulima hawa nao wapewe *incentives* kama watu wanaokuja kufanya vitu vingine wanapewa *tax holidays,* kwa nini kwenye kilimo hakuna unafuu wa kodi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kilimo kikue, lazima hili lipatikane. Mambo ya mafuta kwa maana ya diseli kwa ajili ya kilimo, asilimia 60 ya gharama za kulima mashamba makubwa zinakwenda kwenye mafuta ya dezeli, lakini huyu mkulima hapewi punguzo kwa maana kodi haisamehewi. Huyu mkulima hawezi kutoka, kwa hiyo, lazima tujiulize tunafanyaje ili kuweza kumsaidia mkulima?

Jambo lingine ni *Value Added* kwenye mazao ya kilimo. Wenzangu wamesema humu, kama hatufanyi *Value Added* kwenye mambo ya kilimo, kilimo chetu tutabaki tunalalamika, tunasema tuna maendeleo na kadhalika, lakini kama hakuna *Value* hatuwezi kufika mbali.

Kwa hiyo, ni lazima tuanze kujiuliza na mimi nina-*propose* kwamba kila Halmashauri ianzishe *a small holder* ya *processing* ya mazao yetu, siyo gharama kubwa. Tuanze na Halmashauri chache, tutaweza kusaidia kuongeza *Value* kwenye mazao yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna jambo hili la vyuo vyetu vya kilimo, tuna mpaka Chuo Kikuu cha Kilimo, lakini ninaamini wale watu wa *SUA* hawana shamba la mfano hata moja. Kuna maswali najiuliza na mambo haya lazima tuwe na mfano. Kwamba, tunawachukua wakulima kutoka Mkoa wa Kigoma twendeni tukawaonyeshe mashamba yaliyolimwa kwa utaratibu mzuri. Lakini napata wasiwasi kwamba pamoja na vyuo vingi sana, tujitahidi, hayo mashamba makubwa yawepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikawa naangalia, kwa nini nasema hili la mifano ni la msingi sana? Tarehe 25 Aprili, 2006 aliyekuwa Waziri Mkuu wa Uingereza Tonny Brair alianzisha kampeni ya kutaka Uingereza wafanye mazoezi, lakini kampeni ile hakuanzisha kwa kusema unaziona picha, yupo kwenye *gyim* naye anafanya mazoezi anawaambia, jamani, hatuna *choice.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lLazima Waingereza wote kwa ajili ya afya zetu, mazoezi ni muhimu. Kwa hiyo, sisi lazima tuanze kuwa na mifano sisi kama Viongozi. Jana Mzee Makamba amesema na viongozi tuwe mifano, tusiyaseme haya kwenye maandishi tu. Tumesema inatosha, ni wakati sasa wa kutenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna bonde la Lwiche. Bonde lile ni zuri kweli ! Wakati ule Mkuu wa Mkoa ni kaka yangu Mzindakaya, Mzee wangu aliita watu kwa ajili ya Bonde la Lwiche, Waitaliano wale wakafanya *study* wakasema ukiamua ukafanya kilimo cha kweli kweli cha umwagiliaji kwenye mto wa Lwiche unaweza ukapata chakula cha kulisha Mikoa 10 ya nchi hii. Lakini limekaa tu lile mpaka tutaondoka kitakuja kizazi kingine na maji yale yanaingia ziwani, lakini najiuliza, tatizo ni nini? Ukisoma kwenye kitabu humu, Lwiche haimo *anywhere* hekta 10,000 za *erable land* hakuna anayeongea, *it is non of their business*. Ndugu zangu hatuwezi! Kwa sababu mambo ya kutegemea mvua yana matatizo yake, itakuja siku mvua itakataa, mito tunayo, lakini tunasema eti leo tuna njaa, kwa nini?

Nchi hii ina mito mikubwa, ukiacha mito michache ambayo imefanya kazi ya kutuzalishia umeme, mito mingine yote inapeleka maji baharini na ziwani. Mito hiyo hatuitumii kwa maji kwa ajili ya kupeleka labda watu wanywe katika vijiji na miji yetu, bado kuna matatizo ya maji lakini mito ipo. Mito hiyo hatuitumii hata kwa *tourism* wala *agriculture*. Sasa Mungu alitupa mito hiyo ya nini? Imefika wakati jamani tuitumie! Unatumia kile ulichonacho, *unless* uniambie sisi tuna faida nyingi ambazo hatuzihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kutengeneza *land bank*, ni muhimu sana, sasa wenzetu wa Wizara ya Kilimo watutengenezee hiyo benki ya ardhi tujue ni ardhi gani inafaa kwa kilimo hiki, ni ardhi gani inafaa kwa kilimo kile na iko wapi.

Hatuwezi kuwa tunakwenda tu, ni lazima tu-*integrate* huu mpango mifugo tunaihitaji na kilimo tunakihitaji, lakini tukianza kusema leo tusukumane huku na kule na

dunia inasema, hivi ni kwa sababu hatuna mipango kwa hiyo *land use plan!* Mimi sioni! Lazima tuwe na *land use plan,* tutumiaje ardhi yetu, ni ardhi gani tunalima mahindi, ni ardhi gani tunalima mpunga, ni ardhi gani tunalima kitu gani ili ijulikane na hata watakapokuja hawa *investors* kwa maana labda Watanzania tuwawezesha tuweke mfuko tujue tunawapeleka wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekwenda Kilombero, Kilombero amekuja *investor* pale, tumempa lile shamba. Lakini leo maisha ya watu wale, *out growers* yamebadilika kuliko miaka ile ya nyuma wakati walikuwa na ardhi ile ya miwa, miwa ile haiwasaidii. Kwa hiyo, nasema, ni muhimu sana, sasa hivi tujitahidi kwamba baadhi ya maeneo akipatikana mtu yule ataweka kiwanda. Hiyo *Value Added* ataongeza, lakini watu wetu tutakuwa tumewapa soko la kwenda kuuza yale mazao yao. Kwa kufanya hivyo, ndipo tutakuwa tumewasaidia.

Juzi Mheshimiwa Rais alikuja Kigoma, tukampeleka kule Kigoma kwenye Mto Malagarasi, unapoanzia kule, kuna sehemu ukivuka mpakani Burundi, Burundi wana kiwanda kikubwa sana cha sukari, lakini upande wetu sisi ambao ndiyo tuna ardhi nzuri zaidi kuliko yao hatulimi miwa, lile bonde tunaliangalia tu kwenye Jimbo la Mheshimiwa Nsanzugwanko.

Mheshimiwa Rais akasema naombeni tukubaliane watu walime miwa, soko lile pale, Burundi wakasema mkilima miwa soko hili hapa, lakini yote haya haiwezekani, tunasubiri mpaka tuambiwe, jamani! Umefika wakati watu wetu tuwe *responsible* kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maneno tunasema mimi ninaamini maendeleo ya nchi yoyote duniani katika mazingira sasa ya soko ya uchumi wa soko, tunahitaji Serikali na tunahitaji na *private sector*. Tukidhani tunaweza tukaendelea labda na *private sector* ni Serikali ndiyo ifanye kila kitu basi, tutaongea miaka yote kuhusu kilimo, mvua ikikataa tunapigwa na njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umefika wakati tuweke *clear National Policy* namna ya kuwasaidia watu wetu tuweke mifuko waweze ku-*access*, tuanzishe hiyo benki ili watu hawa waweze kwenda kufanya kazi ya kilimo. Leo hii, mtu hata akimaliza *degree* ya kilimo *incentives* za kwenda kulima hazipo wapi wana-*access* mikopo?

Lakini pia *policy* yetu haipo *clear,* kwa hiyo, matokeo yake hata tungeweka watu wengi sana na kuwapeleka huko vijijini hao wanaoitwa wagani matokeo yake hela nyingi zitaishia kununulia pikipiki, zitaishia kuwapeleka kwenye semina, lakini kwenye kilimo chenyewe pesa hizo hazitakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema, nadhani tumekaa kama Taifa kwa miaka hii yote tuliyopita labda tujiulize upya: Je, *strategy* yetu ya kilimo ni sahihi? Kama kuna maeneo, lazima tubadilishe *our strategy* kwenye kilimo, ni lazima tubadilike sasa ili tuweze kwenda mbele kwa sababu tumepigiwa kengele, juzi ametuambia Naibu

Katibu Mkuu - Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Mtengeti Migiro kwamba hii ni kengele, matatizo yanayoendelea duniani ni kengele kwetu tushtuke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI – MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Ahsante sana Mheshimiwa Serukamba na sasa nitamwita Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha naye atafutiwa na Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura na Mheshimiwa Suleiman Kumchaya ajiandae.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo tu juu ya Muswada huu.

Kwanza, nawapongeza kabisa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu wote wa Wizara ya Kilimo, kwa kweli wamejitahidi sana kutayarisha hotuba nzuri sana ambayo imeletwa kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, sote tunakumbuka na tunajua kwamba kilimo ni muhimu sana, lakini tukishatoka hapa kwenye bajeti, tukishazungumza kilimo hapa kila mtu anakwenda njia yake, tunakisahau kilimo. Kwa nini tunakisahau? Kwa sababu sisi ni wepesi kutangaza majanga kulikoni kutangaza neema, wepesi kutangaza matatizo, kulikoni kutangaza elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inayo sheria ya kilimo, inayo mipango ya kilimo, wapo mabwana shamba mpaka ngazi ya Kata na Serikali imewagharamia mpaka kuwajengea nyumba nzuri kabisa, lakini hawa hawatumiki kuwaelimisha wakulima. Wapo wapo tu! Hawatoi elimu kwa wakulima na pengine hata wenyewe mashamba hawana, kwa hiyo, watu hawana hata mfano wa kuiga. Naomba Wizara iwaambie hawa watu wafundishe wakulima katika aina ya madarasa sasa.

Lingine, dunia imetangaza bei kubwa sana ya chakula na janga kubwa la chakula ambalo lipo mbele yetu, lakini vilevile dunia imetangaza bei za mafuta, tumetangaza hii kwa haraka sana na kwa ukubwa sana mpaka wananchi wote karibu wanajua. Lakini hatushtuki.

Mwaka 1974 Taifa hili lilishtuka, kiongozi aliyekuwepo alitangaza kilimo cha kufa na kupona, watu walilima mpaka kwenye vichochoro vya Dar es Salaam, mpaka viwanja vya mpira watu wakapanda mahindi, mpaka Wakuu wa Mikoa walitia kufuru kulima na kukata chakula. Hivi kinachozuia nchi sasa baada ya kujua, kuna janga kwanza kuchukua hatua ya haraka kusema mwaka huu ni mwaka wa kufa na kupona kwa kilimo, kila mtu alime ekari moja; ni nini? Tatizo letu nini? Mnaogopa nini kuwaambia watu ukweli kwamba sasa jamani tuna matatizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kubwa linalonishangaza, sisi tunajua kabisa kwamba kutakuwa na upungufu wa chakula, bahati nzuri Wizara inatupa taarifa kwamba mwaka huu kutakuwa na upungufu wa chakula wa asilimia kadhaa, lakini upungufu huu wa chakula mara nyingine huwa najiuliza, hivi unapangwa ili wafanyabiashara wa

chakula wapewe nafasi ya kuagiza chakula nje na waambiwe watapewa bila kodi halafu wanakuja hapa wanauza kwa bei kubwa kabisa, kwa sababu kuna Mikoa ambayo inazalisha chakula kwa wingi sana, kwa nini maghala yasijengwe huko na chakula kikanunuliwa na kuwekwa? Kwa nini chakula kinunuliwe nje baada ya Mikoa hii kuzalisha na kuuza chakula hicho nje? Tatizo ni nini? Maamuzi ama pesa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni pesa mbona tunapoteza tunapowapa ruksa hawa wafanyabishara kununua nje bila kodi? Kwa nini hatujengi maghala ya kutosha angalau kila Mkoa na tukafanya makusudi kununua, tukajaza maghala kwenye Mikoa hiyo? Wakati mwingine najiuliza, tatizo ni nini? Ni maamuzi, uwogai? Jamani tusiseme tatizo ni fedha, fedha zipo nchi hii! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji kwenye kilimo unapungua, nami kwa kusema ukweli inanishangaza. Tumeimba kilimo ni uti wa mgongo, kilimo ni uti wa mgongo, sasa sio uti wa mgongo tena, kwa sababu tunaugeuza nafikiri ni mti tu tumeupanda.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Ni kiuno. *(Kicheko)*

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Labda sasa ni kiuno kama anavyosema Mzee Makwetta, kwa sababu unapotoka asilimia 6.2 halafu unatoa asilimia 4.6 ndiyo kusema mwakani utakuwa kwenye asilimia tatu. Lakini sote tunahitaji kula. Zimbabwe wanapigana kwa sababu ya ardhi, chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kila mahali utakapoona kuna mapambano, wanapigania ardhi ambayo ni nzuri kwa kulima mazao ya chakula. Tanzania tunayo ardhi kubwa sana, mipango ipo mizuri, tatizo ni nini? Kukifanya kilimo kiweze kutulisha sisi wenyewe! Tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema nitachangia kidogo na nia yangu ni kuchangia kidogo tu na sasa naomba nichangie kuhusu Jimbo langu. Zao la pamba, wenzetu wa Mkoa wa Mwanza na *zone* nzima ile wanazungumzia tofauti ya bei ya mwaka wa jana na mwaka huu. Kila wakizungumza, namkumbuka Marehemu Indira Gandhi alipokuwa anatoa mfano kwamba, kama wewe unalalamika, huna kiatu, unakwenda miguu mitupu, mwenzako atalalamika hana mguu wa kuvalia kiatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inafanana kabisa na sisi. Wakati watu wa Mkoa wa Mwanza wanalalamika bei ya pamba yao mwaka huu imepungua, sisi hatuna mnunuzi wa pamba. Tunauliza tutamwuzia nani? Nitatoa mfano halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahenge, anapotoka Waziri wa TAMISEMI, sasa huko wakiuliza pamba tutamwuzia nani, hatuna mtu wa kumwuzia, wanaambiwa nendeni Mahakamani mkashtaki. Wakamshtaki nani? Hivyo unapotaka kumwuzia mtu ukamshtaki kwa kutokununua, si atakwambia jibu rahisi tu kwamba sina pesa? Jamani, Mkoa wa Morogoro tunalima pamba, tunaomba Bodi ya Pamba mje mnunue, mlituhamasisha kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu, ukianzia Selembala, Mvuha, Dutumi, Mngazi, Dakawa na Kisaki tunalima pamba na pamba ya *long thread*, lakini ipo majumbani, mnataka nyumba hizi ziungue, nyumba zetu sisi ni *full suit*, kuanzia chini mpaka juu ni mabua, sasa ukiwasha tu kibiriti nyumba imeondoka na pamba imeondoka, inakuwa kama petroli. Tunaomba mnunuzi wa pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna zao la ufuta. Morogoro kuna mbegu ya ufuta mweupe na tunalima ufuta mweupe. Kuna tajiri mmoja ametuma watu wake wa kununua ufuta Morogoro Vijijini, maajabu wanayoyafanya, wananunua ufuta huu mweupe wanachanganya na ule ufuta mweusi.

Kwa hiyo, unatokea ufuta chotara, matokeo yake thamani ya ufuta wa Morogoro imeshuka kabisa kwa sababu anasema ufuta huu sasa nitauza bei gani? Anapelekewa yule tajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana tajiri mwenyewe yupo humu ndani ya Bunge, nami nimeshamwona na namwambia kwamba watu wake anaowatuma wanadhalilisha wakulima wetu na pia wanamwibia fedha kwa kusema wananunua ufuta mchanganyiko. Morogoro tunazo kabisa mbegu za ufuta mweupe zenye bei kubwa, lakini hawa wananunua kwa bei ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi wanaponunua ufuta huo wananunua na madebe ya mchanga, wanachanganya kwenye ufuta kusema kwamba, wazalishaji wa ufuta kule Morogoro Vijijini tunatia mchanga. Ushahidi huu ukienda Dutumi, Mngazi na kwingineko utaupata. Wakulima sasa tunalalamika wenyewe. Tunamwomba yule tajiri awasimamishe watu wake wale wanaomtapeli wanatuharibia soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilihamasisha vijana wa Dutumi, Mvuha, Kisaki kwa sababu kule kuna mito, tulime mazao tofauti kidogo, tembo ambao ninyi hamtaki kusema tembo mnasema ndovu, kule kwetu hatujui ndovu ndiyo huyo huyo tembo, wanatunyanyasa sana kwa mazao haya ya mtama, mahindi, yaani wanatunyanyasa kweli kweli!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mimi mwenyewe nilikwishakuwa tayari kuvuna hekari zangu mbili za zao la maboga, nikaagiza roli kutoka Dar es Salaam kuja kuvuna asubuhi kama vile tembo wametumwa, wamekula ekari mbili zote na watu wakasema wamefanya vizuri wamekula shamba la Mbunge, atachukua hatua sasa. Hatua gani nitakazochukua? Kwa hiyo, tunabadilisha tu mazao, vijana hawa wa Dutumi wanalima sasa kabichi, tikiti, karoti na vitunguu, wanajitahidi kweli kweli!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kufanya Mkutano wananiletea makapu kwa makapu wanasema wewe ulisema tulime, masoko yatakuwepo, sasa nunua wewe. Wakati mwingine unajiuliza, hivi ninyamaze, kwenye mikutano tusizungumze masuala haya, haiwezekani! Wizara ipo, wataalam wapo, Maafisa Ugani wamepotea, lakini najua wapo, pombe zinawasumbua sana, lakini lazima tupate masoko ya kuuza mazao yetu, ama sivyo umaskini utaendelea na Mbunge itabidi unyamaze kuzungumzia kilimo, watu walime

wanavyoweza. Kibaya zaidi wakulima wanasumbuliwa na kuchanganya kilimo na mifugo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa…
*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Muda wangu umekwisha?

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mungu aibariki sana Tanzania. Naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Awali ya yote, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yake bila kumsahau dada yetu Mkurugenzi wa Mfuko wa Pembejeo, dada Mariamu. Kwa kweli kazi kubwa inayofanywa na Wizara hii ni nzito, jukumu ambalo tumewapa Watanzania hawa ni kubwa na tunashukuru kwamba kwa kiasi kikubwa wanajitahidi kufanya kazi hiyo kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja hii, vilevile kuunga mkono yale mengi yaliyoelezwa na wenzangu waliotangulia. Kwa mantiki hiyo, kwa kuwa ni mchangiaji wa mwisho, yale ambayo nilipanga kuyazungumzwa, tayari yamezungumzwa na wenzangu na sio vyema kuyarudia ila kwa bahati nzuri kuna baadhi ya mambo ambayo hawakuyazungumza au yamezungumzwa kwa wepesi kidogo, nitajitahidi kuyaongezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 45 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameelezea juu ya udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao ya kilimo. Akaorodhesha baadhi ya visumbufu hivyo, alielezea juu ya nzige, kwelea kwelea, viwavi jeshi, panya na magonjwa ya mazao ya kilimo. Lakini kwa masikitiko makubwa, hakumzungumzia mnyama tembo licha ya kwamba Wabunge wengi tumekuwa tukilalamika sana juu ya huyo mnyama. Jimbo langu la Tunduru tembo anasumbua sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalazimika kutumia jina hili tembo, kwa sababu ndiyo jina rasmi huku bara, sasa kama wenzetu wa maeneo mengine wanakwazika, wataniwia radhi, labda watafute jina lingine.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtutura tunaomba usitafsiri hilo jina, endeleo na mchango.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, panya inaweza ikamchukua takriban wiki tatu mpaka nne kula hekari moja ya mazao, lakini kama ilivyoelezwa na mchangiaji aliyetangulia, tembo anaweza kutumia masaa matatu tu kugharikisha shamba lenye ukubwa wa hekari mbili mpaka tatu. Sasa nimewashangaa wenzetu wa kilimo, bila kuzungumzia uharibifu unaoletwa na tembo. Sasa tunawaomba watuambie wakati wa majumuisho yao wana mkakati gani wa kumdhibiti mnyama huyu katika uharibifu wa mazao na mimea yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumziwa na wazungumzaji wengi juu ya mapinduzi ya kilimo ni uwezekano wa kutumia vitendea kazi vya kisasa ili kuweza kuboresha kilimo. Sana sana wengi wamegusia zaidi masuala ya trekta. Vilevile naamini wenzetu waliotangulia walilazimika kutumia hatua mbalimbali za kimaendeleo mpaka wakafikia sasa hivi wanatumia matrekta pamoja na ma-*combine harvester*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania hatulazimiki kutumia kupitia hatua zile walizopitia wenzetu, kutoka jembe la mkono, jembe la kukokotwa na ng'ombe, farasi au punda, wakafikia *power tiller* na sasa hivi matrekta na ma-*combine harvester*. Hatulazimiki kupitia hatua hizo zote, hatuna sababu kuona kwa nini tuna-*insist* kutumia wanyama kazi katika karne hii ya sasa hivi na bado tunataka tulete mapinduzi ya kilimo, kwa nini tusichupe baadhi ya hatua ambazo wenzetu waliotangulia walipitia? Walipitia kwa sababu kipindi hicho hakukuwa na matrekta. Sasa hakuna sababu ya ku-*insist* kutumia wanyama kazi, nadhani fikra zetu tuzielekeze katika matumizi ya matrekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini hilo linawezekana, nitatoa mfano mdogo tu kwamba hili linawezekana endapo Serikali na wananchi wote kwa ujumla wetu tutaweza kuamua kulifanya.

Kwa mfano, bahati nzuri hili niliwahi kulizungumza katika michango yangu iliyotangulia. Tunazo hizi shilingi bilioni 21 ambazo zimebatizwa jina la JK. Fedha hizi kama tutaamua kuzitumia, tusitishe mwaka mmoja tu kuwakopesha wajasiriamali, lakini tubadilishe tuwakopeshe wajasiriamali kwa namna nyingine, tukanunue matrekta, shilingi bilioni 21 kama Serikali itatumia fedha hizo kununua matrekta na kuyapeleka katika maeneo ambayo yanazalisha zaidi mazao ya chakula, katika nchi yetu tutaweza kuwa na matrekta yasiyopungua 840 kwa bei ya trekta moja shilingi milioni 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matrekta haya 840 katika Mikoa yetu ya *big four,* kila Mkoa ukapelekewa matrekta 100, maana yake kutakuwa na *balance* ya matrekta 440 ambayo yatagawanywa kwenye Mikoa mingine ambayo inazalisha mazao ya biashara. Nadhani ndani ya mwaka mmoja mapinduzi makubwa sana ya kilimo yatatokea katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizo kama tutaamua kununua *power tiller* kwa bei ya sasa hivi ambayo ni shilingi milioni tano, tutapata *power tiller* 4,200. Sasa *power tiller* 4,200 yaingie kwa mara moja katika nchi yetu, mapinduzi makubwa kiasi gani ambayo tunaweza kuyafanya!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya yangu ya Tunduru sasa hivi ni tegemeo kubwa kwa mchele katika Wilaya ya Nanyumbu, Masasi, Newala, Mtwara pamoja na Wilaya tunazopakana nazo za Mkoa wa Lindi. Tunaweza kuwapelekea mchele ndugu zetu hawa kwa sababu wenzetu hawana mito mingi wala mabonde mengi, lakini Tunduru tuna mito mingi na mabonde mengi.  Tunaweza kuzalisha kiasi hicho cha mchele kwa kutumia jembe la mkono.

Hivi kama tutapelekewa matrekta, ni kiasi gani cha mapinduzi ya kilimo yataweza kutokea katika Wilaya yetu. Naomba suala la matrekta liangaliwe kwa uangalifu mkubwa sana na kwa umakini ili uzalishaji wa chakula uweze kuongezeka katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika moja ya visumbufu ambavyo vimezungumziwa na Mheshimiwa Waziri ni panya na juzi wakati nafuatilia taarifa za habari, nilisikia Mheshimiwa Rais wetu akiwapongeza wananchi wa Mkoa wa Tanga kwa hatua kubwa sana waliyoichukua ya kuangamiza panya kwa asilimia themanini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, panya ana sifa moja kubwa, akioza anatoa harufu kali sana na sifa mojawapo ya mayai yakioza vilevile huwa yanatoa harufu kali sana.  Siku moja wakati nipo katika *laboratory* wakati nipo *form six*, tuliambiwa na Mwalimu wetu tutengeneze hewa ya *nitrogen.* Hewa ya *nitrogen* ina sifa ya kuwa na harufu kali inayofanana na harufu ya panya aliyeoza au ya yai lililooza.

Sasa katika utafiti wetu ule tukiwa *form six* tukagundua kwamba, mayai yana kiwango kikubwa sana cha protini na protini huwa inatengenezwa na vimelea vinavyoitwa *amino acids*.

Sasa kwa kuwa panya naye ana sifa ya kuwa na protini nyingi ndiyo maana harufu yake ni kali, kwa hiyo, maana yake ana *amino acid* nyingi na *amino acid* huwa zinatengenezwa na kimelea kinachoitwa *nitrogen* na *nitrogen* kwa wale wenzetu ambao wana utaalam wa *chemistry*, *nitrogen* ni kipenzi kikubwa sana cha mimea ndiyo maana unasikia *NPK.* Pale kuna *Nitrogen, Phosphate and Potassium*.

Sasa kwa kuwa panya ana *nitrogen* nyingi na panya huyu ana sifa ya kuharibu mazao, natoa shime au ushauri kwa watafiti wa kilimo wawakamate panya, wawakaushe, wawasage halafu unga ule utumike kama mbolea tuone matokeo yatakuwaje?  Naamini kabisa kama utafiti huu utafanikiwa, tutaweza kupata mafanikio makubwa mawili kwa wakati mmoja. Kwanza, tutawaangamiza panya na vilevile panya hao hao watatumika kurutubisha mazao yetu, tutapata mbolea. Hata wale ambao wanatumia kwa kitoweo, hawatatumia tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kutoa shukrani maana nitakuwa sina shukrani kama sitamshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na msaidizi wake Mheshimiwa Mathayo kwa juhudi kubwa sana walizozifanya mwaka jana kuhakikisha kwamba zao letu la korosho linapata bei ambayo ni *stable*, kuhakikisha kwamba soko

nalo linakuwa *stable*. Tunasema juhudi hizi zisiishie hapo, ziendelezwe ila suala hili la hati punguzo sijui inaitwa hati punguzo sina hakika.

**MBUNGE FULANI:** Vocha ya hati punguzo.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Vocha ya hati punguzo, nadhani mtiririko wake uangaliwe upya kwa sababu naona kama utaleta utata kidogo, hizi *signature* naona kama ni nyingi, ndiyo katika utekelezaji tunaweza kugundua kwamba, kuna matatizo fulani yamejitokeza na urekebishaji ukafanywa lakini kwa nini tusubiri tatizo litokee wakati baadhi ya Wabunge wameonyesha hisia kwamba linaweza kuleta tatizo? Naomba tuangalie upya utaratibu utakaotumika katika vocha hizi ili usilete usumbufu kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu umekwisha, naunga mkono hoja na nawatakia kila la kheri watumishi wote na Mama Mariam naomba ombi letu la trekta na mpiga kura wangu Juma Kuchapa kama ulivyoahidi mwaka jana kuwa mwaka huu utatuingiza kwenye bajeti naomba usisahau, nalo ulikumbuke. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Kilimo na napenda nianze kwa kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kwa sababu hotuba hii nimeisoma, inaleta matumaini katika suala zima la kuimarisha kilimo katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusoma Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005, kwa ruhusa yako naomba kusoma kama ifuatavyo: “Kilimo cha kisasa ndiyo msingi wa uchumi wa kisasa. Kilimo ndiyo msingi wa uchumi wetu na kina nafasi ya kimkakati katika *modernization* ya uchumi wa Tanzania. Kilimo cha kisasa ni sharti muhimu katika kujenga msingi wa uchumi wa kisasa.

Kilimo cha Tanzania kina matatizo yafuatayo:- Moja, wakulima walio wengi hawazijui na hawazitekelezi kanuni za kilimo bora cha mazao wanayoyalima, hivyo kilimo chao hakina tija na mavuno yao ni kidogo na mbili, wakulima wetu kwa wastani wanalima vishamba vidogo vidogo”. Naomba kuishia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilani hii, naomba nichanganye na “siasa ni kilimo” ambayo kaka yangu Mheshimiwa Makamba aliisoma jana, maelezo ambayo yametamkwa siku nyingi sana mwaka 1972. Lakini cha ajabu, sijui nitumie neno “ajabu” ama vingine vyovyote vile, miaka ya uhuru wetu sasa ni karibu miaka arobaini na saba, bado tunapoingia hapa Bungeni tunazungumza kilimo cha kusuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kuzungumza siku moja, tatizo letu kubwa pamoja na maelezo yote yanayoelezwa katika vitabu, hotuba zetu lakini utekelezaji wake ni mdogo sana. Leo hii mtaalam wa kilimo ama kiongozi yeyote yule anakwenda kwa

wakulima, anawakuta wakulima wanaotumia vingondola ama majembe madogo, anajishika mikono kiunoni, anahimiza kilimo:

"Enyi wakulima, ndugu wananchi, lazima tuendeleze kilimo chetu", anaondoka na kwa wale ambao wanapata posho wanaandika posho kwamba leo nilikwenda kijiji fulani kwenda kuhimiza kilimo cha kisasa. Anawaacha vile vile! Nafikiri hiyo ni ndoto ya alinacha, hatuwezi hata kidogo kuendeleza kilimo chetu kwa maneno matupu bila zana za kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikubaliane na wengi waliozungumza kwamba hapa iwe isiwe zana za kisasa ni matrekta, ni mbolea za kisasa, utafiti na mambo mengine yanayokwenda kisasa katika kilimo. Hatuwezi kuzungumzia *green revolution* bila kuwa na zana za kisasa.

Naomba basi, kwa kuwa haya yote yamezungumzwa katika kitabu hiki yasiishie katika kitabu hiki, tutekeleze kwa dhati, tuweke mkakati madhubuti wa kupata matrekta, tena nasema wala Serikali isiwe na wasiwasi, wakulima Watanzania wanajua nini maana ya kukopa na wanajua nini maana ya kulipa, wapo tayari wakopeshwe, watakuwa tayari kulipa mikopo hiyo kwa sababu watayatumia na watapiga hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja nilikuwa nazungumza na kiongozi mmoja katika nchi jirani jina nalihifadhi. Wao wamepiga hatua katika kilimo nikawauliza mmefanya nini? Akaniambia kama ni kwa utani au vipi, lakini naona ilikuwa ni kweli, akasema kwamba, mawazo yenu ndiyo tuliyoyatumia mpaka tukapiga hatua katika kilimo. Hii maana yake nini? Maana yake sisi ni hodari sana wa kuzungumza na kuandika, lakini tunapokuja katika utekelezaji tunagwaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuondoke hapo, tunaandika vizuri, tuzungumza vizuri, lakini tunakwama katika utekelezaji. Matarajio yangu ni kwamba, kwa sababu kaka yangu Mheshimiwa Stephen Wasira ana uzoefu mkubwa na nina hakika ana timu nzuri, tutakapokuja mwakani katika kipindi kama hiki kwa maelezo haya tutakuwa tumebadilisha kilimo chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu Waheshimiwa Wabunge wengine wamesema muache kukaa ofisini, mwende kwa wakulima mkawaone, mkajue matatizo yao, mkirudi muandike na myatekeleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara vijijini, huwezi kuzungumza kilimo kama hujazungumzia barabara za vijijini. Nasema hivyo kwa sababu gani? Kwa sababu kilimo hiki hakilimwi Mijini, kinalimwa vijijini ndiko waliko Watanzania zaidi ya asilimia 85. Leo wanalima, kama ni korosho, kama ni pamba ama zao lingine lolote lile, lakini wanashindwa kusafirisha mazao hayo kwa uhakika, wanashindwa kuyafikia masoko, nini matokeo yake? Mazao yataharibika, wananchi watakosa mazao hayo na kama yatafika sokoni bei itakuwa ya ghali kweli kweli!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwape mfano mzuri tu na mfano hai. Kule kwetu kuna sehemu moja inaitwa Chiwata, Chiwata ni hodari sana kulima nyanya, lakini wana tatizo kubwa la barabara ambayo ingewawezesha kusafirisha nyanya zao na kuzipeleka katika masoko ili waweze kubadilisha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu katika Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya TAMISEMI lazima watilie mkazo katika utengenezaji wa barabara vijijini ili tuweze kusafirisha mazao yetu kwa uhakika. Naomba hili walizingatie kweli kweli kwani litatoa mchango mkubwa kwa wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa mbolea bado ni tatizo. Tunazungumza mbolea ya ruzuku, upelekaji wa mbolea, lakini hivi sasa ninazungumza katika maeneo yetu, mbolea hiyo haijafika bado na hasa katika kipindi hiki ambacho wananchi kule kwetu wameanza kupulizia korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha kusikitisha kingine, kule kwetu kuna mtu mmoja anaitwa *Abbas Export*, kila mwaka ni huyo huyo tu, hivi tatizo liko wapi? Hakuna watu wengine ambao wanaweza kufanya hiyo kazi. Naiomba Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ifanye kila linalowezekana apatikane mtu mwingine ambaye atasambaza mbolea hiyo kuliko kumtegemea mtu mmoja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tumezungumzia asilimia ya *export levy*, tunashukuru kwamba tumepata asilimia 6.5. Lakini tunachoomba, kama walivyoahidi Wizara, fedha hizo ziondoke pale ziende moja kwa moja kwenye Halmashauri zetu ili ziweze kutumika katika kuendeleza kilimo chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, kuna fedha za Serikali zinabaki hapa. Tunaomba hizo fedha zinazobaki asilimia 3.5 zipelekwe katika Vituo vyetu vya *research* ili ziweze kusaidia kufanya utafiti ili tuboreshe kilimo chetu. Maana wakati mwingine hivi Vituo vya *research* vinashindwa kufanya kazi kwa sababu ya fedha kidogo kutoka Serikalini na kama hakuna *research*, hatuwezi tukabadilisha kilimo chetu, hatuwezi kuwa na nguvu ya kwenda kwa wananchi kuzungumzia kilimo cha kisasa. Kwa hiyo, naomba hiyo asilimia 3.5 ipelekwe katika Vituo vya kufanyia *research*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho Benki ya Wakulima, tusidanganyane, hakuna benki hata moja mpaka hivi sasa tunazozijua wote sisi ambazo zipo tayari kutoa mikopo kwa wakulima. Naiomba Serikali ifanye kila linalowezekana kama wanavyofanya wenzetu wengine katika nchi nyingine Benki ya Wakulima ianzishwe mara moja. Hatuwezi kulima kwa kubahatisha. Hao wenye mabenki wamekuja kufanya biashara tu, hawakuja hapa kuwaendeleza wakulima wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana suala hili lisitazamwe kwa jicho la pembeni, macho yote yatazame hapo ili Benki ya Wakulima iweze kuanzishwa. Mimi mwenyewe hapa nina mfano!

*(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Castor Ligallama atafuatiwa na Mheshimiwa John Momose Cheyo.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote wa Wizara ya hii kwa hotuba nzuri katika Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kilombero kwa kunipa ushirikiano mpaka hivi sasa katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nitaanza kuchangia kwa kunukuu Ilani ya CCM: "CCM itazitaka Serikali kuongeza msukumo katika kuvutia uwekezaji katika mashamba makubwa ya kilimo cha biashara."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuongelea hapa ni dhana ya hii ya uwezeshaji. Dhana ya uwezeshaji ni dhana mtambuka kwa maana kwamba mwekezaji akiwepo pale wananchi wanaomzunguka watachukua ujuzi alionao kama ni umwagiliaji watu watapata ajira kama na wao kushiriki katika kilimo watatekeleza MKUKUTA, kama watatoa huduma za jamii kama shule na hospitali, wananchi watapata hospitali zaidi kuliko ilivyokuwa kabla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika Ilani ya CCM inavyosema kwamba Serikali itatoa msukumo, sasa ukiangalia msukumo, msukumo ni nini? Msukumo ni kwa maana kwamba iweke mazingira ambayo yatawezesha uwekezaji uwepo na mazingira siyo mengine, hao wawekezaji ni wafanyabiashara, hawezi kuja hapa, anataka kuwekeza kwenye kilimo ukampeleka kwenye pori fulani kwamba tunataka ulime hapa. Ndiyo maana utakuta wote waliokuja wamewahi sehemu ambazo miundombinu tayari ipo. Kwa mfano, viwanda vya sukari, viwanda vyote vilivyojengwa zamani. Lakini siyo sehemu pori ukamwonyesha kwamba anza hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua hilo, mwaka jana katika kuchangia kwenye bajeti, niliiomba Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini na kupitia Wizara ya Miundombinu kwamba nina fursa katika Wilaya yangu na Waheshimiwa Wabunge wengi wameliongelea, nina mito zaidi ya 40 haikauki.

Nina uhakika wa mvua kwa sababu tumeahamisha wananchi wetu kutoka milima ya Udzungwa**,** tukatengeneza *catchments rain forest*. Mimi nina ardhi nzuri yenye rutuba, nina wakulima wa kutosha kufanya kazi. Kwa hiyo, nikasema kwamba sasa Serikali

iweke msukumo kwa kuweka miundombinu mingine ambayo haipo kama umeme na barabara ili mwekezaji avutiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umeme nilijibiwa kwamba akija mwekezaji mwambie aombe, ndiyo msukumo huo. Kuhusu barabara nikaambiwa Serikali haina mpango. Sasa uwekezaji utakuwa hauna maana. Kilimo hakitatusaidia ikiwa fursa hizi hazitumiki na huwezi kuzihamisha pale kama hutaki kuwekeza katika kilimo katika Wilaya ya Kilombero, huwezi kutoa zile fursa uweze ukaichukua Ilani ya CCM ukaipeleka mahali pengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwa kuhifadhi yale maji ndiyo unakuta hata umeme unakuwa wa uhakika, mabawawa yanajaa kwa sababu ya *catchment* ya msitu ule. Labda na sisi baadaye tuanze kuitoza Serikali. Kwa sababu ikiwa wenzetu wa madini, kwa kuwa madini tu wanalipwa *dollar* 200,000 kwa kila mwaka na sisi basi tulipwe kwa kuhifadhi maji yale ambayo Serikali kwa makusudi haitaki kuyatumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mashamba zaidi ya manane yenye hekta zote ukijumlisha zaidi hekta 1,000, hiyo njaa mnayoizungumza itatoka wapi? Ni sehemu moja tu ingeweza kutulisha, sasa ukichanganya na huko alikosema ndugu yangu Mheshimiwa Jackson Makwetta, basi hakuna haja ya kutafuta chakula tena nje ya nchi. Sasa tusipofanya kwa makusudi hilo, basi hakuna haja ya kulalamika kwamba tuna njaa au nini na nini? Hilo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, napenda niishukuru Serikali, nililalamika sana tangu Bunge la kwanza kabisa mwaka juzi juu ya kugeuza shamba ambalo lilikuwa linalimwa michikichi lilimwe mpunga. Sasa napenda niishukuru Serikali, imesikia kilio cha wananchi wa Kilombero lile shamba sasa litalimwa mpunga. Kwa niaba ya wananchi wale, tunaishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe angalizo ambalo nitamwomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hoja yake awahakikishie wananchi wa Kilombero. Wakati Serikali inabinafsisha mashamba ya Kilombero, kwa vile shamba la Kilombero lilikuwa la kwetu sisi Serikali ndani ya mashamba yale tuliweka vijiji vyetu, kijiji cha Nyange, Magombela na Msolwa stesheni.

Sasa tulivyowakabidhi wawekezaji Kampuni ya Ilovu hatukutoa vile vijiji katika eneo lile na wenzetu wapo makini kuja kuangalia *beacons* za shamba wakakuta ndani ya shamba lao wakakuta ndani kuna vijiji vitatu. Kwa hiyo, baada ya mazungumzo na Serikali wakadai fidia ya ardhi ile na ni kijiji kimoja tu cha Nyange walikubali kibaki, lakini wananchi wengine walipata usumbufu wa kuhamishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda katika shamba hilo ninaloliongelea la Kotako ambayo sasa litalimwa mpunga, Serikali itusaidie kitu kimoja. Kwanza, napenda ku-*declare interest,* mimi ni mwananchi katika kijiji cha Lukolongo, Kitongoji cha Mbasa ndiko nilipozaliwa na baba yangu alizaliwa katika kitongoji hicho. Hao

wananchi wa Mbasa ni kilomita tatu kutoka Makao Makuu ya Kata, walihamishwa mwaka 1974 kuja kusaidia ulinzi wa Reli ya *TAZARA*, lakini mashamba yao yakabaki katika kitongoji cha Mbasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu, kwa sababu shamba tayari wamekwishasaini Mkataba tarehe 4 Julai, 2008 na *RUBADA*, bahati mbaya Mwanasheria wa Wizara sikumwona siku ile, lakini Wanasheria wa Kampuni inayokwenda kulima pale alikuwepo, kukawa na makubaliano.

Mimi kama Mbunge, nililitoa hilo kwamba wale wananchi walihamishwa mwaka 1974. Baada ya mambo ya kulinda reli ya *TAZARA* kwisha walirudi kwenye mashamba yao na kwenye kijiji chao cha asili wanalima. Lakini wao katika kupima mwaka 1977 wakawa-*include* wale wananchi kwa kuchukua na eneo la kile kitongoji na wakawaandikia barua wahame juzi juzi hapo. Kwa hiyo, wakanipigia simu Mbunge wao tukafanya maongezi pale na Kampuni na *RUBADA* tukakubaliana kwamba wale wananchi wasihamishwe badala yake itafutwe ardhi nyingine mbadala ya kufidia eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachomwomba Mheshimiwa Waziri, naye awahakikishie wananchi wanaonisikiliza na tangu juzi na jana wananiuliza juu ya hili jambo kwamba watabaki pale kwa sababu wana mazao yao kama minazi, miembe na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni ombi kwa sababu wao watakuwa kama *out growers,* wanamzunguka mwekezaji ndiyo uwekezaji tunaoutafuta siyo ule wa kutafuta ajira tu kwa mwekezaji uende ukalime kama manamba. Tunatafuta wawekezaji ambao mkulima wa nje anajifunza kutoka kwa mkulima wa mtaalam mwekezaji na miundombinu ile anaitumia yule mkulima mtaalam, anampa na yule mwekezaji wa nje. Vile vile itajenga mahusiano mazuri kati ya wenyeji na hawa wanaokuja kuwekeza. Kwa hiyo, hilo naomba Mheshimiwa Waziri anihakikishie wakati anajumuisha ili wananchi wale waweze kutulia kwamba watabaki kwenye Kitongoji cha Mbasa katika Kijiji Lukolongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni zana za kilimo. Watu wetu kule Wilaya ya Kilombero wamehamasika sana katika kutumia zana hizi za kilimo, matrekta madogo madogo ya *power tillers* na wanyamakazi kwa wenzetu wafugaji ambao wako kule. Nimeongea na kampuni mbalimbali pale Dar es Salaam wanachoniomba ni Mheshimiwa Waziri anipe barua tu ya utambulisho. Anitambulishe kwenye kampuni ambayo nitakupa anuani yao ili nikienda tuna makubaliano fulani ambayo nitakueleza Waziri ili niweze kuwapatia zana hizo wananchi wangu kwa njia ya mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenyewe nitachanganua miradi hiyo, nitajua vikundi nitakavyovipa ambavyo vina uhakika wa kulipa ili tuingize matrekta hayo ya *power tillers* kwa mfano 100 kwa pamoja, nina Tarafa tano angalau kila Tarafa ziwekwe trekta 20 za kuanzia. Kwa hiyo, tukianza na matrekta 100 nina uhakika kutakuwa na mabadiliko na tukiunganisha na ugani sasa wa kueleza utaalam wa kupanda mbegu, kanuni bora za

kilimo nafikiri tutabadilika. Hayo mashamba makubwa ambayo tunayasubiri kupata wawekezaji tunaweza kuzalisha mpunga tani 300,000. Kama tutalima mara mbili tani 600,000 kwa mwaka, kwa hiyo, kutakuwa hakuna haja ya kuagiza mchele kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba hao wawekezaji, wametuhakikishia wataweka maghala na kwa hiyo, mtindo wa stakabadhi ghalani, utatumika na wananchi watakuwa na uhakika wa bei nzuri ya mazao yao pindi wakimaliza kuvuna. Kwa hiyo, kabla hatujamaliza Bunge hili Mheshimiwa Waziri anipatie hiyo barua, wanachohitaji ni *introductory letter* kwenda kwenye kampuni hiyo ni hawa waliokuja kutuonyesha hapa *power tiller* ndiyo wale nimekubaliana nao, wanachoomba ni barua yake mengine nitaendelea nayo mimi mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sina la zaidi, ninaunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuongea juu ya Wizara hii muhimu kwa sisi wote, nakushukuru sana. Awali ya yote nataka kutoa pongezi zaidi kwa wakulima wa pamba mwaka huu, kweli wanapaswa kusifiwa sana kwamba mwaka jana waliweza kupata tani 200,000 na mwaka huu wameongeza karibu mara mbili tani 432,000.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri alikuwa anatafuta mahali ambapo anaweza kuona mfano wa wakulima kuweka juhudi na kuongeza pato kwa pamba wakulima wengi wa pamba wameonyesha inawezekana. Sasa tatizo na najua Waziri alijua kwamba na mimi nitazungumzia juu ya pamba tu kwa sababu ndiyo walionituma hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ambalo ninaloliona kwa mambo ya pamba ni kwamba Serikali inawahamasisha wakulima, lakini haijiandai. Wakulima mwaka uliopita walipata Sh. 500/= wakaona hapa ndiyo mahali pa kuponea kwa msimu huu au kwa kilimo cha mwaka 2007/2008 wakaweka nguvu yao yote na wakalima mashamba yao mengi na wengine hata walithubutu kuchanganya mahindi pamoja na pamba kuhakikisha kwamba mwaka huu wanapata pamba nyingi sana. Hilo limefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Serikali imefanya nini? Kwanza, kwa upande wa wanunuzi panakuwa na benki moja tu ndiyo ambayo inatoa mikopo. Kwa mara ya kwanza tunaanza kuona kwamba benki yenyewe ndiyo inaamua wale wanaonunua wanunue kwa bei gani. Sababu ambazo tunazopewa ni za ajabu. Wanunuzi hao wamepata hasara mwaka uliopita. Kwa hiyo, kama walipata hasara mwaka uliopita, ndiyo kusema sasa wachukue hasara zao wakulima maskini waweze wakazifidia hasara zao. Haya ni mawazo ya wapi? Serikali iko wapi kuangalia mawazo kama haya ndiyo yanatawala zao kama pamba?

Mimi naiomba Serikali mara moja waiambie bei ya *CRDB* iache kuweka ukiritimba ndani ya zao la pamba. Wao wako katika biashara ya kutoa fedha. Kama wanaona kwamba zile fedha zao zitapotea, basi waachie benki nyingine na Serikali ihamasishe benki nyingine ili waweze wakatoa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa ni kwa nini iwe benki moja tu? Lakini nimeambiwa kwamba benki nyingine ambayo ingeweza kuingia pale ni *TIB* Benki ya Serikali. Lakini naambiwa haiwezi kuingia katika pamba kwa sababu *TIB* haina Bodi. Ndio maana nasema kwamba Serikali haijiandai. Serikali ilijua kwamba mwaka huu kutakuwa na *bumper crop* kutakuwa na pamba na nyingi, sasa kwa nini isijiandae kuhakikisha kwamba fedha ya kununua hilo zao ipo?

Kwa hiyo, Serikali ndiyo inawakwamisha wakulima na mimi nashawishika kabisa kuungana na Wabunge wengine kwa shilingi chini ya mia tano, hailipi, ni afadhali kulalia pamba. Kama tutauza mwaka unaokuja, bila shilingi mia tano, hakuna pamba. Hili nataka lijulikane kabisa na nashukuru wakulima wengi ambao wameliona hili, mkulima yeye anaambiwa kwamba akitaka mbegu Sh. 250/=, auze pamba yake kwa Sh. 400/=! Sasa abakie na kitu gani? Ukienda kwenye pembejeo na yenyewe ni hela kibao. Kwa hali hii, kaeni na pamba yenu mpaka mwaka kesho na tuone ma-*ginners* watakula mchanga au watakula kitu gani. Naomba mlichukulie kama ni jambo ambalo ni la dharura kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sioni tatizo kwamba Serikali hii mara nyingi inatoa ruzuku eti kwa kusema kuendeleza ushirika. Mwaka uliopita wametoa shilingi bilioni 6.8 kwa sababu eti *SHIRECU* ilikuwa na madeni. Sasa kama *SHIRECU* inakuwa na madeni, wenyewe muwafuatilie kwa nini wamekuwa na madeni ya namna hiyo. Kama wamepoteza hela, muwafuatilie ni kwa nini wamepoteza fedha, siyo kusema *okay* ahsante vijana, vizuri mmepoteza fedha hizi, nawaongezea nyingine. Hii siyo biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna fedha ya kuweza kutoa ruzuku kwa pamba, basi iende kama ruzuku ya kuweza kufaidia bei ya pamba. Lakini haitoshi, bado tumeona kwamba hata Benki Kuu imeweza kuchangia katika kuharibu bei ya pamba mwaka huu kwamba tumeona mwaka uliopita kwamba bei ya dola ilikuwa karibu Sh.1,200/=. Benki Kuu inazidi kuteremsha siku hadi siku, mpaka leo nilikuwa naangalia iko kwenye Sh. 1,150/=. Sawa, kila mmoja anataka shilingi ambayo ina nguvu. Lakini basi unaangalia kwa upeo kama kipindi hiki ndiyo wakati ambapo wakulima wanauza pamba yao kuna njia mbalimbali ambayo mtu anaweza akafanya. Benki Kuu wanaweza wakaamua kwamba wawe na *forward purchases* au wanunue dola kwa *special rate* kwa wakati fulani hii ita-*stabilize* bei. Lakini wewe upande huu una benki moja ambayo inatoa mikopo, Benki Kuu yenyewe na yenyewe ndiyo inateremsha *exchange rate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo kusema mkulima huyu ambaye ndiyo anatoa *foreign exchange* ya kununua mafuta ya kununua dawa, haonekani kwa Serikali kama mshiriki mkuu katika uchumi wa Tanzania. Kwa hiyo, ombi la kwanza nataka Serikali iwaangalie wakulima wa pamba ili kuhakikisha kwamba wanapoanza kulima na wenyewe wanajua watakuja kulipwa hela ngapi na hii inawezekana kabisa.

Mkulima mwaka jana alitegemea Sh. 500/= hata na Mheshimiwa Rais alipokuwa anatembea sehemu zile tunakolima pamba alipokuja Bariadi, alipokwenda Shinyanga na yeye alisema wananchi endeleeni kulima pamba, tutajitahidi angalau bei isiwe chini ya

Sh. 500/=. Sasa leo Sh. 420/=. Kaeni na pamba. Tayari nimeshaanza kuona kwa kukaa na pamba yetu bei imeaanza kuongezeka. Ninavyozungumza sasa, imefika Sh. 450/=. Tung'ang'ane hapo mpaka Sh. 500/=. *No TShs.500/= no cotton.* Ndiyo hali halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hivyo tu, nataka pia kuchukua nafasi hii kuweza kuishukuru Serikali sana kwa kuona kilio cha kitabu cha pembejeo. Kitabu cha pembejeo hiki na Mheshimiwa Stephen Wasira na yeye kwao wanalima pamba na wanamsikiliza wakulima wake. Kilikuwa ni kitabu cha kuwaibia wakulima. Wewe unakatwa Sh. 100,000/= unapewa dawa ya Sh. 50,000/= halafu ndiyo fedha zimepotea. Nashukuru sana kwamba Serikali imeona kwa msimu huu na natumaini siyo kwa msimu huu na kuendelea kitabu hiki kifutwe kabisa. Mimi katika mikutano yote ambayo nimewatembelea wakulima ukiwauliza jambo la kitabu cha pembejeo kinaitwa *pass book* kifutwe watoto wote wanawake, wanaume walikuwa na kauli moja tu kifutwe na mimi nashukuru kwamba hili limefanyika kwa hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini huo siyo mwisho, bado tunataka pembejeo. Kwa hiyo, kitu ambacho nilikuwa nategemea kwa Serikali kabla hatujaanza msimu mwingine ni kwamba watueleze ni utaratibu gani mbadala ambao wanatuletea mapema kabla hatujaanza kulima tujue kwamba mwaka huu tutapata pembejeo kwa msingi ambao unaofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kusema kwamba Serikali ijiandae bila kuambiwa utaratibu mbadala ndiyo kusema wakulima wengine watatumia hela zao kwa mambo mengine labda wakitegemea ruzuku tu. Namwomba Mheshimiwa Waziri atamke wazi kabisa: Je, mwaka huu tutafanya namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu mkulima. Mimi bado nafikiria kwamba Serikali haijatengeneza mawazo yake sawa sawa juu ya mkulima. Mimi nataka kusema kwamba Serikali imwone mkulima kama mtu binafsi ambaye ana shamba lake analotegemea, anaweza kufanya maamuzi ambayo yanamfaa katika shamba lake hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado leo kila wakati sheria, tuchukue sasa hivi sheria mbona imetangazwa na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwamba hakuna kupeleka chakula nje sawa inaeleweka ni kwa nini. Lakini kwa nini sheria hii ije wakati wa mavuno? Ni afadhali kama kuna utaratibu wa namna hiyo tuelezwe mapema ili mtu ajue kwamba mwaka huu badala ya kulima ekari 50, basi alime ekari 20 tu, kwa sababu hii itakuwa ni kwa *local market*. Lakini leo tayari tunaambiwa kwamba hakuna kupeleka chakula na chakula chenyewe Mheshimiwa Waziri hajasema kuna chakula cha kila aina, kuna mahindi, kuna ufuta, kuna karanga, karanga sasa kule Bariadi zinaoza, ufuta kule Bariadi unaoza hakuna soko.

Soko tunajua lililopo liko Kenya, sasa ukituambia tusipeleke, tutafanya nini? Kama wewe unaona tusipeleke, basi Serikali ije itununulie ufuta. Serikali ije itununulie karanga ambazo tulizonazo. Hatujazungumza juu ya mambo ya viazi, hiyo watu watakula, lakini tunachotaka kusisitiza hapa ni kwamba kilimo ndio chanzo cha maisha

cha mkulima. Kwa hiyo, maamuzi ambayo sio sawa sawa Serikali ijiangalie. Siku hizi mimi kule ninakotoka tuna ugomvi sana na Mabwana shamba. Wao wanasema kwamba watu wasichanganye pamba pamoja na mahindi. Wananchi wananiambia Mheshimiwa Mbunge tukichanganya mahindi na pamba, ndugu yangu tunapata pamba na tunapata mahindi. *DC* ameng'ang'ania pale, *DC* anamweka mtu ndani kwa sababu ya mambo kama hayo ya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mimi nikipata pamba ambayo iko pungufu kwani wewe una hasara gani? Kama nisipopata mahindi, wewe una hasara gani? Pamba ni yangu, mahindi ni yangu shamba ni langu, nguvu ni zangu wewe ikakukera mpaka uanze kunikamata kwa sababu ya shamba langu, hiyo kitu inatoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka mkulima aheshimiwe, mkulima aone kwamba yeye pia ana maamuzi ambayo yanayomfaa. Kama Serikali imeamua kabisa kwamba kutochanganya italeta tija, basi watupe shamba darasa. Kama hakuna shamba darasa, tuache tufanye vile ambavyo tunafanya na mwaka huu tumefanya vizuri, tumeongeza maradufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu stakabadhi ghalani, hili limeelezwa kwa ufupi na Mheshimiwa Waziri. Mimi nataka kutahadharisha tu, kwamba korosho ni tofauti na pamba. Pamba hatuuzi kwenye masoko ya nje kama *seed cotton*, tunauza *lint.* Kwa hiyo, katikati pale kuna jina.

Kwa hiyo, jambo hili liangaliwe kabisa kama tutabakia kwa sababu CCM inapenda sana ushirika, mturudishe tena kwa mnunuzi mmoja anayeitwa ushirika, hatutalima pamba, tutakwenda kulima mpunga, ufuta na kadhalika. Mliangalie, tulikuwa tumefika ambapo watu wote wanaolima wanapata *cash.* Ndugu yangu nataka majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Cheyo kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa James Daudi Lembeli. Mheshimiwa Lembeli tafadhali tuhitimishie.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa mwisho jioni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba ya bajeti nzuri imeandaliwa vizuri na kwa kweli kama itatekelezwa kwa jinsi ilivyoandikwa, nina hakika wakulima wa Tanzania wataweza kupiga hatua mbele na hivyo kilimo kuchangia kwa stahili yake katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wengi wamezungumza mambo mengi ambayo ningependa niyazungumze. Kwa hiyo, mimi nitajikita katika zao la pamba. Kwanza, napenda niipongeze Serikali kwa kufuta mfumo ule wa *passbook*. Mfumo huu

ulikuwa ni mfumo dhalimu, kazi yake kubwa ilikuwa ni kumhujumu mkulima, kumwibia mkulima na mkulima hakuwa na mahali popote pa kulalamikia.

Nashukuru kwa sababu Serikali imeliona hilo na kufuta huo mfumo ni dhahiri, imetambua kwamba wakulima walikuwa wanahujumiwa.

Ninaomba sana Serikali wale wote ambao walikuwa wamejikita katika kumdhulumu mkulima, naomba sana Serikali iwatafute popote pale walipo waadhibiwe au warejeshe fedha ambazo kwa namna moja au nyingine walizichukua bila ya ridhaa ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Shinyanga unazalisha asilimia 60 ya pamba yote inayozalishwa nchini. Jimbo la Kahama liko ndani ya Mkoa wa Shinyanga na lina wazalishaji wengi wa zao la pamba. Hivi ninavyozungumza pamba imejaa katika maghala ya wananchi ya wakulima kwa sababu hawataki kuiuza kwa bei ya Sh. 420/=.

Wiki iliyopita nilipokuwa katika jimbo langu, bei ilikuwa Sh. 400/= na katika Kata za Uyogo, Kisuke na Kinamapula niliweza kushuhudia mwenyewe kwa macho yangu pamba nyingi ikiwa bado iko mashambani na nilipohoji ni kwa nini pamba bado iko shambani waliniambia, Mheshimiwa Mbunge usituulize swali hilo sisi hapa. Sisi tunapashwa tukuulize wewe bei ya Sh. 420/= haifai na ni sawasawa na kumwibia mkulima wa pamba. Sababu wanazotoa ni za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani mbegu zilikuwa zinagawiwa bure. Leo hii mbegu lazima ununue. Kilo moja Sh. 250/= na unahitaji zaidi ya kilo 20 kupanda ekari mbili au tatu, ni fedha nyingi. Lakini mkulima anakwambia unaponunua pamba yangu kwa Sh. 400/= maana yake ni kwamba nafanya kazi ya mwaka mzima kwa Sh. 150/= kwa kilo. Lakini hapo hapo anakupa mahesabu anasema mimi nikimwuuzia huyu mnunuzi pamba yangu kwa Sh. 400/= kwa kilo yeye atatoa mbegu, ataniuzia mimi kwa Sh. 250/=, atatoa mashudu anatengeneza mafuta. Mafuta ya pamba sasa hivi hata huko Shinyanga yanakozalishwa mkulima wa kawaida hawezi kuyanunua yako bei ya juu. Wanatoa mashudu hasa mkulima anaulliza, mimi kwa kunipa Sh. 420/= Serikali inafikiria nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha kuona kwamba nguvu ya wananchi katika maeneo mbalimbali ya Jimbo la Kahama na naamini Wilaya yote ya Kahama inapotea bure hivi leo. Wakulima wamejaza pamba yao kwenye maghala majumbani kwao, wakisubiri labda bei itafikia angalau Sh. 500/=. Kwa iliyo mashambani hivi sasa hawaivuni kwa sababu hawana pa kuiweka.
Sasa nilikuwa naomba sana Serikali, suala la bei ya pamba hivi ni kwa sababu gani Serikali wala haina utaratibu wa kumhakikishia huyu mkulima? Mimi sioni tatizo liko wapi?

Kidogo ninapingana na mzee wangu Mheshimiwa Cheyo kuhusu mfumo wa stakabadhi ghalani. Mfumo huu ukiandaliwa kwa utaratibu mzuri utaweza kuipandisha bei ya pamba kutoka pale ilipo mpaka kufikia hata Sh. 800/=. Kinachohitajika hapa ni elimu kwa wananchi, lakini pia kufahamu hayo malipo ya pili na ya tatu yatapatikana

vipi. Lakini kama mbegu pia zitathaminiwa na mashudu yatakayopatikana na mafuta na mkulima alipwe, ninaamini bei ya pamba itafaa kidogo kwa wakulima wa zao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la pamba kwa Mkoa wa Shinyanga kama bei hii itaendelea kuwa hivi ilivyo leo ni bomu mwaka 2010. Mwaka 2005 wakati wa kampeni Rais mwenyewe alisema kwamba tutahakikisha tutajitahidi bei ya pamba iimarike. Kweli mwaka 2006 bei ya pamba ilipanda kidogo Sh. 300/= hadi Sh. 400/=. Mwaka jana Sh. 500/= hadi Sh. 550/= na mwaka huu Sh. 400/=. Sasa tunaelekea wapi? Ni vyema basi, Serikali ikawaambia kabisa, ninaamini kwamba wataalamu wa Bodi ya Pamba wanaweza kuelewa mwenendo wa bei ya pamba mwakani wawaambie wakulima sasa ili waamue walime au wasilime kulikoni kupoteza nguvu zao hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kabisa Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajumuisha hotuba yake anihakikishie kama kweli wakulima wa pamba wa Wilaya ya Kahama, Bukombe na Uyui ambao walikopwa tangu mwaka 2004 hata mimi sijaingia hapa Bungeni kila mwaka wanapewa ahadi kwamba Serikali imemaliza kuhakikisha madeni watalipwa.

Naomba hii iwe mara ya mwisho kuwadanganya wakulima. Najua wakulima wa maeneo mengine ya pamba ambao walikuwa wanadai Vyama vyao vya Ushirika wamelipwa, tatizo ni nini kwa wakulima wa zao la pamba wa Kahama? Inavyoelekea, Serikali haiwaonei huruma watu hao.

Leo nimepata zaidi ya simu 20, wanauliza Mheshimiwa Lembeli tunataka kusikia unaulizia, lini tutalipwa deni letu? Maana yake sasa kwa miaka miwili au mitatu ya nyuma wanadanganywa kila mwaka na barua ninazo kutoka Wizara ya Kilimo kuanzia enzi za Naibu Chibulunje mwaka jana, hivyo hivyo na mwaka huu nimeuliza hapa, jibu watalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa nijue mawili, wawaambie wenyewe Serikali iwaambie wakulima wenyewe kwamba mtalipwa au hamtalipwa wasahau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu jambo hili linanikera, ningependa niishie hapo. Lakini nitataka kumsikia mzee wangu Mheshimiwa Wasira atoe kauli ya mwisho juu ya ahadi ya kila mwaka ya wakulima wa pamba ambao walikopwa pamba yao, ilichukuliwa na ikauzwa. Kuna watu hapo katikati wamekwishapokea fedha, mkulima bado anahangaika huko kijijini kwa Sh. 20,000/= au Sh. 30,000/=, jamani Serikali iwaonee huruma hawa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono hoja hii baada ya kusikia kauli hiyo ya Mheshimiwa Waziri kuhusu madeni ya wakulima wa pamba wa Wilaya ya Kahama ambao walichukuliwa pamba yao mwaka 2004. Nakushukuru, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lembeli. Waheshimiwa Wabunge, huyu anatuhitimishia michango kwa hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Kesho baada ya Maswali Mheshimiwa Waziri ataanza kuhitimisha, nafikiri

ataanza kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri halafu baadaye atakuja Mheshimiwa Waziri mwenyewe kuweza kujibu hizi hoja mbalimbali ambazo zimetolewa na Wabunge katika hizi siku mbili ambazo tumekuwa nazo na hatimaye hii hoja itahitimishwa na jioni tuweze kusikiliza hotuba ya Wizara nyingine.

Kwa kuwa hatuna matangazo na muda umeshakamilika, napenda niahirishe Bunge mpaka kesho tarehe 24 Julai, 2008 Saa tatu Asubuhi.

*(Saa 01.43 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,
Tarehe 24 Juni, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*